SIRI PART 2

MAISHA NA KIFO CHA MELANIE CHUMA

SEASON 8

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

1.MISS TANZANIA
2.I WAS WRONG
3.TEN CHAPTERS
4.I DO
5.SERENA
6.BEFORE I DIE
7.BEYOND PAIN
8.PENIELA
9.QUEEN MONICA
10.THE FOOTBALL
11.I DIED TO SAVE PRESIDENT
12.KIAPO CHA JASUSI
13.KIKOSI CHA SIRI
14.SIRI

MAWASILIANO
0764294499

ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

“Mheshimiwa Rais umenistua uliposema kwamba James Kasai anatakiwa kupatiwa nafasi ndani ya serikali itakayoundwa baada ya mapinduzi kufanyika”akasema Paul

“Sikiliza Paul.Ushiriki wa James Kasai katika suala hili ni muhimu sana.Yeye ndiye atakayemuua Rais Patrice Eyenga.Jeshi la Congo halitahusishwa katika lawama yoyote ya kumuua Patrice Eyenga.Mzigo wote ataubeba James Kasai na mara tu itakapotangazwa kwamba Rais

Patrice amefariki jeshi litatangaza kushika nchi” akasema Jenerali Akiki

“Mpaka hapo kidogo ninakuelewana na mpango huo ni mzuri lakini tatizo liko hapo kwa James Kasai.Japo tunaweza kumtumia katika mpangowetu lakini si mtumzuri kushirikiana naye na hapaswi kupewa nafasi ndani ya serikali kwa sababu ndiye atajulikana na dunia nzima kuwa amemuua Rais Patrice.Tutakuwa ni watu wa ajabu sana kama tutampa madaraka mtu aliyemuua

Rais.Mtu huyu tayari anajulikana ni gaidi na kwa namna yoyote ile hapaswi kushika nafasi yoyote ya madaraka” akasema Jenerali Mutombo na kumtazama Rais Akiki

“Fikiria wewe mwenyewe mheshimiwa Rais jambo hili.Tutachekwa na hata ndege wa angani kumpa James madaraka yoyote ndani ya serikali mtu ambaye dunia nzima inamjua ni gaidi na amekwisha fanya ukatili mkubwa sana”

“Unalolisema Jenerali Mutombo ni jambo la kweli.James Kasai ameharibu sana kushirikiana na magaidi wa IS.Juhudi zote alizozifanya kwa miaka mingi kupambana kwa maslahi ya Congo zimeharibiwa na kitendo chake cha kujiunga na magaidi wa IS.Hata hivyo tunamuhitaji katika mpango huu na kama akishirikiana nasi hatuwezi kumuacha hivi hivi lazima naye afaidike na mapinduzi hayo” akasema Jenerali Akiki

“Mheshimiwa Rais nashauri kila mmoja akatafakari zaidi jambo hili na tuwe tena na kikao kingine ambacho kitatupa mwangaza zaidi.Umekuwa ni mwanzo mzuri.Naomba tukutane tena baada ya siku tatu tuendelee na mjadala huu” akasema Jenerali Mutombo

“Sawa Jenerali Mutombo nakubaliana nawe Tukutane tena baada ya muda huo.Tafadhali tujitahidi kulitafakari kwa kina suala hili ili tutakapokutana tuweze kuzungumza lugha moja halafu

tuanze mchakato rasmi” akasema Jenerali Akiki na kuagana na Jenerali Mutombo akaondoka

“Jenerali Mutombo yuko sahihi kuhusu James Kasai.Ni ukweli ulio wazi aliharibu sana harakati zake pale alipojiunga na kikundi cha kigaidi cha IS.Sifa yake ilibadilika kutoka mpambanaji hadi gaidi.Haitawezekana kumpa madaraka ndani ya serikali pale yatakapofanyika mapinduzi.Nitazungumza naye na kumfahamisha kwamba

suala la urais halitawezekana tena” akawaza Jenerali Akiki

ENDELEA……

Kengele ya mlango wa chumba cha Melanie Davis ililia akainuka na kwenda mlangoni akakutana na jamaa wawili waliovalia suti nzuri wakamtaka ajiandae kwani Rais anahitaji kuonana naye usiku ule

“Nadhani Jenerali Akiki anataka kunipa mrejesho kuhusiana na lile suala tulililoliwasilisha kwake jana kwani aliahidi kutupa mrejesho leo” akawaza Melanie wakati akijiandaa.Alivaa haraka haraka suti ya rangi ya kijivu akachukua mkoba wake na kuongozana na wale jamaa hadi katika gari wakaondoka

“Natamani sana kujua maendeleo ya Gosu Gosu lakini siwezi kumpigia Austin kwani sitaki ajue kama niko Uganda.Sitaki afahamu mambo

yangu.Ngoja nikamsikilize kwanza Rais nijue kuna nini anataka unieleza halafu nitajua kama ntarejea nyumbani kesho au nitaendelea kubaki hapa hapa Kampala” akawaza Melanie akiwa garini

“Kuna wazo limenijia mchana wa leo na sijui lilitoka wapi lakini ni wazo ambalo naona kama lina msingi.Ninampenda sana Gosu Gosu na nimeumizwa na kitendo cha kupigwa risasi lakini ni vipi kama Gosu Gosu atazinduka na kisha

akamueleza Austin kwamba nilikuwa nimemtuma kwenda Paris kuua mtu? Austin lazima atakuwa na wasiwasi nami na wanaweza wakaanza kunichunguza na kama hilo likitokea kuna uwezekano wakanifahamu mimi ni nani.Sitakiwi kuliruhusu hilo litokee lazima niwe mwepesi sana katika kuchukua tahadhari mapema kabla mambo hayajaharibika.Hapa kuna kitu kimoja tu ambacho kinatakiwa kifanyike nacho ni kumuua

Gosu Gosu” akawaza Melanie na kufumba macho

“Oh my God ! akajikuta ametamka kwa sauti na wale jamaa aliokuwa nao garini nao wakastuka

“Madam are you okay?akauliza mmoja wao

“I’m okay” akajibu Melanie

“Kila ninapowaza na kufikia katika sehemu ya kumuua Gosu Gosu mwili wote unanisisimka.Ni mtu ambaye nilitaka kumtumia kwa kazi mbali mbali za uuaji lakini ndani ya moyo wangu ninajihisi

kumpenda pia hasa kwa mambo anayonifanyia na kinachonifurahisha zaidi ni kwamba yuko tayari kufanya kitu chochote kwa ajili yangu kwa sababu ananipenda sana.Nikimuua mwanaume Yule nitaweza kweli kumpata mwingine wa aina yake? Akajiuliza Melanie

“Ngoja kwanza niliache jambo hili nijielekeze katika jambo la msingi la kumuua Rais Patrice Eyenga.Kwa namna yoyote ile lazima Patrice auawe.Niliwaahidi wazazi

wangu hivyo kwamba wale wote waliowakatili uhai wao lazima nao waondoke duniani hivyo lazima niitimize ahadi hii kwa kutumia njia yoyote ile.Sintawatendea haki wazazi wangu kama nitashindwa kuwaua watu hawa Patrice na mwenzake Dr Fabian wakati uwezo wa kufanya hivyo ninao.Ufaransa na washirika wake wamenipa uwezo mkubwa wa kuweza kulipa kisasi kwa wabaya wangu wote kwa malipo ya kuivuruga Afrika Mashariki na kuwatengenezea

njia ya kurejea kuinyonya nchi ya Congo.Kwa hivi sasa wanafurahia sana hiki kinachoendelea Afrika Mashariki laini laiti wangeifahamu mipango yangu katu wasingethubutu kunituma kuja Afrika mashariki.Ngoja niendelee kuwafurahisha huku nikiendelea kutimiza ahadi yangu ya kulipa kisasi na nitakapomaliza hawataamini macho yao kwa kile nitakachowafanyia”akaendelea kuwaza huku gari likienda katika mwendo mkali

Waliwasili katika makazi ya rais ndani ya kambi kubwa ya jeshi nje kidogo ya jiji la kampala.Melanie akashuka garini na kukaribishwa ndani

“Melanie Davis ! akasema Jenerali Akiki

“Mheshimiwa Rais” akasema Melanie na kusalimiana na Rais Akiki

“Karibu sana Melanie.Samahani kwa kukusumbua usiku huu” akasema Jenerali Akiki

“Bila samahani mheshimiwa Rais.Nimefurahi sana kuja hapa kuonana nawe”

“Ahsante Melanie” akasema Jenerali Akiki

“Vipi siku yako imekwendaje?akauliza Jenerali Akiki

“Siku yangu imekwenda vyema mheshimiwa Rais.Nashukuru ninahudumiwa vizuri ninajiona kama nipo nyumbani” akasema Melanie na Jenerali Akiki akatabasamu

“Afrika Mashariki ni ndugu moja.Ukiwa katika nchi yoyote

ndani ya jumuiya hii unajihisi uko nyumbani” akasema Jenerali Akiki

“Mheshimiwa Rais kwa hiki kinachoendelea sasa hivi ndani ya jumuiya hii hudhani kwamba inakwenda kusambaratika?akauliza Melanie.Jenerali Akiki hakujibu akachukua mkebe uliokuwa mezani akaufungua na kutoa sigara moja kubwa akawasha na kuvuta

“Melanie hutajali twende tukakae nje? akauliza

“Sawa mheshimiwa Rais” akasema Melanie kisha wakatoka na kwenda kuketi katika kibaraza wakiyatazama kwa mbali kidogo mataa ya kambi ile kubwa ya kijeshi

“Usihofu Melani sehemu hii ni salama sana” akasema Jenereali Akiki

“Sina hofu mheshimiwa Rais ninapokuwa nawe naamini ulinzi uliopo ni mkubwa” akajibuMelanie

“Uliniuliza kuhusu hofu ya kusambaratika kwa jumuiya ya

Afrika Mashariki” akasema Jenerali Akiki

“Ndiyo mheshimiwa Rais.Kuna kila dalili kwamba jumuiya ya Afrika Mashariki inakwenda kusambaratika.Uganda na Rwanda hazielewani,Uganda na Congo hazielewani,Tanzania na Uganda zina mgogoro,unadhani kwa mgogoro huu uliopo jumuiya hii itaendelea kuwa hai? Akauliza Melanie

“Ni kweli kuna hatari kubwa kuhusu kusambaratika kwa jumuiya ya Afrika

Mashariki.Yote haya ni matokeo ya mipango ya mabeberu.Wanataka kutugawanya,wanataka kuendelea kututawala na kutunyonya ndiyo maana mambo kama haya yanatokea. Melanie mabeberu hawa wanakutumia katika mipango yao,wanatumia kigezo cha kulipiza kisasi lakini kumbe wana mipango yao.Pale Rais Patrice Eyenga atakapokuwa ameuawa basi utakuwa umewatengenezea njia ya kupita kuelekea Congo ndiyo

maana ninataka James Kasai ashike madaraka ya Congo kwani Yule ndiye kiboko yao.Hakuna beberu atapeleka pua yake Congo kama James atakuwa madarakani. ” akasema Jenerali Akiki.

“Ninafahamu mheshimiwa Rais kwamba ninatumiwa na mabeberu katika kufanikisha mipango yao lakini sina namna lazima kwanza nihakikishe nimelipa kisasi kwani viongozi hawa walimuua mama yangu kikatili sana” akasema Melanie

“Usijilaumu Melanie.Usiwaze kuhusu jumuiya kuvunjika.Wewe unachotakiwa kujielekeza ni katika mpango wako wa kulipa kisasi kwa wale wote walioondoa uhai wa wazazi wako na kukuacha yatima.Hiki kinachotokea sasa ni matokeo ya uovu wao na hakuna wa kukulaumu” akasema Jenerali Akiki na kunyamaza akaendelea kuvuta sigara yake

“Melanie narudia tena kukusisitiza kwamba jumuiya ya Afrika Mashariki ivunjike au

isivunjike lakini lazima wale wote waliotoa uhai wa wazazi wako kikatili walipe uovu wao na gharama ya kile walichokifanya ndiyo hii hivyo usirudi nyuma.Songa mbele na mimi niko nyuma yako ninakuunga mkono kwa kila hatua unayochukua hadi pale utakapohakikisha kwamba wote wameuawa.Naamini pale mtu wa mwisho atakapouawa basi kila nchi itakuwa imebaki peke yake hakutakuwa tena na jumuiya.Unanisikia vizuri Melanie?akauliza Jenerali Akiki

“Ninakusikia mheshimiwa Rais”

“Vizuri.Fahamu hauko tena peke yako katika mpango huu tuko pamoja” akasema Akiki

“Nashukuru sana mheshimiwa Rais”

Zilipita dakika mbili za ukimya na Rais Akiki akasema

“Jioni ya leo nimetoka kuzungumza na Jenerali Jean Paul Mutombo mkuu wa mejeshi wa jamhuri ya kidemokrasia ya Congo” akasema Jenerali Akiki na

kunyamaza kama kawaida yake ya kuzungumza kwa vituo

“Labda kwa kukupa tu taarifa nina undugu na Jenerali Mutombo na vile vile amewahi kupata mafunzo katika jeshi la Uganda hivyo basi ni mwanafunzi wangu na nilipomuita aliitika mara moja akaja japo nchi zetu ziko katika mgogoro hivi sasa” akanyamaza tena kwa muda halafu akasema

“Kikubwa nilichomuitia ni kuhusu ule mpango wako wa kumuua Rais Patrice Eyenga.Kama nilivyowaeleza

jana kwamba hatutaweza kumuua Patrice Eyenga bila kuwashirikisha watu wa ndani ya nchi yake na watu wa karibu yake ndiyo maana nikaanzakwa kuzungumza na mkuu wa majeshi” akasema Jenerali Akiki na kunyamaza

“Kwa nini nimetaka kuzungumza kwanza na mkuu wa majeshi?akauliza Jenerali Akiki

“Kuna mpango wa mapinduzi unaandaliwa na viongozi wa juu wa jeshi la

Congo.Wanataka kuiangusha serikali ya Patrice Eyenga”

“Jeshi linataka kufanya mapinduzi?akauliza Melanie

“Ndiyo Melanie.Makamanda wa juu wa jeshi la Congo wana andaa mpango kabambe wa mapinduzi wanataka kumuondoa Rais Patrice madarakani.Machafuko yaliyokuwepo nchini Congo yaliwanufaisha sana makamanda hawa wakuu wa jeshi kwani walikuwa wakifanya bishara ya kuwauzia silaha waasi na kujipatia fedha

nyingi na madini kutoka kwao lakini kwa sasa baada ya Patrice Eyenga kumaliza uasi hawana tena chanzo cha mapato hivyo wanataka kumuondoa Patrice madarakani ili kurejesha uasi na waendelee kujipatia fedha.Ninaufahamu mpango huo na nilimuita Jenerali Paul kumtaka tushirikiane naye katika mpango huo wa kumuondoa madarakani Patrice Eyenga.Kikubwa nilichokuwa nakitaka tuelewane naye ni kumuweka James Kasai madarakani baada ya

mapinduzi hayo kufanyika lakini mambo yamekuwa magumu kidogo” akasema Jenerali Akiki na sura ya Melanie ikaonyesha hofu

“Amekataa kushirikiana nawe?akauliza Melanie

“Hapana hajakataa lakini ugumu unakuja kuhusu James Kasai.Hawako tayari kumpa James Kasai madaraka yoyote yale baada ya mapinduzi kufanyika kutokana na sifa yake mbaya.Sababu alizozitoa Paul hata mimi nimezielewa.Kwa ufupi ni kwamba James Kasai

ameharibu sana sifa yake baada ya kuanzisha mashirikiano na kikundi cha kigaidi cha IS.Kwa sasa kila mtu anamjua kama Gaidi na si mpiganaji kwa maslahi ya Congo”akanyamaza tena kidogo halafu akaendelea

“Melanie italazimu kuendelea na mpango wetu wa kumuua Patrice Eyenga bila ya kumshirikisha James Kasai” akasema Jenerali Akiki

“Unamuondoa James Kasai katika mpango huu? Melanie akauliza

“Ndiyo.Wakuu wale wa jeshi la Congo hawataki kushirikiana naye katika mpango wa mapinduzi.James Kasai ni mtu ambaye amekwisha fanya mauaji ya watu wengi nchini Congo na hata nchi jirani na kwa sasa anatafutwa na mahakama ya kimataifa ya uhalifu wa kivita kutokana na uhalifu mkubwa uliofanywa na kikundi chake cha waasi anachokiongoza.Kama utakumbuka jana nilimuahidi James kwamba nataka awe Rais

wa Congo baada ya mapinduzi lakini hilo halitawezekana tena.Itabidi tumuweke James pembeni.Hatafurahi lakini hakuna namna lazima tumuondoe katika mpango huu.Wale wakuu wa jeshi hawako tayari kushirikiana naye katika mpango wowote wa mapinduzi" akasema Jenerali Akiki

"Mheshimiwa Rais wewe mwenyewe umekuwa ukisema mara kwa mara kwamba ni James Kasai pekee ambaye anapambana kwa maslahi ya

Congo ni wakati wa kulithibitisha hilo kwa kumsaidia aweze kuingia madarakani .Umekiri wewe mwenyewe kwamba ulikubali kumsaidia James Kasai katika harakati zake kwa kuwa uliamini ndiye pekee anayefaa kuiongoza Congo.Tembea katika kauli yako hiyo" akasema Melanie

"Melanie nilichokisema kina ukweli.James hakufadhiliwa na nchi yoyote kubwa kutoka nje ya bAra ya Afrika.Mimi ndiye niliyekuwa

mfadhili wake mkuu kwa kila kitu kuanzia fedha za kujikimu askari wake hadi silaha lakini lazima niwe muwazi kwamba James Kasai ameharibu sifa yake baada ya kujiunga na kundi la kigaidi la IS.Hata raia wa Congo hawatakuwa tayari kumuunga mkono au kuongozwa na mtu mwenye sifa ya kushirikiana na magaidi” akasema Jenerali Akiki

“James hakuwafuata IS bali wao ndio waliomfuata na alikuwa katika shida kubwa ya fedha na silaha ndiyo maana

akakubali kushirikiana nao.Alihitaji kujenga jeshi lake liwe imara ili akapambane na jeshi la serikali ya Congo.Haikuwa rahisi kukataa kushirikiana na IS ambao walimuahidi fedha nyingi na silaha za kisasa.Mheshimiwa Rais kwa namna yoyote ile lazima James Kasai ashiriki katika mpango huu wa mapinduzi na kisha aingie nchini Congo kushika madaraka.Hao wakuu wa jeshi la Congo lazima watakuwa wanaandaa mpango huo kwa

kushirikiana na nchi za nje ambao ni wazalishaji wakubwa wa silaha hivyo hatutakuwa tumeisaidia Congo badala yae tutakuwa tumerejesha tena matatizo na hicho ndicho Ufaransa wamenituma kuja kukifanya na mimi sitaki kuirejesha Congo katika machafuko baadaya kumuua Patrice Eyenga" akasema Melanie

"Melanie utake usitake lazima machafuko yatatokea tu baada ya Patrice kuuawa.Majenerali wale lengo

lao kubwa ni kuanzisha machafuko ili wapate sehemu ya kuuzia silaha.Melanie kuna mambo ambayo hatuwezi kuyalazimisha.Ninaomba unielewe” Akasema Jenerali Akiki

“Mheshimiwa Rais ninakuelewa sana lakini bado naendelea kusisitiza kwamba hatuwezi kuendelea na mpango huu bila ya kumshirikisha James” akasema Melanie

“Melanie shida yako ni Patrice Eyenga auawe.Hata bila ya James Kasai Patrice atauawa”

“Mheshimiwa Rais kwa namna yoyote ile lazima James ashirikishwe” akasisitiza Melanie

“Kwa nini unasistiza sana ushiriki wa James Kasai?akauliza Jenerali Akiki

“Kwa sababu ninamuamini anaweza akafanya vile ninavyotaka.Siwezi kuwaamini jenerali hao wa jeshi ambao yawezekana mpango wao ukashindwa kufanikiwa au wanaweza wakafanya mapinduzi bila kumuua Rais Patrice lakini James Kasai kama

atashiriki atahakikisha Patrice anauawa”

“Melanie usihofu bado majadiliano na mkuu wa majeshi wa Congo yataendelea hivyo suala hilo la kuhakikisha Patrice Eyenga anauawa litazingatiwa”akasema Jenerali Akiki

“Mheshimiwa Rais sifahamu mazungumzo hayo yatachukua muda gani na mimi sina muda mrefu wa kusubiri.Nahitaji jambo hili lifanyike haraka kwani nina mambo mengi ya kukamilisha

hivyo nashauri tuendelee na mpango wetu wa kumuua Patrice Eyenga bila kushirikiana na jeshi la nchi hiyo” akasema Melanie na Jenerali Akiki akawasha sigara nyingine.

“Melanie una mpango wowote kichwani mwako ambao unadhani tunaweza kuutekeleza bila kulihusisha jeshi la Congo?akauliza Jenerali Akiki.

“Ndiyo ninao mpango mheshimiwa Rais” akasema Melanie

“Nieleze tafadhali”

“Hivi sasa nchi yako na Congo hazina maelewano mazuri.Nataka kuitumia fursa hiyo.Utampigia simu Rais wa Tanzania na kumueleza kwamba unataka kukutana na kufanya mazungumzo naye pamoja na Rais wa Congo mazungumzo yanayolenga kutafuta amani katika nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki na mazungumzo hayo yafanyike nchini Tanzania.Naamini Rais wa Tanzania atakubali jambo hilo na atamualika Rais Patrice kuhudhuria mazungumzo

hayo.Kikubwa utakachowaeleza utakaputna nao ni kwamba uko tayari kutoa taarifa za mahala alipo James Kasai.Wakati mazungumzo hayo yakifanyika litapandikizwa bomu ndani ya ndege ya Rais Patrice na atakapoondoka akiwa angani bomu hilo litalipuliwa na utakuwa ndio mwisho wa Patrice Eyenga” akasema Melanie na Jenerali Akiki akamkazia macho huku akipuliza moshi mwingi.

“Mpango huo”Melanie akaendelea

“Hautawahusisha watu kutoka ndani ya serikali ya Congo lakini naamini majenerali hao wa jeshi ambao wanaandaa mpango wa mapinduzi pindi watakaposikia kwamba Patrice Eyenga ameuawa basi watatangaza jeshi kushika nchi na hiyo ni fursa nyingine kwa James Kasai kuanzisha mapambano na jeshi la serikali na huku wewe ukimuunga mkono na hiyo ndiyo fursa yako kama unataka James Kasai aiongoze Congo” akasema Melanie.Baada ya

kutafakari kwa muda Jenerali Akiki akasema

“Melanie mpango huo si mbaya.Ni mpango mzuri lakini ni wa hatari kubwa sana na utekelezaji wake unaweza kuwa mgumu mno” akasema Jenerali Akiki

“Mheshimiwa Rais mpango huu japo unasema ni mgumu lakini ndio hasa mpango ambao mimi nauona ni rahisi na utakaotusaidia kumuua Patrice Eyenga kwa haraka”

“Ugumu ninaouzungumza mimi ni namna ya kuliingiza

hilo bomu ndani ya ndege.Kuhusu kuwaita marais hilo halina ugmu ninaweza nikajishusha na nikaomba kukutana nao lakini je hilo bomu litaingizwa vipi ndani ya ndege? Ni vipi kama likagundulika mapema na mpango ukashindwa kufanikiwa?Sote tutakuwa katika hatari kubwa”akasema Jenerali Akiki

“Usihofu mheshimiwa Rais.Ninao mtandao mkubwa na nina uhakika suala la kuingiza bomu katika ndege ya Rais

halitakuwa tatizo.Ninachohitaji ni wewe kukubali kujishusha na kuitisha kikao na marais hao wa Tanzania na jamhuri ya kidemokrasia ya Congo”akasema Melanie

“Hata kama mpango huo utafanikiwa na Patrice Eyenga akauawa lazima lawama zote zitaiangukia serikali ya Uganda.Lazima dunia nzima itaamini sisi ndio tuliomuua na huo utakuwa ni mgogoro mwingine unaoweza kusababisha hata vita kati ya Congo na Uganda ndiyo maana

nilitaka kuwatumia watu wa ndani ya Congo ili hata kama ni vita basi iwe ni baina yao wenyewe sisi tusihusishwe na lolote” akasema Jenerali Akiki

“Pamoja na faida zake lakini mpango huo utachukua muda mrefu.Majadiliano hatujui yatachukua muda gani hadi kufikia makubaliano na mimi nataka jambo hili liende haraka haraka kwani bado nina mambo mengi ya kufanya.Naomba mheshimiwa Rais kama kweli una nia ya dhati ya kunisaidia kubaliana na mpango wangu

huu nilioupendekeza” akasema Melanie na ukimya ukatawala mahala pale.Baada ya dakika kadhaa za tafakari Jenerali Akiki akasema

“Melanie endapo nitakubali kufanya haya yote unayoyataka niyafanye nini yatakuwa malipo yangu? Nataka kujua namna nitakavyofaidika kupitia mpango huo. Wewe utakuwa umelipiza kisasi na utajihisi amani na mimi pia nahitaji kufaidika” akasema Jenerali Akiki

“Endapo tukiamua kuukubali mpango wa mapinduzi kwa kushirikiana na jeshi wewe utafaidika na nini?akauliza Melanie

“Zipo faida ambazo ningezipata kupitia mpango ule tena kubwa tu” akasema Jenerali Akiki

“Wewe unahitaji nini mheshimiwa Rais?Fedha? Kiasi gani?akauliza Melanie na Jenerali Akiki akatabasamu

“Sihitaji fedha.Ninazo fedha za kutosha.Nahitaji kitu kingine”

“Kitu gani? Melanie akauliza

“Wewe” akajibu Jenerali Akiki akiwa na macho makavu.Melanie akatoa kicheko kidogo na kusema

“Unanihitaji mimi?! Akauliza Melanie

“Ndiyo”

“Unanihitaji kivipi mheshimiwa Rais?Melanie akauliza

“Melanie wewe si mtoto mdogo wa kushindwa kutambua ninamaanisha nini”akasema Jenerali

Akiki.Ukapita ukjimya mfupi Melanie akauliza

“Mheshimiwa Rais tafadhali niambie kama humaanishi hicho unachokisema” akasema Melanie

“Ninaamisha Melanie.Nakuhitaji wewe.Nakuhitaji uwe mpenzi wangu wa siri” akasema Jenerali Akiki na Melanie akacheka kidogo

“Mheshimiwa Rais jana ulisema kwamba ulikuwa na ukaribu mkubwa sana na wazazi wangu hasa mama

ambaye alisoma na mke wako na ukatamka kwa ulimi wako kwamba kutokana na ukaribu huo mimi ni kama mwanao kwa nini leo unataka kulala na mwanao?

“Sikiliza Melanie wewe tayari ni mtu mzima na mambo ya kupenda unayaelewa vyema.Ni kweli nilikuwa na ukaribu na wazazi wako lakini nimeshindwa kuudhibiti moyo wangu kufukuta toka nilipokuta machoni.Melanie hakuna kitu chochote kibaya kitatokea kama mimi nawe tutakuwa wapenzi

wa siri.Nikubalie nikitakacho na ninakuahidi utapata kila unachokitaka” akasema Jenerali Akiki

“Nimekutana na kigingi kingine tena.Wanaume hawa wakoje? Wameumbwaje?Mbona wote wako sawa? Akawaza Melanie

“Melanie unasemaje kuhusu hilo nililokuomba?akauliza Jenerali Akiki huku akiwasha sigara nyingine tena

“Kwa nini unanifanyia hivi mheshimiwa Rais?akauliza Melanie

“Kuna ubaya gani mimi na wewe tukiwa wapenzi wa siri Melanie?Au ukinipa hicho ninachohitaji utapungukiwa nini?Ninachokiomba kutoka kwako ni kidogo sana ukilinganisha na kile ambacho nitakifanya kwa ajili yako.Ninakwenda kuubeba mzigo mzito sana kwa ajili yako.Wewe hautajulikana bali ni mimi ambaye ninaweza kutilia shaka kuhusika na mauaji hayo hivyo sidhani kama kuna haja ya kuwa na majadiliano makubwa zaidi

katika suala hili” akasema Jenerali Akiki

“Huyu anaweza akanikwamisha mipango yangu kwa kuwa anajua ninamuhitaji sana.Ni kweli namuhitaji sana katika suala hili lakini mzee mzima naye amekwisha waka tamaa na sasa anataka nimpe mwili wangu.Sina namna ngoja nimpe anachokitaka ili mambo yangu yaende lakini ajue kila mwosha huoshwa.Iko siku yake” akawaza Melanie

“Mheshimiwa Rais sina namna.Ninakuhitaji sana katika

mpango huu.Niambie lini unanihitaji na wapi mimi nitakuja” akasema Melanie na Jenerali Akiki akatoa tabasamu

“Tunaanza usiku wa leo”

“Leo?

“Ndiyo.Hakuna anayejua kesho yake hivyo ninakuhitaji kuanzia usiku wa leo”

“Mpaka lini?Lazima kuwe na ukomo hatuwezi kuendelea na mchezo huu.Wewe ni rais wa nchi una mke ambaye ni rafiki wa mama yangu ambaye akijua kama unatembea na mimi ambaye ni sawa na mwanao

utaingia katika mgogoro mkubwa wa familia yako” akasema Melanie

“Ni kweli mimi ni Rais wa nchi lakini vile vile ni binadamu na nina mahitaji kama wanadamu wengine hivyo mambo yangu mimi na wewe hayahusiani chochote na urais wangu”

“Nimekuelewa mheshimiwa Rais lakini usiku wa leo niache niende na kesho nitakuwa mgeni wako.Ninataka nije nikiwa nimejiandaa vyema kimwili na kiakili kwa siku ya

leo sikuwa nimejiandaa kwa suala hilo” akasema Melanie

“Hakuna tatizo Melanie.Nashukuru kwa kunielewa.Nadhani kesho tutapata wasaa mzuri zaidi wa kujadili kwa kina hili suala letu namna tutakavyoweza kulikamilisha.Ninachokuomba James Kasai asifahamu chochote kuhusiana na haya tuliyoyazungumza leo hadi pale wakati muafaka utakapofika” akasema Jenerali Akiki.Hakukuwa na mazungumzo mengine tena

akamsindikiza Melanie hadi katika gari akaondoka.Jenerali akiki akarejea ndani

“Melanie Davis ! akawaza huku akiwasha sigara akavuta mikupuo kadhaa huku akiachia tabasamu pana sana

“Ningechekwa na dunia kama mtoto Yule angeondoka Uganda bila kumgusa hata kidogo.Ni kweli mama yake alikuwa ni rafiki wa familia yetu lakini nimeshindwa kuvumilia.Japo uzuri wake ni wa kutegenezwa lakini

umenichanganya sana” akawaza Jenerali Akiki.

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Ndege ya shirika la ndege la Misri ilitua katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es salaam saa nne za usiku ikitokea jijini Cairo kupitia Nairobi Kenya.Abiria walishuka ndegeni na kuingia katika jengo la uwanja ili kukamilisha taratibu za kuingia nchini.Mathew Mulumbi akiwa miongoni mwa abiria waliokuja na ndege hii alikuwa na hati ya

kusafiria inayomuonyesha kuwa ni raia wa Saudi Arabia mwenye jina la Abu Al Zalawi.

“Ninarejea nyumbani kama mgeni wakati hii ni nchi yangu ya kuzaliwa lakini imenilazimu nirejee namna hii.Hapa uwanjani wapo watu wengi wanaonifahamu ila naamini kwa mwonekano huu nilio nao sasa hakuna atakayenigundua.Nilifanya jambo zuri kufuga hizi ndevu nyingi.Kwa muonekano huu kila mtu atadhani labda mimi ni kiongozi wa kidini huko

nilikotoka” akawaza Mathew akiingia ndani ya jengo la uwanja.Hakuwa akizungumza Kiswahili alizungumza kiingereza akichanganya na kiarabu kidogo.Aliwaona baadhi ya watu kadhaa pale uwanjani aliokuwa akifahamiana nao akajitahidi kuwakwepa asionane nao.

Baada ya kukamilisha taratibu na kuruhusiwa kuingia nchini Mathew akaenda katika duka la kubadili fedha za kigeni akabadili fedha alizokuwa nazo na kupata fedha za Tanzania na

kutoka nje.Alitamani asujudu na kuibusu ardhi ya Tanzania kwa furaha aliyokuwa nayo.

“Natamani niibusu ardhi ya nchi yangu kwani sikuwa nimetegemea kuikanyaga tena katika maisha yangu lakini leo kwa nguvu ya Mungu nimerejea nchini” akawaza akiendelea kukokota torori lenye mabegi yake hadi alipotoka nje.Hakukuwa na mtu yeyote aliyekuja kumpokea hivyo akachukua taksi.

“Nikupeleke wapi kaka?akauliza dereva taksi kwa lugha ya kiingereza

“Ninaomba unipeleke katika hoteli yoyote nzuri yenye utulivu mkubwa lakini kabla hujanipeleka huko nahitaji kupita katika supermarket yoyote kubwa kuna vitu nahitaji” akasema Mathew na dereva akaondoa gari

“Baada ya miaka mitatu hatimaye niko tena ndani ya jiji la Dar.Jiji limebadilika sana.Maendeleo makubwa yamefanyika katika kipindi

hiki” akawaza Mathew akiwa amekaa kiti cha nyuma akielekeza macho nje

Hatimaye baada ya kuzunguka katika supermarket kadhaa kubwa na kukuta zimefungwa ,wakaipata ambayo ilikuwa wazi.Mathew akashuka garini na kuingia ndani ya duka lile akaelekea katika upande wa vifaa vya elektroniki akachukua mashine ya kunyolea nywele pamoja na vitu vingine kadhaa akaenda kuilipia na kurejea garini safari ikaendelea.Dereva Yule alimfikisha katika hoteli

moja nzuri wakaagana huku Yule dereva akimpa kadi yake ya biashara.Mathew akapokewa na wahudumu wachangamfu na kupewa chumba

“Ni kama ndoto lakini ni kweli niko Dar es salaam.Kwa anayenifahamu atashangaa sana kuniona hapa hotelini kwani ninafahamika sana hapa Dar es salaam kama mmoja wa watu matajiri.Nimewekeza katika majumba mengi tu lakini kwa mujibu wa Habiba Jawad Peniela ameuza mali zangu zote zilizoko Dar es salaam hivyo

siwezi kujua katika mauzo hayo nyumba ipi imeuzwa na ipi imesalimika.Zipo baadhi ya nyumba ambazo Peniela hazifahamu anayezijua ni Gosu Gosu.Mtu wa kwanza kabisa ambaye natakiwa kumtafuta kesho ni Gosu Gosu,nikimpata huyu nitafahamu mengi kutoka kwake" akawaza Mathew na kuingia bafuni akaanza kunyoa ndevu zote alizofuga akajitazama na kutabasamu

"Hii ndiyo sura halisi ya Mathew Mulumbi.Nilipotoka kwa Ammar Nazari nilikuwa

nimechakaa sana lakini baada ya kuanza kuishi na Najma kidogo najiona nimeanza kunawiri” akawaza huku akipaka dawa katika kidevu chake halafu akajitazama tena katika kioo

“Welcome back Mathew Mulumbi” akasema kwa sauti ndogo akaoga kisha akaenda kujilaza kitandani.

“Natakiwa kumjulisha Habiba kwamba tayari nimefika salama Dar es salaam” akawaza Mathew.Hakuwa na simu akachukua kompyuta yake

akaiunganisha na intaneti.Hoteli ile ilikuwa na huduma ya mtandao wa intaneti.Baada ya kuunganisha akamtafuta Habiba Jawad na kumpigia simu kwa kutumia mtandao wa skype.

“Mathew Mulumbi” akasema Habiba baada ya kupokea simu ya Mathew

“Mama Habiba” akasema Mathew huku akitabasamu

“Naona uso wako una furaha kubwa leo.Umenyoa ndevu umebadilika sana.Umerudi kuwa Mathew

Mulumbi na si Abu Zalawi” akasema Habiba huku akitoa kicheko kidogo

“Ni kweli mama nina furaha ya kufika nyumbani.Nimekupigia kukujulisha kwamba tayari nimefika Tanzania na hapa nilipo nipo hotelini”

“Pole kwa safari Mathew.Nashukuru umefika salama.Kwa sasa endelea kupumzika hadi kesho tutazungumza zaidi.Jitahidi upate simu kwa ajili ya mawasiliano utakapokuwa

hapo kwani hatuwezi kuwasiliana kila mara kwa kupitia mtandao”

“Ni kweli mama.Kesho nitashughulikia kila kitu na jioni nitakupigia tuzungumze” akasema Mathew na kuagana na Habiba kisha akachukua juisi aliyonunua supermarket akanywa .

“Sasa nijipumzishe nijiandae kwa siku ya kesho.Nitakuwa na mizunguko mingi” akawaza na kujilaza kitandani

****

Sauti za watu waliopita wakizungumza nje ya mlango wa chumba alicholala ndizo zilimstua Mathew kutoka usingizini akafungua macho na chumba kilikuwa na mwanga wa kutosha.Akayaelekeza macho ukutani kulikokuwa na saa kubwa ambayo ilionyesha ni saa mbili na dakika kumi na nane

“Usingizi wa nyumbani mtamu sana ndiyo maana nimelala hadi nikapitiliza

namna hii.Kawaida yangu huamka saa kumi na mbili za asubuhi” akawaza Mathew kisha akatoka pale kitandani akavaa nguo za mazoezi na kuelekea katika chumba cha mazoezi.Hoteli ile aliyofikia ilikuwa na chumba maalum cha mazoezi.Alifanya mazoezi kuuweka mwili sawa halafu akaenda kuoga kujiandaa kwa ajli ya kuikabili siku.Siku hii alivaa suruali ya jeans rangi nyeusi na fulana ya rangi nyeupe kichwani akavaa kofia ya rangi nyeusi ,macho

akayafunka kwa miwani myeusi bila kusahau mkufu wa dahabu kifuani akajitazama katika kioo akaridhika kwa mwonekano ule kisha akaelekea sehemu ya chakula akaagiza kifungua kinywa.Wakati akiendelea kupata kifungua kinywa akapita kijana muuza magazeti Mathew akanunua magazeti matatu akapitia kwa juu juu lakini kubwa ambalo lilitawala magazeti yale ni matukio ya kushambuliana yanayoendelea baina ya Uganda na Rwanda.Alipomaliza kifungua

kinywa akaenda kulipa na kumuachia chenji muhudumu kisha akatoka nje akaanza kutembea kwa miguu

“Sijui kwa nini nikiwa sina silaha ninajiona mzito sana lakini hata kama itatokea hatari yoyote ninao uwezo wa kukabiliana nayo bila kuwa na silaha” akawaza huku akivuka barabara kuelekea upande wa pili ambako aliona taksi nyingi zimeegeswa.Akakodisha taksi moja akamtaka dereva ampeleke sehemu Fulani

“Sehemu ya kwanza ninakoanzia leo ni nyumbani kwangu.Nataka nikamfahamu aliyenunua ni nani na nijue vitu vilivyokuwamo mle ndani vimepelekwa wapi.Kulikuwa na vitu vyangu vingi na vingine vya siri kabisa.Nilijenga nyumba ile kwa ajili yangu na ndiyo maana nikaweka baadhi ya vitu kama sehemu za siri za kuhifadhia silaha n.k.Peniela alikosea sana kuiuza nyumba yangu ile lakini siwezi kumlaumu kwa sababu anajua tayari nimefariki dunia na yeye hana mpango wa kuja

tena kuishi Tanzania ndiyo maana akaamua kuiuza.lakini kwa nini Peniela akaamini haraka namna hii kwamba nimefariki dunia?Kitu gani klichomuaminisha haraka hivyo?Kwa nini hakutaka kufanya uchunguzi kujua kama kweli nimekufa? Anyway nisiumize kichwa kwa hilo majibu yote anayo yeye mwenyewe” akawaza Mathew huku gari likiendelea kukata mitaa kuelekea katika nyumba ya Mathew

“Natamani sana kumtafuta Ruby na kujua maendeleo yake.Najua nilimuacha katika wakati mgumu sana,nakumbuka ni siku moja tu ilipita toka anieleze kwamba ananipenda na anataka tuwe wapenzi na nilimuahidi kwamba baada ya kumaliza operesheni ile basi tungekwenda mahala sisi wawili pekee kupumzika.Tayari nilikwisha amua kuwa na mahusiano ya siri na Ruby lakini kwa bahati mbaya sikurejea tena

Tanzania.Atakuwa aliumia mno.Yuko wapi sasa hi0vi?Anafanya nini?Ameolewa au bado?Yote haya natakiwa kujua.Nitamuuliza Gosu Gosu nikionana naye" akaendelea kuwaza Mathew

Hatimaye dereva wa ile taksi aliyopanda alifika katika mtaa ilipo nyumba ya Mathew.

"Huu mtaa wangu nimeukumbuka sana.Umejengeka mno sasa hivi.Mimi ndiye muasisi wa mtaa huu.Nilianza kujenga wakati hakuna nyumba hata

moja” akawaza huku akitabsamu na gari likienda kwa mwendo wa taratibu.Dereva akakata kushoto kufuata barabara ya zege iliyoelekea nyumbani kwa Mathew.Mapigo ya moyo wake yakaanza kumwenda kasi walipokaribia geti la nyumba yake.Kulikuwa na walinzi wawili wakawasimamisha.Mathew akafungua mlango akashuka akamlipa dereva akaondoka halafu akawafuata walinzi.Hakuwa akiwafahamu

walinzi wale akasalimiana nao vizuri kisha wakamuuliza shida yake

“Nahitaji kuonana na wahusika wa nyumba hii” akasema Mathew

Walinzi wale wakataka kufahamu yeye ni nani na katokea wapi akawajibu kwamba ametokea nje ya nchi na ni ndugu ya wanaoishi pale.Mmoja wa walinzi akaingia ndani na kupiga simu ndani ya nyumba akieleza kwamba kuna mgeni wao ametokea nje ya nchi.

“Subiri kidogo kuna mtu anakuja” akasema Yule mlinzi aliyeingia ndani kupiga simu.Baada ya dakika tatu mlango mdogo wa geti ukafunguliwa na msichana mmoja akajitokeza

“Lucy !! akasema Mathew huku akivua miwani na kofia mara kikatokea kitu kilichowashangaza wote.Lucy aligeuka haraka akatimua mbio kurudi ndani huku akipiga kelele wale walinzi wakaanza kumkimbiza.Mathew akavuka geti akaingia ndani.Lucy

hakufika mbali akaanguka chini na kupoteza fahamu.Walinzi wale wakaungana na Mathew wakaanza kumpatia huduma ya kwanza

“Ana matatizo gani huyu? Mathew akauliza

“Tukuulize wewe kwani alipokuona tu ndipo alipoanza kupiga makelele na kukimbia.Wewe ni nani?akauliza mlinzi mmoja

“Tusubiri azinduke tutajua tatizo lake” akasema Mathew huku walinzi wale wakionekana kuwa na woga.

Baada ya muda Lucy akaamka na mara tu alipomuona Mathew yuko pale sebuleniakaanza tena kupiga kelele na kutaka kukimbia lakini walinzi wakamzuia,Mathew akamuendea

“Jamani msimruhusu anisogelee ni mzimu huyo ! akapiga kelele Lucy na wale walinzi wakabaki wanashangaa

“Lucy ! akaita Mathew lakini Lucy akapiga kelele kubwa.Mlinzi mmoja akataka kumzuia Mathew asimsogelee

Lucy lakini Mathew akamsukuma akasogea pembeni

“Lucy !! akaita Mathew na kumshika Lucy mabegani.Alikuwa anatetemeka

“Mimi si mzimu.Nitazame vizuri ni mimi Mathew.Ni mimi Yule Yule unayenifahamu” akasema Mathew

“Mathew amekwisha fariki miaka mitatu iliyopita ! akasema Lucy huku akitetemeka

“Hapana Lucy sikufariki.Mimi ni mzima ila

nilikuwa katika matatizo makubwa na taarifa mliyoipata kwamba nimefariki si taarifa ya kweli.Mimi ni mzima kabisa.Mimi si mzimu" akasema Mathew lakini bado Lucy aliendelea kutetemeka

"Lucy usiwe na wasiwasi ni mimi Mathew nimerejea" akasema Mathew na mara mmoja wa walinzi akamsogelea Lucy

"Lucy unahitaji msaada wa polisi? Akauliza mmoja wa walinzi

“Msijali ndugu zangu.Mimi ni mwajiri wake wa zamani na ndiye mmiliki wa nyumba hii.Nilipotea kwa miaka mitatu na taarifa waliyopata ni kwamba nimekufa kumbe niko hai”Mathew akajaribu kujieleza

“Ni kwel Lucy hayo anayoyasema huyu jamaa?akauliza mlinzi na Lucy akatingisha kichwa kukubali

“Una hakika hatakuwa na madhara tukikuacha naye humu ndani?akauliza mlinzi

“Ndugu zangu msiwe na wasiwasi na mimi hata

kidogo.Hii ni nyumba yangu na huyu ni mfanyakazi wangu.Hamnifahamu lakini mimi ndiye mwenye nyumba hii” akasema Mathew

“Nendeni msiwe na wasi wasi hakuna tatizo” akasema Lucy na walinzi wale wakatoka lakini bado wakiwa na wasiwasi.

“Lucy tafadhali nyamaza kulia ni mimi Mathew nimerudi” akasema Mathew baada ya Lucy kuanza tena kulia baada ya walinzi kutoka.

“Tafadhali usilie Lucy” akasema Mathew na kutoa kitambaa akamfuta machozi na mara Lucy akamkumbatia kwa nguvu.

“Mathew jamani kaka yangu !! akasema Lucy huku akiendelea kumwaga machozi

“Imetosha Lucy usiendelee kulia” akasema Mathew

“Mathew niache nikulilie kaka yangu hujui ni machungu gani nimeyapata kwa kuamini kwamba umefariki dunia.Nimekulilia usiku na mchana.Nimekuombea sana

upumzike kwa amani nikiamni umekufa ndiyo maana nilipokuona nilipatwa na mstuko mkubwa sana.Niache nikulilie kaka Mathew” akasema Lucy.

“Nyamaza Lucy.Nimerudi niko mzima wa afya.Hakuna sababu ya kuendelea kumwaga machozi.Ahsante kwa maombi yako ambayo naamini yamenisaidia sana hadi tumekutana tena hapa”akasema Mathew

“Nini kilikutokea Mathew?Ulikuwa wapi?Nani

waliosambaza taarifa kwamba umekufa? Lucy akauliza huku akifuta machozi

“Tutazungumza hayo yote baadae nitawaeleza nilikuwa wapi lakini kwa sasa nataka kufahamu nani wanaishi hapa?

“Tunaoishi hapa ni mimi na Gosu Gosu”

“Gosu Gosu?

“Ndiyo”

“Hakuna watu waliouziwa nyumba hii?

“Hakuna kaka.Nilisikia kuna mali zako zimeuzwa lakini nyumba hii

haikuuzwa.Tunaendelea kuuishi mimi na Gosu Gosu”

“Ahsante Mungu” akasema Mathew na kushusha pumzi

“Gosu Gosu yuko wapi?akauliza Mathew na Lucy akaanza tena kulia

“Imetosha Lucy usilie tena” akasema Mathew

“Nieleze tafadhali mahala alipo Gosu Gosu”

“Gosu Gosu…” akasema Lucy na kushindwa kuendelea akaendelea kulia

“Yuko wapi Gosu Gosu? Mathew akauliza

“Yuko hospitali amepigwa risasi juzi”

“Amepigwa risasi?

“Ndiyo?

“Nani kampiga risasi?

“Bado haifahamiki nani waliompiga risasi” akasema

Lucy na Mathew akavuta pumzi ndefu na kuuliza

“Vipi hali yake?

“Hali yake ni mbaya anapumua kwa msaada wa mashine”

“Oh my God ! akasema Mathew

“Yuko hospitali gani?akauliza

“Hospitali ya Mtodora” akajibu Lucy na Mathew akasimama

“Lucy vile vitu vilivyokuwa chumbani kwangu vimewekwa wapi?akauliza Mathew

“Hakuna kitu hata kimoja kilichotolewa chumbani kwako.Chuba chako kilifungwa .Ni mimi tu ambaye huingia na kufanya usafi”

“Ahsante sana Lucy naomba ufunguo wa chumbani kwangu” akasema Mathew na Lucy

akaenda chumbani kwake akachukua funguo na kumpatia Mathew wakaelekea katika chumba cha Mathew.Akaufungua mlango wakaingia ndani

“Kila kitu ni kama nilivyokiacha” akasema Mathew

“Nimekuwa nikiingia mara kwa mara kufanya usafi”

“Lucy nakushukuru sana.Naomba unipe dakika chache nisubiri hapo nje” akasema Mathew na Lucy akatoka.Mathew akaenda kukaa kitandani

“Chumba hiki sikutegemea kukiona tena.Ahsante Mungu kwa kunifikisha leo katika chuba changu.Nawashukuru pia hawa waliokitunza chumba hiki kwa umakini mkubwa.Kila kitu kiko vile vile nilivyokiacha” akawaza Mathew na kufungua chumba chake cha siri ambacho hukitumia kuhifadhi silaha mbali mbali

“Silaha zangu zote ziko vile vile”akawaza na kuchukua bastora moja akaijaribu ikiwa haina risasi na kutabasamu

kisha akaweka risasi na kuifutika kiunoni

“Nani kamshambulia Gosu Gosu na kwa nini? Akajiuliza Mathew

“Tayari nimepata pigo la kwanza.Gosu Gosu nilimtegemea sana katika misheni hii hivyo sintaweza kuwa naye.Kama anapumua kwa msaada wa mashine basi hali yake ni mbaya sana.Ninamuombea aweze kupona.Sitaki kumpoteza Yule mwanajeshi.Hata kama nitamkosa katika misheni hii

lakini nitamuhitaji huko mbeleni.Kwa sasa ngoja nielekee hospitali alikolazwa nikajue maendeleo yake” akasema Mathew na kutoka akamuomba Lucy funguo za gari.Kulikuwa na gari limeegeshwa mbele ya nyumba aina ya Mercedece benzi alilokuwa analitumia GosuGosu.Mathew akamuaga Lucy kuwa anakwenda hospitali kumtazama Gosu Gosu.

“Nimefurahi kwa Peniela kutokuiuza nyumba yangu.Nimefurahi pia kwa

namna Gosu Gosu alivyoitunza hadi leo hii.Chumba changu hakijawahi kuguswa kila kitu kiko vile vile.Je Gosu Gosu aliamini siku mojaninaweza kurejea ndiyo maana akakifunga chumba changu na hakutaka kukitumia? akawaza Mathew na kuingia katika kituo cha mafuta akajaza mafuta ya kutosha katika gari na kuelekea hospitali

Geti la kuingilia hospotali ya mtodora lilikuwa wazi Mathew akapita na kwenda hadi maegesho akafungua

mlango na kushuka akatazama pande zote kuhakiki usalama halafu akaanza kupiga hatua kuelekea katika jengo la mapokezi ambako aliwakuta wahudumu kadhaa akawauliza mahala alipo mgonjwa wake Gosu Gosu,akaelekezwa kwamba yuko katika jengo la wagonjwa mahututi bila kupoteza muda Mathew akaelekea huko.Alipolikaribia jengo hilo akasimama ghafla baada ya kumuona mtu Fulani kwa mbali

“Austin ?! akajiuliza Mathew kwa sauti ndogo

“Ni yeye kweli au nimemfananisha? Akajiuliza akiendelea kumtazama

“Macho yangu bado yana nguvu ya kutosha.Sina shaka na kile ninachokiona.Yule atakuwa ni Austin.He’s alive” akawaza Mathew na kuanza kupiga hatua kumsogelea.Mtu Yule alikuwa ameinamisha kichwa akitazama chini alionekana kuwa na mawazo mengi sana

“Hallo brother” akasema Mathew na kumstua Yule mtu

ambaye aliinua kichwa wakatazamana.Mathew akavua kofia na miwani.

“Mungu wangu !! akasema Austin kwa mstuko mkubwa.Alikuwa ameshika karatasi kadhaa zikamponyoka.Walitazamana kwa muda wa sekunde kadhaa

“Hallo Austin ! akasema Mathew

“Ma..mamamamath…” Austin alitetemeka mdomo akashindwa kutamka.Akatazama kulia na

kushoto kama vile anataka kukimbia

“Usiogope Austin ni mimi Mathew Mulumbi” akasema Mathew na kumpa mkono

“How’re you?akauliza Mathew.Bado Austin aliendelea kumtazama kwa hofu

“Austin usiwe na hofu.Ni mimi Mathew.I’m not a ghost.Nishike mkono tafadhali” akasema Mathew akiwa ameunyoosha mkono wake.Taratibu Austin akauinua mkono wake wa kulia na kuushika mkono wa Mathew

akauminya kidogo na kumtazama usoni

“This is unbelievable !! akasema kwa sauti ndogo halafu akamkumbatia Mathew kwa nguvu.

“Ouh Mathew my brother !! akasema Austin na Mathew akahisi bega lake lilikuwa linaloa machozi

“It’s okay Austin.Imetosha.Hatuna sababu ya kumwaga machozi.We cry for the dead but I’m not dead.I’m still alive” akasema Mathew lakini Austin akajikuta

amechuchumaa chini akimwaga machozi.Watu waliokuwepo eneo lile wakawatazama wakihisi labda Austin amepata taarifa mbaya kuhusu mgonjwa wake

“Austin usilie.Inuka tafadhali” akasema Mathew na kumnyanyua .

“Mathew Mulumbi ! akasema Austin na kumkumbatia tena Mathew.

“Huu kwangu ni muujiza mkubwa sana ambao sikuwa nimeutarajia kabisa.Mathew !!

Bado Austin alikuwa katika mshangao .

“Austin tutazungumza mengi lakini kikubwa kilichonileta hapa ni Gosu Gosu.Nataka kujua maendeleo yake”

“Hali yake si nzuri.Naamini hadi umefika hapa tayari umekwisha pewa taarifa kwamba hata kupumua ni kwa msaada wa mashine.Mathew tunaweza kumpoteza Gosu Gosu.Anything can happen! akasema Austin akionekana kukata tamaa.

“Dah ! hili ni pigo kubwa sana.Nahitaji kumuona. I need to talk to him” akasema Mathew na Austin akazungumza na wauguzi,Mathew akavishwa mavazi maalum na kuingia ndani ya chumba alimolazwa Gosu Gosu.Akamtazama

“Please God don’t take him yet.We still need him” Mathew akaomba kimya kimya kisha akavuta kiti akaketi karibu na Gosu Gosu

“Papi Gosu Gosu it’s me Mathew Mulumbi.I’m not dead

and I’m back home” akasema na kuvuta pumzi ndefu

“Kwa mara ya kwanza nilipokuja kukuchukua kutoka kwa Kasu niliamini mimi nawe tunaweza kuwa watu wa karibu sana na ndivyo ilivyokuwa.Sifahamu kwa nini nilikuamini sana na baada ya operesheni ile kumalizika nikakuweka msimamizi wangu wa miradi kazi ambayo uliifanya kwa umakini na uaminifu mkubwa sana.Umekuwa si rafiki bali ndugu yangu.Nikiwa njiani

nikirejea nyumbani wewe ndiye mtu wa kwanza ambaye nilitaka kukutana naye lakini kwa bahati mbaya nimekukuta ukiwa katika hali hii.Gosu Gosu wewe ni mwanajeshi usiyeogopa chochote.I know you're going to fight this.Please fight my brother.I need you so badly so don't leave me yet.I know you're listening to me right now so fight for your life.I have a bigger mission and I need you.Utakapoamka nitakueleza nilikuwa wapi na

kwa nini ninakuhtaji sana” akasema Mathew na kusimama

“Please fight Gosu Gosu and wake up very soon ! akasema Mathew na kutoka

“Umeona mwenyewe hali yake ilivyo” akasema Austin

“Hali yake inakatisha tamaa sana lakini Gosu Gosu ni mpiganaji nimemwambia apambane aamke naamini amenisikia” akasema Mathew

“Hata mimi nimekuwa nikiamini hivyo kwamba ataamka muda si mrefu kutokana na ujasiri wake lakini

naona siku zinakwenda hakuna maendeleo yoyote ya kutia moyo.Usiku unapita unakuja mchana unaingia tena usiku lakini bado Gosu Gosu hana dalili zozote za kuamka.Mathew mimi ni jasiri sana lakini katika hili nimeanza kukata tamaa.Tunakwenda kumpoteza Gosu Gosu" akasema Austin

"Austin usiruhusu hata siku moja roho ya kukata tamaa ikakuingia.Unatakiwa uwe na imani hata pale ambapo hakuna matumaini.Kuwa na moyo mgumu kama wa jiwe usikubali

kushindwa.Kwa hili la Gosu Gosu bado hatuna sababu ya kukata tamaa.Tuendelee kusimama imara karibu yake na atazinduka.Akiwa katika hali ile anaweza akakaa hata mwaka na hatupaswi kukata tamaa.Ni wajibu wetu kumkumbusha kila mara kwamba tuko karibu yake na tunamuhitaji azinduke.Atatusikia na atazinduka.Gosu Gosu is our brother,we love him and we don’t give up on people we love.You understand me Austin ? akasema Mathew

“I understand Mathew” akasema Austin.Baada ya muda kidogo Mathew akauliza

“Tukio hili limetokeaje?Nani waliompiga risasi Gosu Gosu?

“Mpaka sasa haifahamiki nani waliofanya tukio hili.Taarifa za Gosu Gosu kupigwa risasi nilizipata kutoka kwa mchumba wake anaitwa Melanie.Alinipigia simu usiku na kunijulisha kwamba Gosu Gosu yuko hospitali amepigwa risasi ndipo nikaja hapa mara moja na kumkuta akiwa

ametoka kufanyiwa upasuaji na alikuwa anaendelea vyema lakini usiku hali yake ikabadilika akalazimika kuwekwa katika mashine ya kumsaidia kupumua” akasema Austin

“Gosu Gosu tayari ana mchumba?Yuko wapi? Mathew akauliza

“Hata mimi sikuwa nikifahamu alifanya siri.Baada ya tukio hili kutokea ndipo nikamfahamu.Aliniaga juzi kwamba atakuwa na safari lakini hakunieleza anakwenda

wapi na toka wakati huo sijamuona tena hapa hospitali wala kupiga simu kuulizia hali ya mchumba wake ikoje” akasema Austin

“Kwa maelezo aliyonipa Melanie ni kwamba Gosu Gosu alikuwa anatoka ofisini kwake nyakati za jioni na wakati akijiandaa kuingia katika barabara kuu ikatokea piki piki ikiwa na watu wawili wenye silaha wakaanza kulishambulia gari la Gosu Gosu kwa risasi.Walikuwa na lengo la kumuua kabisa lakini

kilichomsaidia akanusurika ni fulana isiyopenya risasi aliyokuwa ameivaa.Ilimsaidia kuzuia risasi nyingi kuingia mwilini.Nimekuwa nikifuatilia kwa jeshi la polisi kama kuna mtuyeyote amekamatwa kuhusiana na suala hili lakini mpaka leo hii hakuna aliyekamatwa ila uchunguzi unaendelea" akasema Austin

"Kikubwa kwa sasa ni kumuombea ili apone.Yeye ndiye mwenye majibu yanani waliompiga risasi na yawezekana labda aliwaona

kwa macho.” akasema Mathew na ukimya mfupi ukapita

“Nimefurahi kukuona Austin.Vipi maendeleo yako? Akauliza Mathew

“Mimi ninaendelea vyema lakini bado niko kwenye mstuko mkubwa.Sikutegemea kabisa kukuona hapa” akasema Austin lakini Mathew

“Hata mimi sikutegemea kabisa kama ningekukuta hapa.Sikujua kama ulisalimika usiku ule” akasema Mathew

“Nilisalimika Mathew lakini tulipoteza watu wengi sana

usiku ule na wote tuliamin……..” akasema Austin lakini Mathew akamkatisha

“Austin tuna mengi ya kuzungumza na mazingira haya si rafiki sana.Tutafute sehemu nzuri tutulie tuzungumze” akasema Mathew na haraka haraka Austin akaenda kuzungumza na wauguzi kisha akamfuata Mathew akamtaka waondoke.

“Jaribu kumpigia simu huyo mchumba wa Gosu Gosu ninataka kuonana naye” akasema Mathew na Austin

akapiga simu lakini simu ya Melanie haikuwa ikipatikana

“Hapatikani simuni” akasema Austin

“Unafahamu anakoishi?

“Hapana sifahamu.Kwa ujumla simfahamu vyema huyo mwanamke.Nimefahamiana naye hapa hapa hospitali na hatujapata nafasi ya kuzungumza kujuana vizuri.Nimeshangaa kwa Gosu Gosu kutonijulisha kuhusu suala hili la kuwa na mchumba wakati masuala yake karibu yote huwa ananijulisha”

akasema Austin.Mathew akakata kona kuingia katika hoteli iliyokuwa karibu na hospitali.Wakatafuta sehemu tulivu wakaketi muhudumu akafika na kuagiza vinywaji

“Austin najua una maswali mengi unataka kufahamu kuhusu mimi.Nilikuwa wapi na yote yaliyonitokea lakini nakuomba usiniulize chochote kuhusu suala hilo.Kitu cha msingi ni kufahamu tu kwamba niko hai inatosha” akasema Mathew

“Ni kweli Mathew kuna mengi ninataka kuyafahamu.Kuanzia usiku ule wa tukio hadi leo hii ulipotokea.Hakuna aliyeamini kama uko hai kufuatia shambulio lile baya” akasema Austin.Mathew akanywa kinywaji chake kidogo kisha akauliza

“Did you search for me? Akauliza Mathew.Swali lile lilimfanya Austin abaki kimya

“Answer me Austin.Baada ya tukio la usiku ule mlijaribu

kunitafuta kujua mahala nilipo?akauliza Mathew

“Rais alituma kikosi maalum siku iliyofuta kwenda kukutafuta lakini ni kikosi hicho kilichorejea na majibu kwamba kuna uwezekano mkubwa uliuawa na kuliwa na fisi” akasema Austin

“Siulizi kuhusu Rais nauliza kuhusu wewe.Did you search for me? Akauliza Mathew na Austin akabaki kimya

“Wewe ndiye uliyeongoza kikosi cha pili ambacho jukumu lake kubwa lilikuwa ni kulinda

kikosi cha kwanza ambacho nilikuwa nakiongoza mimi.Baada ya shambulio lile kutokea ukiwa kama kiongozi ulijaribu kunitafuta? Akauliza Mathew na Austin akafikiri kidogo kisha akasema

“Baada ya shambulio lile la ghafla kukoma tulianza kukusanya miili ya watu wetu na karibu kikosi chako chote ulichokuwa unakiongoza kiliuawa na miili ikapatikana lakini ni wewe pekee uliyekosekana.Niliwaelekeza watu wangu tuendelee

kukutafuta tukagundua pia kwamba watu wa IS nao karibu wote walikuwa wameuawa lakini Edger Kaka hakuwa miongoni mwao.Tuliamini labda umejificha sehemu Fulani karibu na pale lakini wakati tukiendelea kukutafuta taarifa zilimfikia Rais ambaye kwa wakati huo alikuwa kambini akifuatilia kwa karibu tukio lile na akaamuru tuondoke haraka sana eneo lile.Nilimueleza kwamba wewe umekosekana lakini akaamuru niondoe kikosi mhala pale kwani tayari ilikuwa

ni hatari kwetu.Kama tungeendelea kukaa pale kukutafuta tungeendelea kuwaweka hatarini hata wale mateka tuliowakomboa hivyo nikaondoa kikosi.Samahani sana Mathew mzigo wote wa lawama nastahili kuubeba mimi" akasema Austin

"Hustahili lawama.Ulitimiza amri uliyopewa na mkuu wako.Najua usingekubali kuniacha porini kwani siku zote kiongozi unapopewa kikosi ukiongoze katika misheni Fulani unapaswa kuwarejesa

watu wako wote nyumbani wakiwa wazima au wamekufa”

“Ahsante Mathew kwa kulitambua hilo lakini ni jambo ambalo limekuwa likinitesa sana moyoni kwamba sikufanya juhudi za kutosha usiku ule kukutafuta”

“Austin usibebe lawama ambazo hustahili.Tuachane na hayo vipi kuhusu wale mateka tuliokwenda kuwakomboa walifika nyumbani salama?

“Wote walifika nyumbani salama”

“Pamoja na yote yaliyotoea lakini kumbe misheni ilifanikiwa.Vipi kuhusu Olivia huwa mnaonana?

“Mara chache sana huwa tunaonana.Taarifa za kifo chako zilimumiza mno” akasema Austin

“Vipi kuhusu Ruby mnawasiliana?akauliza Mathew

“Ruby amekuwa akiwasiliana na Gosu Gosu mara kwa mara na kwa sasa anafanya kazi katika mamlaka kuu ya mawasiliano ya kiintelijensia nchini Uingereza GCHQ”

“Anafanya kazi GCHQ?

“Ndiyo.Mahusiano yangu naye si mazuri toka wakati ule ulipopotea na ananilaumu mimi kwa kile kilichotokea na kusababisha kile ambacho wengi tuliamini kifo chako.Mara ya mwisho kuwasiliana naye ni miezi kadhaa imepita.Mimi na Gosu Gosu tulihitaji msaada wake katika misheni Fulani muhimu sana”

“Misheni ipi?akauliza Mathew

“Ilikuwa ni misheni moja muhimu sana kwa nchi na

ambayo ilileta kiza zaa kikubwa” akasema Austin

“Ilihusu nini hiyo misheni? Mathew akauliza

“Tulitakiwa kumuua mwanasiasa mmoja wa kutoka jamhuri ya kidemokrasia ya Congo” akasema Austin

“Nini ilikuwa sababu ya kutaka kumuua?Nieleze kwa undani zaidi jambo hilo”akasema Mathew

“Mheshimiwa Rais Dr Fabian alipewa taarifa na Rais Patrice Eyenga wa Congo kwamba kuna mwanasiasa

mmoja anatumiwa na mataifa ya nje katika mpango wa kuisambaratisha jumuiya ya Afrika mashariki.Rais wa sasa wa Congo Patrice Eyenga amefanikiwa kumaliza mchafuko yaliyoitawala nchi hiyo kwa muda mrefu na hilo halijawapendeza nchi kubwa waliokuwa wakifaidika na machafuko hayo ndiyo maana wakataka kumtumia mwanasiasa huyo ili awe daraja la kuwavusha kurejea tena kuendelea kuinyonya Congo.Baada ya kupewa taarifa

hiyo Ras Dr Fabian alitupa sisi kazi ya kumuondoa mwanasiasa huyo aliyeitwa Lucy Muganza”

“Mwanasiasa huyo alikuwa ni mwanamke?Mathew akauliza

“Ndiya alikuwa ni mwanamama bilionea.Nikishirikiana na Gosu Gosu na vijana wengine tulifanikisha misheni hiyo na kumuua Lucy Muganza na mume wake Laurent Muganza.Baada ya mauaji hayo kuna makosa yalifanyika.Tulipomuua Lucy

Muganza na mumewe tulitakiwa kwenda mbali zaidi lakini tulijisahau na miili le ikafanyiwa uchunguzi na ikagundulika kwamba risasi zilizotumika katika mauaji hayoni kutoka katika bunduki zinazotumiwa na wadunguaji na taarifa hiyo ikamfikia balozi wa umoja wa Ulaya hapa nchini ambaye aliendelea kuishinikiza serikali kuruhusu wachunguzi wa kutoka umoja wa ulaya kuja chini kuchunguza mauaji yale.Balozi huyo alikuwa na taarifa kwamba bunduki

ambazo zilitumika kuwaua Lucy Muganza na mumewe zinamilikiwa na jeshi na hapo ndipo Rais akatutaka tumchunguze balozi huyo tujue anapata wapi taarifa nyeti kama hizo za kuhusiana na silaha za nchi.Ilitulazimu kumuomba msaada Ruby katika kumchunguza balozi huyo na ndipo nilipofahamu kuwa anafanya kazi katika mamlaka kuu ya mawasiliano ya kiintelijensia nchini Uingereza.Tulifanikiwa kugundua kwamba balozi huyo

alikuwa na mawasiliano ya karibu na mkurugenzi wa idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi aliyejulikana kama Tamar.Kwa bhati mbaya kabla ya kupiga hatua kubwa kumchunguza balozi huyo aliuawa” Austin akaendelea kumueleza Mathew kwa undani namna misheni ilivyokuwa hadi pale ambapo mambo yalikuja kutulia

“Dah ! hongereni sana kwa kazi kubwa mliyoifanya.Nimefurahi kwa namna mlivyoendesha misheni

hiyo.Umeniambia kwamba mlimshauri Rais amuite Ruby nyumbani ili awe mkurugenzi wa ile idara ya SNSA”

“Ndiyo.Tulimshauri hivyo mheshimiwa Rais na aliahidi kulitekeleza hilo suala lakini mpaka leo hatujapata mrejesho wowote kutoka kwake amefikia wapi katika suala hilo la kumshawishi Ruby aweze kuja hapa nchini” akasema Austin

“Ahsante sana kwa kumshauri Rais jambo hilo.Idara ile ni muhimu sana kwa nchi lakini tayari mabeberu

wamekwisha pandikiza watu wao.Naamini hata baada ya Tamar kuondoka bado kuna mapandikizi yamebaki kwani hawezi kuwa peke yake lazima wawepo watu aliokuwa anashirikiana nao ambao wataendeleza kufanya kile wanachokitaka mabeberu.Ruby ni chaguo zuri na anafaa sana kuongoza idara kama ile.Kuna ulazima wa kufuatilia kujua Rais amefikia wapi katika suala hilo.Una namba za simu za Ruby?akauliza Mathew

“Hapana sina nanba zake.Ni Gosu Gosu ndiye aliyekuwa akiwasiliana naye”

“Simu ya Gosu Gosu iko wapi?

“Sifahamu mahala ilipo simu hiyo” akajibu Austin.

“Unafahamu anakoishi Rais mstaafu Dr Evans?akauliza Mathew

“Ndiyo ninafahamu.Anaishi katika nyumba yake mpya” akajibu Austin

“Nipeleke huko nahitaji kuonana naye” akasema Mathew huku akisimama

wakaondoka kuelekea katika gari la Mathew ambaye alimtaka Austin aendeshe kwa kuwa yeye hakuwa na leseni.Austin akaondoa gari wakaondoka kuelekea katika makazi ya Rais mstaafu Dr Evans.

****

Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania Dr Fabian Kelelo aliwasili katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere akitokea

mkoani Mbeya katika mazishi ya mke wake Millen Kelelo.Kutoka katika uwanja wa ndege wa Julius Nyerere Dr Fabian alielekeza apelekwe katika nyumba yake aliyokuwa akiishi kabla ya kuwa Rais.

Ruby akiwa amepumzika ndani ya chumba chake alistushwa na muungurumo wa magari akainuka kuchungulia nje kupitia dirishani akayaona magari ya msafara wa Rais yakijipanga

“Rais amekuja” akasema Ruby na haraka haraka

akaelekea katika meza ya vipodozi akaanza kurekebisha uso wake kabla ya kukutana na Rais.Akiwa katika kujiandaa mlango wake ukagongwa.Akajitazama katika kioo halafu akaenda mlangoni akaufungua akakutana na walinzi wawili ambao walimtaka aongozane nao wakaelekea hadi sebuleni ambako alimkuta Rais Dr Fabian akiwa ametulia sofani.Akasimama baada ya Ruby kuingia

“Ruby ! akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais shikamoo”

“Marahaba Ruby vipi maendeleo yako?

“Ninaendelea vyema mheshimiwa Rais” akasema Ruby na Rais akamfanyia ishara aketi

“Pole sana mheshimiwa Rais” akasema Ruby

“Ahsante Ruby nimekwisha poa.Ni mapito ya mwanadamu na sote njia yetu ni hiyo isipokuwa mwenzetu ametutangulia.Japo nina

majonzi lakini nimefurahi kukuona Ruby karibu sana.Jana nilishindwa kurejea kama nilivyokuahidi niliombwa na wazee nibaki kwa ajili ya kukamilisha mambo ya kimila.Naamini umekuwa ukihudumiwa vizuri” akasema Dr Fabian

“Usijali mheshimiwa Rais.Nafahamu unapitia kipindi kigumu hivyo hata kama ingenichukua mwezi mzima kukusubiri hakuna tatizo kwa upande wangu kwani hapa niko nyumbani” akasema Ruby

“Ruby napenda kwanza kabla ya yote kukupa pole nyingi sana kwa yote uliyopitia katika safari ya kuja hapa.Najua mimi ndiye sababu ya mambo yale yote kutokea kwa kukutaka uache kazi uliyokuwa unaifanya uje nyumbani.Umepitia mambo magumu sana hata kunusurika kifo.Nilipoona jina lako katika orodha ya watu waliofariki katika ile ajali ya ndege nilijilaumu mno kwa kukuomba uje nyumbani lakini nakushukuru kwa namna ulivyopambana kuhakikisha

unafika salama Tanzania.Naamini hii yote ni mipango ya Mungu kwani umefika katika kipindi ambacho unahitajika sana” akasema Dr Fabian

“Ni kweli mheshimiwa Rais nimepitia mambo magumu hadi kufika hapa.Kazi niliyokuwa naifanya nchini Uingereza iliniwezesha kufahamu mambo mengi sana ya siri hivyo nilipowasilisha maombi ya kuacha kazi walistuka na walifanya kila mbinu kunishawishi nibatilishe

mpango wangu huo wa kuacha kazi lakini niliendelea kushikilia msimamo wangu na ndipo walipoamua kupanga mpango ule wa kuniua.Ulikuwa ni mpango wa siri sana na ninamshukuru mmoja wa marafiki zangu ambaye aliweza kunijulisha kile kilichokuwa kimepangwa dhidi yangu na akanisaidia hadi nimefika hapa.Ilikuwa ni safari ndefu na ngumu kwangu lakini namshukuru Mungu nimefika salama nikiwa na afya njema” akasema Ruby

“Kwa nini walikuwa na hofu ya wewe kuacha kazi?akauliza Dr Fabian

“Edward Snowden wa Marekani amewapa fundisho ndiyo maana walistuka sana na walihisi labda na mimi nina mpango kama ule wa kutoa siri zao.Waliamini nimelipwa pesa nyingi ili niweze kuuza siri ndiyo maana suluhisho pekee walilokuwa nalo ni kuniua.Ninasikitika kwamba maisha ya watu wengi yalipotea kwa sababu yangu” akasema Ruby

“Pole sana Ruby.Ninakuahidi kukulinda kwa kila namna dhidi ya hawa jamaa ambao mpaka sasa wanaamini tayari umekwisha fariki”

“Nashukuru sana mheshimiwa Rais”

“Mimi ndiye ninayepaswa kukushukuru wewe kwa niaba ya watanzania.Kitendo ulichokifanya ni cha kizalendo.Umeacha kazi uliyokuwa ukiifanya ambayo ilikuwa na maslahi manono na ukakubali kuja kuitumikia nchi

yako.Ni uzalendo wa hali ya juu sana” akasema Dr Fabian

“Tanzania ni nchi yangu na lazima niitike ndiyo kila pale ninapoitwa kuitumikia.Mheshimiwa Rais niko tayari kwa ajili ya kazi ya kuitumikia nchi yangu” akasema Ruby

“Karibu sana Ruby.Kwa kuwa kwa sasa nina ratiba nyingine nitakuomba jioni ya leo ikulu kwa ajili ya chakula kisha tutazungumza kwa kirefu sana kuhusiana na kazi ambayo

nimekuita uje kuifanya”
akasema Dr Fabian

“Nitafika mheshimiwa Rais”
akasema Ruby na Dr Fabian
akasimama na kumpa mkono

“Ruby kwa mara nyingine
tena karibu Tanzania.Karibu
nyumbani” akasema Dr Fabian
kisha akaagana na Ruby
akaondoka.

KAMPALA – UGANDA

Gari nne aina ya range rover zenye rangi nyeupe zilifika katika nyumba ambayo alifikia Melanie.Ulikuwa ni msafara wa James Kasai ambaye alishuka na kuingia ndani ya jumba lile.Melanie akiwa chumbani kwake akafuatwa na mmoja wa wahudumu akaitwa akatoka kwenda kukutana na James Kasai aliyekuwa sebuleni.

“James Karibu sana” akasema Melanie

“Nashukuru sana Melanie.Habari za toka juzi?akauliza James Kasai

“Ninaendelea vizuri sana sina tatizo lolote.Unapendeza sana ukivaa suti kuliko yale mavazi yako ya kijeshi”akatania Melanie na wote wakaangua kicheko

“Nashukuru kusikia hivyoMelanie lakini nimezoea sana kuvaa mavazi yale ya jeshi kwa kuwa muda wote niko katika mapambano.Samahani kwa kutokuja kuonana nawe siku ya jana”

“Usijali James ninaelewa.Nimekupigia simu ili tuje tuzungumze kuhusiana na lile suala letu.Umekwisha pata mrejesho wowote kutoka kwa Rais?akauliza Melanie

“Hapana sijapata mrejesho wowote bado kutoka kwa Rais.Alituahidi angewasiliana nasi jana lakini hakufanya hivyo.Wewe hujapata chochote kutoka kwake? Akauliza James na Melanie akatoa kicheko kidogo

“Hawezi kuwasiliana nami kabla hajakujulisha kwanza

wewe.Hata hivyo dhumuni la kukuita hapa kuna jambo nataka tulijadili kuhusiana na ule mpango wetu wa kumuua Patice Eyenga”

“Karibu”akasema James

“Juzi tulipokwenda kuzungumza na Rais alitueleza kwamba anataka kushirikiana nawatu kutoka ndani ya serikali ya Congo katika mpango wa kumuua rais Patrice Eyenga.Anachotaka kukifanya Rais Akiki si kitu kibaya lakini tatizo la huo mpango wake ni kwamba utachukua muda

mrefu kwanza kuwashawishi watu waweze kukubaliana na mpango huo na vile vile upo uwezekano kwamba watu hao ambao anataka kuwashirikisha wakakataa kushirikiana naye.Kama ikitokea watu hao wakakataa kushirikiana naye mpango utakuwa umekwama na siri itakuwa imevuja kwamba Rais Patrice anataka kuuawa.Nimelitafakari sana hilo nikaamua kuja na mpango mpya ambao tutauwasilisha kwa Rais Akiki" akasema Melanie na kunyamaza kidogo

“Mpango gani umekuja nao?akauliza James

“Kwa hivi sasa Uganda na Congo hazina maelewano mazuri.Hii ni fursa ambayo tunatakiwa kuitumia.Jenerali Akiki atawasiliana na Rais wa Tanzania ambaye ndiye mwenyekiti wa jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sasa na atamuomba wakutane pamoja na rais wa Congo ili kutafuta suluhu ya mgogoro unaoendelea hivi sasa na kikao hicho kifanyike jijini Dar es salaam.Wakati kikao hicho

kikiendelea tutapandikiza bomu katika ndege ya Rais Patrice na pale atakapokuwa angani akirejea Congo tutailipua ndege yake.Ni mpango ambao hautahitaji mtandao mkubwa kama anaotaka kuutengeneza Rais Akiki na vile vile hautachukua muda mrefu.Unauonaje mpango huo?akauliza Melanie.James akafikiri kidogo na kusema

“Ni mpango mzuri japo nao una changamoto yake.Changamoto kubwa ni namna ya kulipandikiza hilo

bomu katika ndege ya Rais ambayo inakuwa na ulinzi mkali wakati wote” akasema James

“Ndiyo maana nikauita hapa ili tuweze kujadiliana suala hilo.Mimi kwa upande wangu ninaweza kutengeneza mtandao ambao unaweza ukatusaidia kuingiza bomu katika ndege hiyo ya Rais Patrice ”akasema Melanie

“Hilo ndio hasa kubwa tunalolihitaji katika huo mpango.Kama unao uwezo wa kutengeneza mtandao unaoweza kutusaidia basi

hakuna tatizo tunaweza kuendelea na mpango huu”akasema James

“Katika huo mpango tutawahitaji watu wa IS.Baada ya mlipuko kutokea na Patrice kuuawa IS watajitokeza na kudai kwamba wao ndio waliohusika katika shambulio hilo bila kutoa sababu yoyote.Hakuna ambaye atajua umehusika bali mzigo wote wataubeba IS.Baada ya kifo cha Patrice jeshi naamini linaweza kutangaza kuchukua nchi na hapo ndipo machafuko

yatakapoanza na wewe utaendelea na mapambano na serikali na safari hii ukiwa na jeshi lenye nguvu na zana za kisasa.”akasema Melanie

“Kweli ni mpango mzuri na hata mimi nimeupenda sana hivyo basi tuanze maandalizi.Kwanza tuanze kwa kuzungumza na Rais Akiki.Nitawasiliana naye kumueleza kwamba tunahitaji kuzungumza naye na tukikutana nitajaribu kumshawishi aukubali mpango huu ambao naamini hataweza

kuukataa hivyo jambo kubwa ni kuandaa namna bomu hilo litakavyoweza kuingizwa katika ndege ya Rais.Hata hivyo kuna kitu ninakiwaza.Kwa nini bomu hilo lisiingizwe ndegeni jijini Kinshasa? Tunaweza kumchagua rubani mmoja wa ndege ya Rais tukaiteka familia yake na kumlazimisha aliingize sanduku lenye bomu ndani ya ya ndege ya Rais wakati akijiandaa na safari ya kuja Tanzania na Rais Patrice auawe kabla hajafika Dar es salaam.Unaonaje wazo hilo?

“Ni wazo zuri pia.Tutayajadili haya yote na Rais Akiki pale tutakapokutana naye.James mimi ninafanya hivi kwa ajili ya kulipiza kisasi kwa wazazi wangu lakini wewe fanya kwa ajili ya harakati zako za kuiomboa Congo.Kama alivyosema Jenerali Akiki kwamba ni wewe pekee ambaye unapambana kwa maslahi mapana ya Congo lakini wengine wote wanapambana kwa maslahi yao na wakubwa wanaowafadhili hivyo hakikisha mapambano yanandelea na siku

moja unafanikiwa kuingia hadi Kinshasa”
akasema Melanie

“Melanie ahsante kwa ushauri huo mzuri.Ni kweli kama alivyosema Rais Akiki kwamba ninapambana kwa ajili ya maslahi ya Congo na ndiyo maana siungwi mkono na taifa lolote la Ulaya bali anayeniunga mkono ni Rais Akiki pekee ambaye anafahamu nia yangu ya dhati ya kuikomboa Congo.Ninakuahidi kwamba mapambano yataendelea hadi pale nitakapohakikisha

nimeitawala Congo” akasema James

“Kuhusu IS umepanga kushirikiana nao hadi lini? Melanie akauliza

“IS nitaendelea kushirikiana nao kwa ajili ya kuniwezesha kijeshi.Kwa sasa ninahitaji kikosi chenye nguvu kubwa hivyo basi nategemea kupata silaha kali na za kisasa kutoka kwao.Mkataba wa mashirikiano yangu nao ni kwa ajili ya kuwasaidia kujenga kambi yao ya mafunzo katikati ya misitu”

“Ni vipi kama baadae likawa jeshi kubwa na wao pia wakaanza kupigana na serikali? Akauliza Melanie

“Wanachokitaka wao ni sehemu ya kufanyia mafunzo kwa watu wao ambao watawatuma sehemu mbalimbali duniani.Hawana mpango wowote wa kushambulia Congo” akasema James

“James nimeuliza swali hilo kwa sababu watakapopata sehemu ya kuweka kambi ya mafunzo wataanza kujiimarisha

taratibu na pale watakapokuwa na jeshi kubwa basi wataanzisha mapigano na serikali na kama unavyojua hawa jamaa wakikita mizizi yao sehemu Fulani kuwaondoa huwa vigumu sana” akasema Melanie

“Usiwe na hofu Melanie.Nimekwisha kubaliana nao kuwasaidia kupata kile wanachokitaka na mimi niweze kupata kile ninachokitaka.Tuachane na suala hilo una taarifa zozote za Gosu Gosu?

“Sijapiga simu nyumbani kuuliza hivyo sijui kinachoendelea kuhusu hali yake” akasema Melanie

“Melanie unatakiwa kumjulia hali mpenzi wako.Piga sim…” akasema James na Melanie akamkatisha

“Nitawasiliana nao kujua maendeleo yake usihofu” akasema na James akamuaga kwa ahadi ya kumpa mrejesho baadae pale atakapokuwa amezungumza na Jenerali Akiki.

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Gari la akina Mathew lilisimamishwa na askari waliokuwa wakilinda geti la kuingilia nyumbani kwa Rais mstaafu wa jamhuri ya muungano wa Tanzania Dr Evans.Hawakuwa na miadi ya kuonana na Dr Evans hivyo mmoja wa askari akapiga simu ndani ikapokelewa na mtumishi wa ndani akamuomba azungumze na Dr Evans akamjulisha kuwa kuna wageni wake ambao ni Austin January

na mwenzake wamefika kuonana naye.Baada ya kuzungumza na simu askari Yule akaelekeza geti lifunguliwe na akina Austin wakaruhusiwa kuingia ndani.

“Umewahi kuja huku?akauliza Mathew

“Ndiyo nimekuwa nikifika mara kadhaa kumsalimu mzee” akajibu Austin.

Waliegesha gari na kushuka.Mmoja wa watumishi wa Dr Evans akaenda kuwapokea na kuwaongoza

kuelekea ndani.Austin alitangulia mbele na Mathew akamfuata nyuma.Aliwakaribisha sebuleni akawahudumia vinywaji halafu akaenda kumuita Dr Evans.Baada ya dakika chache Dr Evans akatokea akiwa ameshika gazeti mara gazeti alilolishika likaanguka chini baada ya kukutanisha macho na Mathew Mulumbi.

“Jesus Christ ! akasema huku akigeuka na kutazama nyuma kama vile alitaka kukimbia

“Shikamoo mzee” akasema Austin

“Mar..marahaba Austin ! akaitika Dr Evans huku macho yake akiwa bado ameyaelekeza kwa Mathew.

“Shikamoo mzee”akasema Mathew na Dr Evans akamtazama Austin

“Is this real?akauliza

“It’s real mr President” akajibu Austin.

Mara Dr Evans akashika kifuani na kunza kupepesuka akataka kuanguka.Austin

akamuwahi akamdaka na kumkalisha sofani

“My pills” akasema Dr Evans kwa taabu.Mathew akamuita mtumishi wa Dr Evans na kumtaka aonyeshe zilipo dawa za mzee.Mtumishi Yule akakimbia na kwenda kuleta kichupa kidogo cha dawa akatoa dawa mbili na kumpa Mathew ambaye alimpa Dr Evans akanywa haraka haraka kisha akalazwa sofani.

“Mzee amekuwa akisumbuliwa na matatizo ya moyo na tatizo kama hili

limekuwa likimtokea mara kwa mara” akasema Yule mtumishi wake.Mathew akamuelekeza ampigie simu daktari wake.

“Mathew utaua watu kwa mstuko.Kila anayekuona anapatwa na mstuko mkubwa.Hakuna anayeamini kama bado uko hai mpaka sasa.Hata mimi nilipatwa na mstuko mkubwa na nilichuchumaa chini kwa kuwa miguu iliniisha nguvu” akasema Austin

“Naomba ujio wangu usije ukasababisha maafa” akasema Mathew.

Daktari wa Dr Evans alifika akampima na kumkuta anaendelea vizuri.

“Hakuna tatizo anaendelea vyema” akasema Daktari na kumpa maelekezo Yule mtumishi kisha akaondoka

“Mlinzi wa mzee yuko wapi?Alipaswa kuwa naye hapa” akasema Mathew

“Mlinzi wa mzee amepata dharura ndiyo maana leo

hayupo” akajibu Yule mtumishi.Dr Evans akainuka sofani na kuketi

“Mzee unajisikiaje? Akauliza Austin

“Najisikia vizuri” akajibu Dr Evans

“Pole sana mzee” akasema Mathew

“Mathew ..” akasema Dr Evans na kutaka kunyanyuka lakini Mathew akamtaka aketi.Akaendelea kumtazama kwa macho yaliyojaa hofu.

“I can’t believe this.Ni wewe kweli Mathew Mulumbi? Akauliza Dr Evans

“Ni mimi mzee.I’m still alive” akajibu Mathew

“I’m so sorry Math……”

“Usijali mzee.Austin tayari amekwisha nieleza kila kitu kilichotokea” akasema Mathew

“Mathew ninatamani hata niyapofue macho yangu nisiweze kukutazama usoni.Ninaona aibu.Ulifanya jambo kubwa sana kwa nchi na kwangu pia.Uliwakomboa

watoto waliokuwa wametekwa na magaidi na vile vile ukamkomboa mwanangu aliyekuwa mikononi mwa magaidi lakini kama alivyokueleza Austin usiku ule lilipotokea lile shambulio baya kabisa nilifanya maamuzi magumu ya kumtaka akiondoe kikosi kile na miili yote iliyopatikana.Nilihofia kungekuwa na shambulio lingine na yawezekana tungeweza hata kupoteza kikosi kizima.Nakiri yalikuwa ni maamuzi magumu sana

kuyafanya katika kipindi changu chote cha urais.Nilikubali kikosi kiondoke na kumuacha mtu muhimu kabisa kwa taifa.Siku iliyofuata nilituma tena kikosi kingine kwenda eneo la tukio kutafuta kama wangeweza kukupata walau hata mwili wako lakini hawakupata kitu chochote na taarifa waliyoirejesha ni kwamba utakuwa ulifariki dunia na maiti yako kuliwa na fisi kwani walikuta kuna mabaki kadhaa ya maiti zilizoliwa na fisi eneo

lilipofanyika lile shambulio.Baada ya kupewa taarifa ile nilituma ujumbe kwa mke wako Peniela jijini Paris Ufaransa kumfahamisha kilichotokea na kumpa pole sana.Hakuna aliyejua kama uko hai Mathew tusamehe sana" akasema Dr Evans

"Mheshimiwa Rais nafahamu yalikuwa ni maamuzi magumu kabisa uliyafanya na siwezi kukulaumu kwani hata mimi ningekuwa mahala pako ningefanya hivyo hivyo lakini unapotuma watu katika misheni

Fulani lazima uhakikishe wote wanarejea nyumbani wawe wazima au wamekufa.Watu wanapotumwa misheni Fulani wanakwenda kupambana kwa ajili ya nchi hivyo lazima hata kama wamefariki wazikwe kishujaa katika ardhi ya nyumbani kwao.Kilichofanyika kwangu kiwe somo wakati mwingine kuwathamini wale wanaotumwa kupambana kwa maslahi ya nchi.Hata hivyo ninataka kujua baada ya taarifa kurudi kwamba nimeliwa na fisi mlichukua hatua

zipi?Mlithubutu hata kutengeneza kaburi mkazika hata kiatu changu kuonyesha kunithamini? Akauliza Mathew

“Hatukufanya hivyo” akasema Dr Evans

“Hukuwa na mawazo hayo kwa kuwa kile ulichokuwa unakihitaji ulikwisha kipata.Mwanao alikombolewa na hukujisumbua tena kuhusu Mathew Mulumbi.Hukutaka hata kutuma timu ya kufanya uchunguzi wa kina kufahamu nini kilitokea.Ulifanya hivyo?

“Hatukufanya hivyo” akajibu Dr Evans

“Mpaka leo hamjui nini hasa kilitokea usiku ule! Hamjui nani walitushambulia na kwa nini! Hukutaka kusumbuka kwa sababu mwanao alikuwa amepatikana.Katika orodha ya watu waliofariki dunia kwenye ile misheni mlithubutu hata kuliweka jina langu? Akauliza Mathew na wote wakawa kimya

“Mheshmiwa Rais ninaipenda sana nchi yangu lakini ninyi viongozi mnakatisha tamaa wazalendo

kama mimi ambao wako tayari kumwaga damu yao kwa ajili ya nchi.Licha ya mchango mkubwa nilioutoa kwa nchi yangu lakini bado thamani ninayoipata ni ndogo mno.Hata hivyo siko hapa kuomba nithaminiwe kwani ni Mungu pekee atakayeweza kunilipa lakini ninataka kuwaeleza mtambue makosa mliyoyafanya.Najua hauko katika uongozi hivi sasa lakini unayo sauti na unasikika ukiongea hivyo basi nataka uwashauri walio katika madaraka hivi sasa

kuwathamini watu kama mimi,kama Austin watu kama Gosu Gosu ambaye hivi sasa yuko mahututi akipigania maisha yake.Hatuombi litokee kwani Mungu ndiye mpanga yote lakini anaweza akapoteza maisha na akifariki ndiyo anasahaulika kabisa.Nataka uwabadilishe viongozi walio madarakani wawe na uthubutu wa kuthamini mchango wa wale wanaojitolea kwa ajili ya nchi yao.Wapo wanajeshi,askari polisi na wengine kutoka vyombo mbali mbali vya ulinzi

na usalama.Mnawajali vipi pindi wakistaafu utumishi au wakiumia wakiwa kazini? Fikisha ujumbe huu kwa wenzako walio madarakani ”akasema Mathew kisha akavua fulana aliyokuwa ameivaa akafungua fulana ya kuzuia risasi aliyokuwa ameivaa ndani na kuwaonyesha Austin na Dr Evans makovu yaliyoko mwilini mwake

“Dah ! akasema Austin

“Haya ndiyo niliyopitia.Mwili wangu wote

umechafuliwa na makovu ya vidonda” akasema Mathew

“Pole sana Mathew.Unaweza ukatueleza nini hasa kilichotokea?Ulikuwa wapi? Akauliza Dr Evans

“Lengo la kuja hapa si kueleza mahala nilikokuwa na yapi nimepitia.Ukurasa huo umekwisha fungwa lakini nilitaka tu kuwapa somo kwamba mlichokifanya kilikuwa ni kitu kibaya kabisa” akasema Mathew

“Mathew ninakosa maneno ya kusema kijana wangu” akasema Dr Evans

“Usiseme chochote.Sikuja hapa kwa malumbano au kwa hasira kwa nini mlinicha porini lakini kubwa lililonileta hapa ni kukujulisha kwamba niko hai na sijafa kama mlivyoamini” akasema Mathew na Dr Evans akavuta pumzi ndefu

“Mathew hapa nilipo sijitambui kama nina furaha au majonzi lakini kikubwa ambacho ninataka kukwambia kwamba watu kama wewe

huzaliwa wachache sana katika dunia ya sasa.Kwa nini ninasema hivyo? Ni kwa sababu kwa sasa nchi yetu iko katika mgogoro mkubwa na kati kati ya mgogoro huo umeibuka kutoka kusikojulikana.Mathew unaongozwa na roho wa Mungu ndani yako ndiyo maana umetokea kwa wakati huu ambao nchi hii inakuhitaji sana" akasema Dr Evans

"Sijakuelewa mzee nchi inanihitaji kivipi?Walijua nitarejea?Wanafahamu mahala nilikokuwa?Wanafahamu

niliyoyapitia hadi umeniona hapa leo?akauliza Mathew

“Hakuna aliyefahamu mahala ulipo,hakuna aliyekuwa anafahamu kama utakuja lakini nchi ilikuhitaji sana mtu kama wewe.Umetokea wakati ambao ni muafaka kabisa.Mathew Mungu amekuleta kwa wakati huu isikie sauti yake na uisaidie nchi” akasema DrEvans

“Mzee sijakuelewa nini unakimaanisha” akasema Mathew

“Mathew naamini Austin amekwisha kueleza kile ambacho kimetokea hapa nchini siku chache zilizopita kama bado hujasikia katika vyombo vya habari huko ulikokuwa”

“Ninafahamu kilichotokea mzee.Ninafuatilia kila siku taarifa za nyumbani kujua kila tukio linalotokea hapa” akasema Mathew

“Nashukuru kama unafuatilia habari za nyumbani. Kinachoendelea hivi sasa ni mpango wa kuisambaratisha

jumuiya ya Afrika Mashariki.Huu ni mpango wa nchi kubwa kutugawanya.Kikubwa wanachokitaka ni kuvuruga umoja wetu kila nchi ikae peke yake ili wapate nafasi nzuri ya kutunyonya.Huu ni mkakati mzito san…..”akasema Dr Evans na Mathew akamkatisha

“Mzee ninafahamu kila kitu kinachoendelea hapa nchini na kila kitu kuhusiana na mpango huu wa kuigawanya afrika Mashariki.Ninafahamu nchi inayolengwa zaidi katika

mpango huu ni jamhuri ya kidemokrasia ya Congo.Wanataka machafuko yarejee nchini Congo ili wapate nafasi ya kurejea kuchuma mali za nchi hiyo.Ninafahamu kila kitu mzee huna hja ya kuelezea sana" akasema Mathew.

"Where have you been Mathew?akajiuliza Dr Evans na ukimya ukatawala pale sebuleni.

"Mzee najua nyote mko katika mstuko mkubwa kwa kuniona.Nafahamu mnayo maswali mengi mngependa

kuniuliza,mngetaka kujua nilikuwa wapi muda huu wote lakini kitabu kile kilikwisha malizika kwa mimi kutoweka hivyo hakuna tena haja ya kuendelea kuulizana maswali kuhusiana na suala hilo.Kikubwa ambacho mnapaswa mkifahamu ni kwamba niko mzima na nimerejea nyumbani" akasema Mathew na kunyamaza kidogo halafu akasema

"Mzee umezungumza maneno fulani kwamba Mungu amenileta kwa wakati huu

ambao ni muafaka.Nakubaliana nawe mzee kwa sababu hata mimi sikutegemea kama ningekuwa hapa muda huu nikizungumza nanyi lakini kwa uweza wa Mungu niko tena katika ardhi ya nyumbani.Nimekuja nyumbani kumaliza kile ambacho kinaendelea hivi sasa" akasema Mathew na mstuko mkubwa ukaonekana katika nyuso za Dr Evans na Austin

"Huyu ni binadamu kweli au ni mzimu? Alikuwa wapi

huyu hadi akaibuka kwa wakati huu?akajiuliza Dr Evans

“Bado mpaka sasa inaniwia ugumu kuamini kama kweli huyu ndiye Yule Mathew halisi.Nina wasiwasi tusije kuwa tunachezewa na mzimu hapa” akawaza Austin.

“Naona nyuso zenu zimepatwa na mshangao lakini narudia tena kuwahakikishia kwamba nimekuja kumaliza hiki kinachoendelea hivi sasa hapa nchini.Nimekuja kuiokoa jumuiya ya Afrika Mashariki isisambaratike.Nimekuja

kummaliza James Kasi na kuung'oa mzizi wa ugaidi hapa Afrika mashariki" akasema Mathew

"Mathew unaniogopesha kwa maneno hayo unayoyatamka" akasema Dr Evans

"Usiogope mzee.Ulisema mwenyewe kwamba nimekuja kwa wakati muafaka.Ninaweza kusema kwamba Afrika Mashariki imeniita na siwezi kusema hapana.Mimi ni mtoto wa Afrika na Tanzania ambayo iko ndani ya Afrika Mashariki

inaponihitaji lazima niitike haraka sana.I’m back guys.I’m the same Mathew Mulumbi.Yawezekana mkaona nimebadilika kidogo lakini mimi ni Yule yule mliyenifahamu” akasema Mathew na kuwatazama akina Austin ambao wote bado walikuwa kimya wakimsikiliza.Dr Evans akasimama

“Come here my son.I need to hug you ! akasema Dr Evans na Mathew akainuka akamfuata Dr Evans wakakumbatiana

“Karibu tena nyumbani mwana Tanzania.Sasa moyo wangu una amani baada ya kukuona wewe na nimepata faraja kubwa kwa maneno yako kwamba umekujwa kuiokoa Afrika mashariki.Baada ya shambulio lile la kigaidi kutokea na kuuawa kwa wake za marais nilikesha nikitafakari dhumuni la shambulio lile na nikagundua kwamba ule ulikuwa ni mtego na viongozi wetu tayari wamenasa katika mtego huo kwa kuamsha hasira baada ya wake zao kuuawa na kutaka

kuanza kushambuliana wao kwa wao.Kila nchi kwa sasa inaweka majeshi yake katika utayari.Hakuna tena nchi inayomuamini mwenzake.Rwanda na Uganda zinashambuliana japo mapambano si makubwa lakini amani baina ya nchi hizo mbili haipo.Kitendo cha nchi mbili ndani ya jumuiya kurushiana risasi ni kiashiria kikubwa kwamba jumuiya hiyo inaelekea ukingoni.Uganda imewarejesha nyumbani mabalozi wake kutoka nchi za Rwanda na

Congo na kuwatimua mabalozi wa nchi hizo walioko Uganda.Nilimfuata Rais wetu Dr Fabian na kuzungumza naye nikamuonya kuhusiana na hatua za kijeshi mbazo wanataka kuzichukua dhidi ya Uganda.Wanaandaa kikosi cha jeshi ambacho kitakwenda Uganda kumsaka James Kasai.Uganda imekwisha onya kuhusu kitendo chochote cha kutuma kikosi cha jeshi katika ardhi yake kwamba ni kitendo cha kichokozi na imeapa kujibu kwa nguvu zote uchokozi

wowote utakaofanywa na nchi yoyote ya ndani au nje ya jumuiya ya Afrika mashariki.Nilijaribu kumueleza kuhusu hatari ya kusambaratika kwa jumuiya ya Afrika Mashariki lakini inaonekana Rais ameyapuuza mawazo yangu na kwa taarifa niliyoipata ni kwamba tayari wanajeshi kutoka katika nchi za Rwanda na Congo wamekwisha wasili nchini na maandalizi ya kikosi cha jeshi cha umoja kwa ajili ya kwenda Uganda yanaendelea.Viongozi wetu

wametanguliza hasira mbele bila kujali maslahi ya nchi zao na jumuiya.Wameungana pamoja na wanachokitaka ni kulipa kisasi kwa wake zao kuuawa” akasema Dr Evans

“Mzee ukilitazama jambo hili utakuta kati kati yake anasimama mtu anaitwa James Kasai.Yeye ndiye aliyesababisha haya yote yakatokea.Kama asingefanya shambulio nchini Tanzania kusingekuwa na hofu iliyoko hivi sasa ya nchi zetu kufikia hatua ya kutaka kushambuliana.Misheni yangu

ya kwanza ni kumuondoa James Kasai.Huyu jamaa kama akiondolewa hakuna nchi ambayo itaendelea na mpango wa kuishambulia nyingine.Tanzania,Rwanda na Congo wanajiandaa kufanya operesheni ya kijeshi nchini Uganda kumsaka James.Kama ulivyosema mzee wameingia mtegoni bila wao kujua kwani hawataweza kumpata James Kasai kwa kutumia nguvu za kijeshi hivyo James akiondolewa hakutakuwa tena na ulazima wa kutuma kikosi

hicho cha jeshi” akasema Mathew

“Jambo la pili ni kwamba James Kasai hayuko peke yake.Anashirikina na kikundi cha igaidi cha IS na kwa pamoja ndio waliotekeleza shambulio lile na kuua wake za marais na mabalozi.Baada ya kummaliza James Kasai itafuata operesheni nyingine ya kuung’oa kabisa mzizi wa IS hapa nchini na Afrika Mashariki.Hizi mbili si operesheni nyepesi nitahitaji sana msaada wenu” akasema Mathew.

“Sema chochote unachokihitaji Mathew.Mimi niko tayari kukusaidia”

“Nitahitaji kuonana na Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania .Mimi naye hatufahamiani.Ameingia madarakani wakati sipo hivyo nahitaji mtu wa kuniunganisha naye.Nataka nikamshauri aachane na operesheni za kijeshi anazotaka kuzifanya na mimi nitamuhakikishia kummaliza James Kasai” akasema Mathew

“Nitakuunganisha na Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania.Alikwenda Mbeya kwa ajili ya mazishi ya mke wake nitampigia simu baadae kujua kama amerejea Dar es salaam”

“Sawa mzee.Suala hili nililokueleza naomba iwe ni siri yako” akasema Mathew

“Usihofu Mathew siwezi kumueleza mtu bila ridhaa yako”

“Kwa sasa sina mawasiliano yoyote utawasiliana nami kwa kutumia simu ya Austin”

akasema Mathew wakaagana na Dr Evans wakaondoka.

“Austin kama nilivyowaeleza kwamba nimerudi hapa nchini kwa kusudi maalum.Nina misheni nzito ya kumuondoa James Kasai na ninakutaka uungane nami katika misheni hiyo” akasema Mathew

“Mathew unafahamu jibu lake.Katu siwezi kusema hapana.Tulikula kiapo cha kuilinda nchi dhidi ya adui wa ndani na wa nje kwa hiyo kila pale linapotokea jukumu la

kuilinda nchi siwezi kusema hapana” akasema Austin

“Ahsante sana Austin.Ningefurahi sana kama Gosu Gosu angekuwa mzima ajiunge nasi lakini kwa bahati mbaya haitawezekana.Ruby naye angekuwepo ni mtu muhimu sana.Misheni za sasa zinakwenda sambamba na teknolojia.Tutahitaji kuongeza watu wawili katika timu yetu badala ya Gosu Gosu na Ruby” akasema Mathew

“Wapo vijana wawili Tom Denzel na mwingine anaitwa

Aidan Kengele.Hawa ni vijana mahiri sana ambao wametoka mafunzoni hivi karibuni.Wana uwezo mkubwa sana”akasema Austin

“Utanipa mafaili yenye taarifa zao niyapitie” akasema Mathew na ukimya ukapita halafu Mathew akauliza

“Unazo taarifa zozote za mali zangu kuuzwa?

“Mali zako kuuzwa?Austin naye akashangaa

“Ndiyo.Una taarifa zozote?

“Hapana sina taarif zozote za mali zako kuuzwa.Nani kauza?Gosu Gosu?akauliza Austin

“Hapana si Gosu Gosu.Mke wangu Peniela” akasema Mathew

“Sina taarifa zozote za jambo hilo.Kwa nini kachukua maamuzi hayo? Mbona Gosu Gosu hajanieleza chochote? Tufuatilie tufahamu undani wa suala hili” akashauri Austin

“Usijali Austin.Kama kauza siwezi kumlaumu sana kwani

yeye kama wengine wote aliamini nimekwisha fariki dunia.Isitoshe sikuja kwa ajili ya hilo.Nimekuja kwa misheni maalum kabisa” akasema Mathew ukapita ukimya kidogo Austin akauliza

“Peniela hajakueleza chochote kuhusu jambo hilo?akauliza Austin

“Sina mawasiliano naye.Hafahamu kama niko hai” akasema Mathew

“Where were you Mathew? Akauliza Austin

“Austin let’s focus on our mission” akasema Mathew na kumuelekeza Austn waelekee katika hoteli aliyokuwa amefikia ili akachukue mizigo yake.

Mara tu baada ya akina Mathew kuondoka,Dr Evans akampigia simu Rais Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais” akasema Dr Evans baada ya Dr Fabian kupokea simu

“Mzee shikamoo”

“Marahaba Dr Fabian.Vipi maendeleo yako?

“Tayari nimekwisha rejea Dar es salaam.Nilishindwa kurejea jana.Nashukuru kila kitu kimekwenda vizuri na tumerejea salama”

“Dr Fabian najua mambo ni mengi sana lakini nakuomba nipate nafasi ya kuonana nawe jioni ya leo.Kuna jambo la muhimu sana nataka kuzungumza nawe” akasema Dr Fabian

“Mzee kwa siku ya leo utanisamehe sana.Ratiba yangu imebana sana.Mambo ni mengi .Kuna mengi ya kuzungumza

nawe mzee wangu naomba iwe kesho ili tupate nafasi ya kutosha kuzungumza.Samahani sana mzee” akasema Dr Fabian

“Usijali Dr Fabian.Hata kesho tunaweza kuonana” akasema Dr Evans wakaagana na Dr Evans akampigia simu Austin akamjulisha kuwa kikao kitakuwa siku ya kesho

****

Saa moja za jioni Ruby aliwasili katika makazi ya Rais ikulu Dar es salaama.Mlango wa gari lake ukafunguliwa na

mmoja wa walinzi aliokuwa ameongozana nao akashuka na kupokewa na msaidizi wa Rais akamkaribisha ndani akamtaka amsubiri Rais alikuwa anamalizia mazungumzo na watu waliokuja kumpa pole.Dakika arobaini baadae Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania Dr Fabian Kelelo akaingia sebuleni akiwa ameongozana na walinzi wake.Ruby akasimama kwa heshima

“Ruby ! akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais” akasema Ruby na Dr Fabian akampa mkono

“Karibu sana Ruby” akasema Dr Fabian na kuketi

“Samahani kwa kuchelewa.Nilikuwa na kikao na mabalozi waliokuja kunipa pole hivyo nikashindwa kuwaacha peke yao”

“Usijali mheshimiwa Rais” akasema Ruby

“Ruby nimefarijika sana kukuona hapa” akasema Dr Fabian na kumtaka Ruby

waelekee katika chumba cha chakula ambako kulikuwa kumeandaliwa chakula maalum.

“Ruby karibu sana.Nimeandaa hiki chakula kwa heshima yako” akasema Dr Fabian

“Ahsante sana mheshimiwa Rais” akasema Ruby na kila mmoja akajisaidia chakula alichohitaji

“She used to sit there” akasema Dr Fabian akimuonyesha Ruby kiti ambacho mke wake Millen

alipenda kukaa wakati wa chakula

“Pole sana mheshimiwa Rais”akasema Ruby

“Itanichukua muda mrefu kuizoea hali hii ya maisha bila Millen.She was everything to me” akasema Dr Fabian na kuweka kijiko mezani

“Mheshimiwa Rais hili ni jaribu kubwa ambalo unapitia hivyo itakulazimu kuwa jasiri sana kulikabili.Najua unaumia moyoni lakini jitahidi kuirejesha akili katika jukumu

kubwa la kuongoza watu zaidi ya milioni hamsini ambao wote wanakutazama wewe.Utalia siku utakapomaliza urais lakini kwa sasa bado una kazi kubwa ya kuongoza so focus ! akasema Ruby kwa sauti kavu.Dr Fabian akamtazama halafu akainua kijiko

“Ahsante Ruby.Katika wote waliokuja kunipa pole wewe ni wa kwanza kunieleza maneno kama hayo na uko sahihi ninatakiwa kuielekeza akili yangu katika masuala ya msingi

ya uongozi wa nchi” akasema Dr Evans

“Watoto wako wapi?akauliza Ruby

“Wamebaki Mbeya na ndugu wengine kuna ibada itafanyika kesho.Watarejea baada ya wiki moja.Tuliweke hilo pembeni.Pamoja na yote yaliyotokea Ruby nimefurahi sana kukuona.Ujio wako umenifarji sana” akasema Dr Evans na kuendelea kula walipomaliza wakaenda katika chumba cha mapumziko

“Ruby naomba nianze kwa kukueleza sababu iliyopelekea kukuita hapa nyumbani” akasema Dr Evans na kuanza kumuelezea Ruby kila kitu toka mauaji ya Lucy Muganza hadi walipogundua kwamba Tamar aliyekuwa mkurugenzi wa idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi kushirikiana na balozi wa umoja wa Ulaya aliyeuawa na watu wasiojulikana.

“Baada ya Tamar kuuawa ndipo Austin aliponifuata na kunieleza kwamba kuna mtu ambaye anafaa sana na

anaweza kuiongoza SNSA na akakupendekeza wewe.Sikuwa nikikufahamu na ilikuwa ni mara ya kwanza kusikia jina lako” akanyamaza kidogo

“Nilipoingia madarakani nilikumbana na changamoto moja ambayo ni kuamini watu wanaonizunguka.Nilipata somo kutoka kwa rais aliyenitangulia Dr Evans ambaye aliyekuwa waziri mkuu wa serikali yake alikuwa ni mfuasi wa mtandao wa kigaidi wa IS.Nilipata taabu kidogo kupata watu nitakaowaamini kwa ajili ya ile

misheni ya kumuua Lucy Muganza na ndipo Dr Evans akanitambulisha kwa Austin ambaye alinihakikishia ni mtu ninayeweza kumuamini.Toka wakati huo nimekuwa na imani kubwa kwa Austin ndiyo maana aliponieleza kwamba unafaa kuiongoza idara nyeti kama ya SNSA sikumuhoji mara mbili moja kwa moja nikamtaka anielekeze mahala ulipo.Nashukuru sana kwa kulikubali ombi langu na ukafanya kila jitihada kuhakikisha unafika Tanzania

kuifanya kazi hiyo niliyokuomba.Sina neno zuri zaidi la kukushukuru Ruby kwa hiki ulichokifanya”akasema Dr Evans

“Mheshimiwa Rais naamini Austin alikueleza historia yangu.Mimi ni mtanzania lakini kwa sasa nina uraia wa Uingereza.Kwa muda mrefu sikuwahi kurejea nyumbani na sikuwa na mpango huo hadi pale nilipokutana na mtu mmoja anaitwa Mathew Mulumbi ambaye ndiye aliyenifundisha kwamba

japokuwa nina uraia wa nchi nyingine lakini nina deni kubwa kwa nchi walikotoka wazazi wangu ambako ndiko asili yangu” akasema Ruby

“Mathew Mulumbi hili si jina geni katika masikio yangu.Who is he?akauliza Dr Fabian

“Mathew Mulumbi aliwahi kufanya kazi katika idara ya ujasusi.Anatajwa mmoja wa majasusi mahiri kabisa kuwahi kutokea hapa nchini.Ni yeye ndiye aliyenirejesha nyumbani Tanzania na kunishirikisha

katika misheni mbali mbali alizokuwa akizifanya.Misheni ya mwisho kushrikiana naye ni miaka mitatu iliyopita ambapo tulishirikiana kuwakomboa mateka waliokuwa wametekwa na kundi la kigaidi la IS” akasema Ruby

“Where is he now?

“Alifariki katika misheni hiyo.Alikwenda nchini Kenya katika misheni ya kuwakomboa mateka waliokuwa wanashikiliwa na kundi la IS na miongoni mwao alikuwemo mtoto wa Rais Dr

Evans.Walifanikiwa kuwakomboa mateka lakini Mathew hakurejea tena nyumbani.Alifia huko” akasema Ruby na kuinamisha kichwa

“Dr Evans hajawahi kunieleza chochote kuhusiana na suala hilo” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais,Mathew Mulumbi ndiye hasa aliyenifundisha kuipenda nchi nilikotoka na ndiyo maana uliponipigia simu kunitaka nije Tanzania kufanya kazi sikujiuliza maswali bali nilianza

mara moja mchakato wa kuondoka kule Uingereza kurejea huku.Haikuwa rahisi kama nilivyokueleza kwamba waliamini nimenunuliwa ili nikatoe siri zao na ndiyo maana wakapanga mpango ule wa kuniua.Kwa bahati nzuri nilijulishwa juu ya mpango ule na kuukwepa.Haikuwa safari rahisi hadi kufika hapa lakini nashukuru Mungu ameniongoza nimefika salama na niko tayari kwa kazi" akasema Ruby

"Kweli haya ni maongozi ya Mungu kwani hata mimi

sikutegemea kama ungeweza kufika Tanzania salama.Kama nilivyokueleza wakati ninakupigia simu kwamba kazi unayokuja kuifanya ni kuongoza idara nyeti ya usalama wa ndani wa nchi ambayo inafanya kazi zake kwa siri”

“Ninaifahamu idara hiyo na majukumu yake” akasema Ruby

“Nashukuru kama unaifahamu lakini idara hii ina umuhimu mkubwa sana kwa nchi tofauti na unavyoifahamu ndiyo maana ninahitaji mtu wa

kuiongoza ambaye atakuwa ni mzalendo wa kweli ambaye hataitumia idara hii kwa ajili ya manufaa yake kama walivyofanya waliotangulia” akanyamaza kidogo na kusema

“Kufuatia Tanzania kuchafuka kimataifa kutokana na kifo cha Lucy Muganza,Millen alinishauri tufanye kitu kwa ajili ya kuirejesha tena sifa ya Tanzania kama kisiwa cha amani na akashauri kuandaa mkutano mkubwa wa wake za marais wa dunia nzima kupitia taasisi

yake.Tulitumia gharama kubwa kuandaa mkutano huo muhimu na wiki moja kabla ya mkutano kufanyika balozi wa jamhuri ya kidemokrasia ya Congo hapa nchini alimfuata Millen akamueleza kwamba anataka kuwakutanisha wake za marais wa Rwanda na Congo na akamtaka Millen kumsaidia katika mpango huo.Millen alikubali kwa kujua kwamba ni jambo jema na maandalizi ya hafla ya kuwakutanisha wake hao za marais ikaandaliwa na siku ilipofika wakakutana kwa

ajili ya hafla hiyo na ndipo mabomu matatu yakalipuka.Mke wangu Millen,wake za marais wa Rwanda na Congo,mabalozi wanaoziwakilisha nchi hizo hapa Tanzania pamojana familia zao na raia wengine wa kutoka nchi hizo waliokuwa wamealikwa walipoteza maisha”

“Pole sana mheshimiwa Rais.Nilikuwa melini na sikujua chochote kilichotokea” akasema Ruby

“Ninafahamu ndiyo maana nilikwambia nitakuja kukueleza nitakaporejea” akanyamaza kidogo

“Baada ya shambulio kutokea alijitokeza mtu mmoja anaitwa James Kasai akadai kuhusika na lile shambulio akisaidiana na kikundi cha kigaidi cha IS”

“James Kasai.Who is he?akauliza Ruby

“Huyu anaongoza kikundi cha waasi ambacho kwa muda mrefu wamekuwa

wakipambana na serikali ya jamhuri ya kidemokrasia ya Congo lakini wa sasa baada ya kufurushwa nchini Congo inaaminika ameenda kuishi nchini Uganda”

“Katika maelezo aliyoyatoa alidai nini sababu ya kufanya shambulio hilo? Ruby akauliza

“Alidai ni kulipiza kisasi kwa Rais Patrice Eyenga” akasema Dr Fabian na kunyamaza akatazama na Ruby kwa muda halafu akasema

“Kwa hvi sasa Tanzania ikiungana na Rwanda na Congo tuko katika maandalizi ya kuandaa kikosi cha jeshi kitakachokwenda nchini Uganda kumsaka James Kasai na kuhakikisha anapatikana akiwa mzima au amekufa.Mazoezi ya kikosi hicho yanaendelea na pale watakapokuwa tayari wataelekea nchini Uganda kumsaka James Kasai” akasema Dr Evans na kunyamaza kwa sekunde chache

“Tunaamini balozi Germinus Mapupu hakuwa peke yake lazima kuna watu alioshirikiana nao katika kuandaa hafla ile.Nimewapa jukumu hilo SNSA la kuhakikisha wanachunguza na kujua nani waliokuwa wanashirikiana na balozi Mapupu lakini hadi sasa hakuna taarifa yoyote ya maana kutoka kwao.Umefika kwa wakati muafaka kabisa ninataka uanze na jambo hili.Ninataka uhakikishe tunafahamu nani walioshirikiana na balozi

Mapupu.Tunajua James Kasai ndiye aliyefanya shambulio lakini lazima wapo watu wa hapa nchini ambao walishirikina naye na hao ndio tunaotaka kuwafahamu.Jambo lingine ninataka kufanya mabadiliko makubwa katika idara ile na nitategemea sana ushauri wako.Utakapoanza kazi rasmi utaisoma ile idara na kutoa mapendekezo ni wapi panahitaji mabadiliko na mimi nitafanya bila kusita” akasema Dr Fabian

“Nimekuelewa mheshimiwa Rais na ninakuahidi utendaji uliotukuka” akasema Ruby

“Ahsante Ruby naamini utaweza kwani wenzako wamekusifia sana na kukupendekeza kuwa unafaa.Tafadhali naomba ukarejeshe heshima ya idara hii ambayo ina umuhimu mkubwa sana.Kwa kuwa umesafiri safari ndefu naamini bado una uchovu hivyo basi ninakupa wiki moja ya mapumziko ili kujiweka tayari kwa kazi.Wiki ijayo nitakutangaza rasmi kama

mkurugenzi mpya wa SNSA” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais.Mimi nimezoea kufanya kazi usiku na mchana hivyo hata sasa ukiniambia nikaanze kazi niko tayari” akasema Ruby na Dr Fabian akatabasamu kidogo

“Ninapenda sana watu kama wewe Ruby wenye ari ya kazi walio tayari kufanya kazi usiku na mchana kwa ajili ya nchi yao lakini ninakupa mapumziko hayo ya wiki moja ili kujiandaa kwa sababu kazi unayokwenda kuifanya si kazi

ndogo.Unakwenda kuongoza idara kubwa sana na nyeti kabisa.Nimekwisha toa maelekezo kwa wasaidizi wangu wakuandalie nyumba utakayoishi yenye hadhi yako,utapata pia walinzi wa kukulinda kila uendako na kuhakikisha unakuwa salama.Mambo hayo yote yatakapokamilika utafahamishwa” akasema Dr Evans

Waliendelea na mazungumzo na ilipofika saa nne za usiku Ruby akaondoka

kurejea katika makazi yake ya muda.

KAMPALA – UGANDA

Gari tatu ziliwasili katika nyumba alimofikia Melanie.Tayari ilikwisha timu saa mbili za usiku.Rais wa Uganda Jenerali Akiki Rwamirama akashuka na kuelekea ndani akiwa na walinzi wake.Moja kwa moja wakaelekea katika mlango wa chumba cha Melanie mmoja wa walinzi wake akagonga mlango na baada ya sekunde kadhaa mlango ukafunguliwa na

Melanie akiwa na tabasamu akajitokeza.Jenerali Akiki akawaelekeza walinzi wake wampe nafasi akaingia ndani na kuufunga mlango.Kabla hajaketi Melanie ambaye usiku huu alikuwa amevaa gauni jepesi lililoonyesha kila alichokivaa ndani akamkumbatia na kumbusu

“Karibu sana mheshimiwa Rais” akasema Melanie na Jenerali Akiki akatabasamu

“Nashukuru sana Melanie” akasema Jenerali Akiki na

kuketi sofani,Melanie akamkaribisha kinywaji

“Umeshindaje leo Melanie?

“Nimeshinda salama kabisa.Pole na mihangaiko ya siku nzima”akasema Melanie huku akimvua koti Jenerali Akiki akalitupa pembeni akachukua glasi ya pombe kali akamnywesha

“Melanie mapokezi yako si ya kawaida.Ni miaka mingi sijawahi kupokelewa namna hii” akasema Jenerali Akiki

“Mke wako hakupokei namna hii?Melanie akauliza

“Hapana.Mambo kama haya amekwisha yasahau kabisa.Yawezekana umri ukawa kigezo.Tumekwisha kuwa watu wazima sasa.Wanawake wana tatizo hilo wakifikia umri Fulani yale manjonjo yote waliyokuwa nayo mwanzo wa ndoa yanatoweka mnabaki mkiishi kwa mazoea”

“Usiseme wanawake.Wewe umechukua hatua gani kuboresha penzi lenu?.Mheshimiwa Rais

mapenzi hayana umri.Ili muyafurahie hata pale mtakapokuwa mmezeeka lazima kila mmoja aweke juhudi za kuyaboresha”akasema Melanie

“Ahsante kwa somo hilo Melanie nitalizingatia” akasema Jenerali Akiki na Melanie akamnywesha tena kinywaji kisha akaanza kufungua vifungo vya shati la Akiki akaanza kukichezea kifua chake.

“Mimi ni wako kwa usiku wa leo ninajiweka katika mikono yako” akasema Melanie

na kumbusu Jenerali Akiki ambaye tayari mashetani yake yalikwisha amka akashika hatamu.Maandalizi ya mechi yalifanyika kisha wakaingia uwanjani.

“Hili jamaa linatumia nguvu kana kwamba hii ni mara yake ya mwisho kufanya mapenzi.Hakuna raha yoyote ninayoipata hapa zaidi ya karaha.Ndiyo maaana ninampenda GosuGosu.Ni mwanaume wa aina yake.Ana nguvu lakini anajua kuzitumia na si kama huyu jamaa.Ngoja

nimuache ajiridhishe ninachotaka ni mambo yangu yafanikiwe.Ninaamini baada ya kuonja asali hataacha atataka tena na tena na hapo ndipo nitampeleka kama ng'ombe" akawaza Melanie wakati Jenerali Akiki akiendelea kujishughulisha kwa nguvu

Akiki alifika mshindo na kujitupa pembeni akihema kama amekimbia kilometa elfu moja.

"Keshamaliza hoi kabisa.Muone kwanza.Yale maguvu yote alikuwa

anakimbilia wapi? Akawaza Melanie na kumkumbatia Akiki

“Ahsante sana mheshimiwa Rais.Sikutegemea u mjuzi hivi wa haya mambo.Umenipeleka mbio..” akasema Melanie.

“Ahsante pia Melanie.Huu umekuwa ni usiku wangu wa kipekee kabisa” akasema Jenerali Akiki huku Melanie akiendelea kumchezea kifua kwa mkono wake.

“Melanie nina ombi moja kwako” akasema Jenerali Akiki

“Omba chochote mheshimiwa Rais.Unataka nini?

“Ninaomba tusiishie hapa.Nataka tuendelee.Nataka tuwe wapenzi kwa siri na mimi nitakufanyia kila kitu unachokitaka.Hata ukitaka nikununulie ndege uwezo ninao lakini tafadhali naomba tuendelee” akasema Jenerali Akiki .Melanie akatabasamu na kumbusu kisha akasema

“Una maneno matamu sana mheshimiwa Rais.Mimi sina tatizo na ombi lako ili mradi tu

unihakishie kwamba mkeo hatajua”

“Usihofu Melanie mke wangu hatatafahamu chochote.Itakuwa ni siri yetu kubwa” akasema Jenerali Akiki

“Kama unanihakikishia hivyo mimi sina kipingamizi chochote.Tuendelee na mahusiano ya siri”

“Ahsante Melanie.Nakuahidi kukupa kila unachohitaji.Nitakufanyia mambo hadi utashangaa mwenyewe” akasema Jenerali

Akiki huku Melanie akifanya juhudi za kuamsha mambo ikulu bila mafanikio

“Ikulu kumelala kabisa.Haamki tena” akawaza Melanie akainuka kitandani na kumimina pombe kali katika glasi na kumpa Jenerali Akiki wakakaa kitandani

“Leo nimekutana na James Kasai” akasema Melanie

“Umekutana naye wapi?

“Nilimpigi simu akafika hapa.Nilimueleza kuhusiana na

ule mpango wangu niliokueleza jana”

“Akasemaje ulipomueleza?

“Aliukubali ni mpango mzuri lakini akashauri hadi tukutane nawe kwanza tujadili kwa kina.Tafadhali kubali kukutana nasi pale atakapokupigia simu kukuomba”akasema Melanie

“Usijali Melanie kesho tutakutana sisi watatu kulijadili hili suala na tutalijadili lile suala lako.Kwa sasa ushirikiano na

wale majenerali wa jeshi hakuna tena”

“Nakushukuru sana mheshimiwa Rais kwa namna unavyonijali na kukubali kunisaidia katika mpango wangu huu” akasema Melanie

“Melanie nimekwisha kueleza kwamba niko tayari kukufanyia kitu chochote unachokitaka ili mradi kiwe ndani ya uwezo wangu.Nimekwambia hata ukitaka ndege nitakununulia” akasema Jenerali akiki ambaye tayari macho yake yalianza

kuwa mazito akionekana kuwa na usingizi

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Ilikuwa siku ndefu kwa Mathew Mulumbi.Saa tatu za usiku alikuwa chumbani kwake amekaa kitandani.

“Imekuwa siku ndefu nashukuru imekwenda vizuri na sasa ni wakati wa kuwasiliana na Habiba Jawad”akawaza na kuchukua kompyuta yake akajiunga na matandao wa intaneti kisha akampigia simu Habiba

“Habari yako Mathew Mulumbi” akasema Habiba Jawad

“Nzuri mama shikamoo”

“Marahaba habari za Dar es salaam?akauliza Habiba

“Dar es salaam kwema ninaendelea vizuri”

“Nafurahi kusikia hivyo”

“Vipi maendeleo ya Najma?

“Anaendelea vyema.Usimpigie simu sitaki ajue uko wapi” akasema Habiba

“Nitafanya hivyo mama”

“Vizuri.Tayari umekwisha anza kufanya maandalizi ya operesheni?

“Ndiyo mama nimekwisha anza maandalizi”

“Vizuri.Ukisha kuwa tayari unijulishe.Jitahidi ndani ya kipindi kifupi uwe umekamilisha maandalizi yote”

“Nadhani baada ya kesho kila kitu kitakuwa tayari”

“Ukishakuwa tayari nijulishe ili niweze kukupa taarifa za kuhusina na James

kasai’ akasema Habiba na kuagana na Mathew.

“Baada ya miaka mitatu hatimaye leo ninalala katika kitanda changu” akawaza Mathew wakati akijiandaa kulala.

****

Saa kumi na mbili za asubuhi ilimkuta Mathew Mulumbi akiwa hospitali ya Mtodora alikoenda kumtazama Gosu Gosu.Pale hospitali alikutana na Austin ambaye alilala pale pale na kumjulisha

kwamba hali ya Gosu Gosu bado haikuwa na mabadiliko yoyote.Mathew akaomba kuingia ndani ya chumba kile alimo Gosu Gosu akavishwa mavazi na kuingia akavuta kiti na kumsogelea

“Gosu Gosu najua unanisikia.It’s me Mathew Mulumbi again.I’m back and I need you.Please wake up.Fight and wake up.Please don’t force me to switch off this machine.If you want to live my brother please fight and wake up !You hear me?Please fight ! Don’t

quit ! akasema Mathew kisha akatoka mle ndani.Tayari Austin alikwisha muita mmoja wa vijana kutoka katika kikosi chake kukaa pale hospitali kuhakikisha Gosu Gosu anakuwa salama.Akamtambulisha kijana Yule kwa Mathew

“Austin we need to go.Saa tano leo tuna miadi ya kwenda kuonana na Rais.Tunatakiwa kujiandaa” akasema Mathew wakaelekea katika gari na kuondoka

“Umewasiliana na mchumba wa Gosu Gosu?Mathew akauliza wakiwa garini

“Bado simu yake haipatikani”

“Inanipa taabu kidogo.Ni mwanamke wa aina gani huyo ambaye anaweza akamuacha mchumba wake katika hali ile na kuondoka.Kweli ni mchumba wake? Mathew akauliza

“Kwa mujibu wa Lucy ni kwamba Gosu Gosu alikwenda Ufaransa na aliporejea ndipo alipoanza kuonekana na huyo

mwanamke.Lucy anadai kwamba mwanamke huyo amekuwa akienda karibu kila siku nyumbani kwa Gosu Gosu lakini hajawahi kulala pale.Wakimaliza mambo yao huondoka zake.Hata Lucy mwenyewe hana taarifa za kutosha kuhusiana na huyo mwanamke”akasema Austin

“Unasema Gosu Gosu alikwenda Ufaransa? Mathew akauliza

“Ndiyo.Kwa mujibu wa Lucy ni kwamba Gosu Gosu alisafiri ya kwenda Ufaransa na

aliporejea akaanza kuonekana na huyo mwanamke”

“Alikwenda kufanya nini Ufaransa?Mathew akauliza

“Hata mimi sifahamu.Hakuwahi kunieleza chochote kama anasafiri na hata suala la kuwa na mchumba alinificha pia.Nimeyafahamu haya yote baada ya kupigwa risasi.Mathew unahisi labda mwanamke huyo anaweza akahusika na tukio hili?akauliza Austin

“Siwezi kusema moja kwa moja kwamba anahusika but

something is not right about this woman.How she looks like?akauliza Mathew

“She’s pretty.Very pretty” akasema Austin

“Austin tunatakiwa kumtafuta huyo mwanamke.Nahitaji kumfanyia mahojiano” akasema Mathew

“Tutamuuliza zaidi Lucy kwani yeye ndiye anayemfahamu zaidi.Anaweza akatusaidia kufahamu mahala tunakoweza kumpata huyo mwanamke” akasema Austin na ukimya mfupi ukapita

“Gosu Gosu alipokwenda Ufaransa alifanikiwa kuonana na Peniela? Akauliza Mathew

“Natamani Gosu Gosu afumbue macho hata sasa.Kuna maswali mengi ambayo anatatakiwa kuyajibu” akasema Mathew

“Mathew I’m sorry to say this.Hudhani kama Peniela anapaswa kufahamu kwamba uko hai?akauliza Austin na Mathew akatafakari kwa sekunde chache halafu akasema

“Hapana.Hapaswi kufahamu chochote kuhusu

mimi.Tayari anafahamu kuwa nimekwisha kufa na itaendelea kubaki hivyo.Wamekwisha kubaliana na ukweli na sitaki kuvuruga maisha yao” akasema Mathew

“Vipi kuhusu watoto?

“Austin sitaki tuongelee suala hilo.Tuna mambo mengi ya kufanya tujielekeze huko kuliko kujadili kuhusu masuala yangu” akasema Mathew

“Sorry” akasema Austin na safari ikaendelea kimya kimya

“Mathew alikuwa wapi?Kwa nini hataki

kuongelea chochote kuhusiana na mahala alikokuwa?Ameibuka tu kutoka kusikojulikana na hataki kuzungumza chochote.Amekuja moja kwa moja akijielekeza katika misheni ya kutaka kumuua James Kasai.Amekuja akiwa anafahamu kila kitu kilichotokea hapa nchini.Amefahamuje mambo haya? Kurejea kwake kunaibua maswali mengi lakini hataki kuulizwa chochote" akawaza Austin.

Walikwenda kwanza nyumbani kwa Austin akajiandaa kisha wakaondoka hadi nyumbani kwa Mathew akajiandaa haraka haraka akajitazama

“Mwonekano huu unaruhusu kuingia ikulu” akawaza na kutoka chumbani kwake na kukutana na Lucy mtumishi wake

“Lucy naomba kwa dakika chache unieleze kuhusu mchumba wa Gosu Gosu” akasema Mathew

“Simfahamu vyema.Gosu Gosu hakuwa na mazoea ya kuleta mwanamke hapa nyumbani hadi hivi majuzi aliporejea kutokea Paris Ufaransa ndipo nilipoanza kumuona na huyo mwaname akamtambulisha kwangu kwamba anaitwa Melanie na amekuwa akija hapa mara kwa mara”

“Unaweza kufahamu mahala anakoishi?

“Hapana sifahamu hajawahi kunieleza”

“Kuna kingine chochote unachoweza kukikumhuka kuhusu huo mwanamke?

“Simfahamu kiundani na kila ajapo huwa wanajifungia chumbani kwa Gosu Gosu na hajawahi kulala hapa.Simfahamu vyema” akajibu Lucy

“Gosu Gosu alikwambia anakwenda Ufaransa kufanya nini?akauliza Mathew

“Aliniambia kwamba anakwenda katika mambo ya kibiashara.Hakunieleza zaidi” akasema Lucy

“Ahsante Lucy.Nitakuomba kitu kimoja.Ingia katika chumba cha Gosu Gosu jaribu kutafuta picha ya huyo mwanamke ninataka kumuona” akasema Mathew wakaingia garini na kuondoka kuelekea kwa Rais mstaafu Dr Evans.Wakati safari ikiendelea Mathew alikuwa akiyapitia mafaili mawili aliyopewa na Austin kuhusiana na wale watu wawili ambaoMathew alitaka waongezwe katika timu anayoiandaa kwa ajili ya operesheni ya kumuondoa

James KasaiAkayapitia kwa makini halafu akayafunika

“Si wabaya.Wameiva.Tunaweza kuwatuia” akasema

“Itakuwa ni misheni yao ya kwanza toka wametoka mafunzoni” akasema Austin na safari ikaendelea

“Mathew kuna kitu nataka ukifahamu” akasema Austin

“Kitu gani Austin?akauliza Mathew na Austin akameza mate kulainisha koo na kusema

“Watu wote waliamini kwamba umekufa except me

and Gosu Gosu.Hatukuamini hilo jambo na tuliwahi kujadiliana tufanye uchunguzi wetu kuufahamu ukweli ” akasema Austin na Mathew akatabasamu

“Kwa nini mliamini sijafariki dunia?

Mathew akauliza

“Binafsi kuna kitu ndani mwangu kilinifanya niamini hivyo.Hakuna hata usiku mmoja umewahi kupita bila kukukumbuka” akasema ustin

“Thank you so much.I appreciate that.You are true

brothers” akasema Mathew na safari ikaendelea hadi walipofika nyumbani kwa Rais mstaafu Dr Evans.Walinzi wakawafungulia geti wakaingia ndani na kupokewa na mlinzi wa Dr Evans.Siku hii Dr Evans alikuwa na walinzi watatu.Baada ya muda DrEvans akatokea na kusalimiana na akina Mathew

“Hatuna muda vijana tuanze safari”akasema Dr Evans wakaingia katika magari na kuondoka.

“Ulipozungumza na Rais kuomba kuonana naye ulimueleza jambo linalotupeleka huko?akauliza Mathew

“Hapana sikumueleza chochote” akajibu Dr Evans ambaye alionekana bado anamuogopa Mathew

“Taarifa nilizozipata asubuhi ya leo ambazo haijatangazwa ni kwamba usiku wa kuamkia leo ndege za Uganda zimeshambulia vijiji vilivyo karibu na mpaka wao na Rwanda na inasemekana watu

kadhaa wameuawa.Bado taarifa rasmi haijatolewa lakini hiyo ni taarifa ya kweli kabisa.Taratibu jumuiya ya Afrika Mashariki inamomonyoka.Kinachoniumiz a ni kwamba wakati wa uongozi wangu niliweka nguvu kubwa sana pamoja na marais wengine kuiimarisha jumuiya hii.Zipo faida nyingi za jumuiya hii ambayo kwa sasa imefikia hatua nzuri na kubwa ya kuwa na sarafu moja kwa hiyo haya yanayoendelea hivi sasa yananisonnesha mno" akasema Dr Evans

“Usihofu mzee.Jumuiya haitaweza kusambaratika wakati vijana wa kusimama kuitetea tupo.Ninakuahidi tutasimama imara kuhakikisha kwamba jumuiya inaendelea kuwepo na kustawi.Wale wote waliopandikiza chuki na kuleta chokochoko baina ya wanachama ili wapigane wanakwenda kushindwa vibaya.Si muda mrefu wale makuwadi wa mabepari watakwenda kukiona cha mtema kuni.Siku zao

zinahesabika” akasema Mathew na Dr Evans akatabasamu

“Mathew hujabadilika.Bado ni Mathew yuleyule mwenye maneno mazito ya kizalendo.Nilifanya kos……” akasema Dr Evans na Mathew akamkatisha

“Mzee tumekwisha toka huko.Kitabu kile tumekwisha kifunga na kama kuna makosa yalifanyika yote tumeyafukia sasa tunajielekeza katika mambo mengine ya msingi.By the way how’s your daughter?.akauliza Mathew

“She’s fine.Kwa sasa anaishi nchini Afrika kusini amepata kazi huko.Huwa ninakwenda kumtembelea mara kwa mara na haachi kukushukuru kwa ushujaa uliouonyesha siku ulipowakomboa” akasema Dr Evans Mathew na safari ikaendelea

Waliwasili ikulu na kupokewa na msaidizi wa Rais wakakaribishwa ndani ambako wakamkuta Dr Fabian akiwasubiri.

“Mzee karibu sana” akasema Dr Fabian akipeana mkono na Dr Evans

“Ahsante sana mheshimiwa Rais”

“Nilidhani uko peke yako kumbe umekuja na ugeni” akasema Dr Fabian huku akisalimiana na Austin

“Austin.Sikujua kama unakuja na mzee.Vipi hali ya Gosu Gosu? Sikuweza kukupigia kujua hali yake kutokana na kutingwa sana na mambo mengi ya mazishi ya mke wangu.Utanisamehe usije

ukaona kama nimewatupa vijana wangu” akasema Dr Fabian

“Usijali mheshimiwa Rais tunaelewa kipindi unachokipitia na sisi tuko pamoja nawe” akasema Austin

“Anaendeleaje mwenzako?akauliza Rais

“Hali yake bado iko vile vile hakuna mabadiliko”

“Poleni sana.Nimekwisha wasiliana na uongozi wa hospitali kufanya kila lililo ndani ya uwezo wao kuokoa maisha yake na mimi nikipata

wasaa nitakwenda kumtembelea vile vile nimemuagiza mkuu wa jeshi la polisi kuhakikisha jeshi la polisi linawapata watu waliofanya kitendo hicho” akasema Dr Evans

“Tunashukuru sana mheshimiwa Rais’ akasema Austin na kukaa Dr Evans akajikuta akitazamana na Mathew

“Karibu sana ndugu” akampa mkono.Hakuwa akimfahamu

“Anaitwa Mathew Mulumbi.Aliwahi kufanya kazi katika idara yetu ya ujasusi” Dr Evans akamtambulisha Mathew kwa Rais ambaye alishindwa kuzuia mstuko usionekane katika uso wake

“Mathew Mulumbi?!! Akauliza kwa mshangao

“Ndiyo mheshimiwa Rais.Ninaitwa Mathew Mulumbi” akasema Mathew na bado Dr Fabian akaendelea kumtazama kwa woga

“Mathew Mulumbi yupi? Kwa taarifa nilizonazo ni

kwamba Mathew Mulumbi amefariki dunia.Ni jana tu nilikuwa na Ruby hapa tukizungumza akanieleza kwamba ni Mathew Mulumbi ambaye alimfundisha kupenda nchi alikotoka na akasikitika kwamba huyo Mathew amefariki dunia lakini leo ninaletewa Mathew Mulumbi mbele yangu.Dr Evans what is this?akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais umesema ulikuwa na Ruby?akauliza Mathew

“Ndiyo nilikuwa naye jana na tulizungumza kuhusu marehemu Mathew Mulumbi”

“Oh my God ! Ruby is here?akauliza Mathew kwa furaha Dr Fabian akabaki anashangaa

“Dr Evans what’s going on?akauliza DrFabian

“Mheshimiwa Rais utanisamehe kwa mkanganyiko huu uliotokea.Tunaweza kuzungumza faragha kidogo?akauliza Dr Evans

“Excuse us guys” akasema Dr Fabian akatoka mle sebuleni na Dr Evans

“Ahsante Mungu.Ruby amekuja nchini ! akasema Mathew kwa furaha

“Austin ahsante sana kwa kumshauri Rais amuite Ruby nyumbani.Ulifanya jambo kubwa na zuri sana.I can’t wait to see her ! akasema Mathew na kumpa Mathew mkono wa pongezi

“Haya ni maajabu.Nyote wawili watu muhimu mmefika

kwa wakati mmoja” akasema Austin

“Hii ni mipango ya Mungu.Ni yeye ambaye ametaka iwe hivi ilivyo.Sasa unaweza ukaamini kwamba kwa namna yoyote ile Afrika Mashariki haitaweza kusambaratika” akasema Mathew

Dr Fabian na Dr Evans waliingia katika chumba Fulani ambacho hakikuwa na mtu ndani.

“Dr Evans nini hiki kinaendelea?I real don’t understand.Mathew Mulumbi

ambaye nilielezwa na Ruby kwamba alifariki dunia ni huyu uliyeongozana naye hapa au kuna mwingine?akauliza Dr Fabian

“Dr Fabian kuna Mathew Mulumbi mmoja tu ambaye ni huyu niliyeogozana naye” akasema Dr Evans

“Haya ni maajabu.Niliambiwa amefariki sasa ametokea wapi tena?Ni yeye kweli au ni mzimu ule? Akauliza DrFabian

“Ni yeye mwenyewe Mathew Mulumbi” akasema Dr

Evans.Ukapita ukimya mfupi Dr Fabian akauliza

“Kwa nini ikadaiwa amefariki dunia?

“Kuna hadithi ndefu hapa nitakueleza lakini ukweli ni kwamba Mathew hakufariki dunia kama tulivyodhani.Mathew ni mzima”

“Alikuwa wapi?

“Hajasema chochote kuhusu mahala alikokuwa.Ameibuka tu toka kusikojulikana.Dr Fabian mimi nawe tutakuwa na mazungumzo marefu kidogo

baadae na nitakueleza kila kitu lakini nakuomba nimekuja na hawa vijana tuna mazungumzo nawe” akasema Dr Evans na Dr Fabiana akaonekana kusita

“Tafadhali Dr Fabian tunahitaji kuzungumza na hawa vijana”

“Kuna nini? Akauliza Dr Fabian

“Kuna jambo kubwa la kujadili.Tafadhali sana” akasema Dr Evans

“Mzee naomba liwe ni jambo lenye maslahi kwa

sababu dalili ninazoziona si njema”

“Niamini mimi Dr Fabian” akasema Dr Evans kisha wakatoka na kurejea mahala walikowaacha Mathew na Austin

“Samahani tuliwakimbia kidogo.Tulikuwa na mazungumzo ya faragha.Karibuni sana vijana.Mathew Mulumbi karibu sana.Ni furaha yangu kukutana nawe leo” akasema Dr Fabian.

“Hata mimi nafurahi kukutana nawe mheshimiwa Rais” akasema Mathew

“Mzee wangu hapa anasema kwamba kuna mazungumzo muhimu.Naomba tuelekee katika chumba cha maongezi” akasema Dr Fabian na kuwaongoza akina Mathew kuelekea katika chumba cha mazungumzo ya faragha

“Karibuni sana vijana wangu.Mtanisamehe kwa mkanganyiko uliotokea awali” akaanzisha maongezi Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais nimekuja na hawa vijana wangu kwa ajili ya mazungumzo muhimu yanayohusiana na kile kilichotokea na kinachoendelea hivi sasa katika nchi yetu na Afrika Mashariki kwa ujumla.Nisiwe mzungumzaji mkubwa naomba nimpe nafasi Mathew Mulumbi aendelee” akasema Dr Evans

“Karibu Mathew” akasema Dr Fabian na bila kupoteza muda Mathew akasema

“Mheshimiwa Rais,kama rais mstaafu Dr Evans

alivyokwisha nitambulisha kwako naitwa Mathew Mulumbi,niliwahi kufanya kazi katika idara ya ujasusi Tanzania kabla ya kuanza kujishughulisha na biashara lakini hata wakati ninafanya biashara zangu bado niliendelea kushiriki katika misheni mbali mbali kubwa zenye maslahi mapana kwa nchi yetu”akanyamaza kidogo

“Sitaki kuongelea tukio la mimi kupotea na kujulikana nimefariki dunia na nisingependa kuulizwa

nilikuwa wapi.Ninaomba nijielekeze moja kwa moja katika suala la msingi lililotuleta hapa” akanyamaza tena kidogo

“Japokuwa sikuwepo hapa nchini lakini ninafahamu kile kilichotokea na kinachoendelea na baada ya kufika hapa nchini nikapata tena taarifa nyingine ambazo sikuwa nikizifahamu kuhusiana na hiki kinachoendelea hivi sasa.Ambacho sikuwa ninakifahamu ni mauaji ya Lucy Muganza na mumewe” akasema

Mathew na kunyamaza huku wote mle ndani wakimsikiliza kwa makini sana

“Mheshimiwa Rais kinachoendelea hivi sasa ni mpango mkubwa wa nchi kubwa tajiri kuisambaratisha jumuiya ya Afrika Mashariki nadhani unalifahamu hilo ndiyo maana Lucy Muganza akauwa” akasema Mathew na Dr Fabian akatikisa kichwa kukubaliana naye.

“Baada ya kifo cha Lucy Muganza mambo hayakuishia pale.Mpango ule bado

uliendelea na hiki kinachoendelea hivi sasa ni muendelezo wa kile alichotakiwa kukifanya Lucy Muganza lakini akawahi kuuawa.Mataifa walioandaa mpango huu wanailenga zaidi jamhuri ya kidemokrasia ya Congo lakini hawawezi kuingia nchini Congo bila kuiondoa kwanza nchi hiyo katika jumuiya ya Afrika Mashariki na ili kuiondoa nchi ya Congo katika jumuiya ya Afrika mashariki lazima kwanza kuisambaratisha jumuiya hiyo

na kile kilichotokea juzi hapa nchini ni mkakati wa mabeberu kuisambaratisha jumuiya ya Afrika Mashariki na kutengeneza njia kuelekea Congo.Tayari mpango wao huo umeanza kuonyesha matunda kwani umetokea mvurugano mubwa baina ya nchi wanachama na kuna kila dalili kwamba uhai wa jumuiya hii uko mashakani" akanyamaza kidogo na kumtazama Dr Fabian aliyekuwa ameweka mkono shavuni akisikiliza kwa makini sana

“Wametumia akili kubwa kumtumia James Kasai kutekeleza shambulio lile na kuamsha hasira kali na sasa kila nchi inataka kuishambulia Uganda kwa kigezo cha kumsaka au kulipiza kisasi kwa James Kasai.Utaniwia radhi mheshimiwa Rais lakini sina lugha nyingine ninayoweza kuitumia kulisema hili lakini mlikurupuka sana kuanza kuchukua hatua za kijeshi.Hamkutakiwa kuishambulia au kupanga mipango ya kuingia Uganda

kijeshi kwa ajili ya kumsaka James Kasai.Wewe mheshimiwa Rais ukiwa kama mwenyekiti wa jumuiya ya Afrika mashariki ulitakiwa kuwa mstahimilivu na kutafuta njia muafaka ya kulimaliza hili suala lakini ulikuwa mstari wa mbele kuwaunganisha Rwanda na Congo kuunda kikosi cha jeshi kwenda nchini Uganda.Naweza kusema kwamba kuna mkono wako katika mvurugano huu unaoendelea hivi sasa katika eneo la Afrika Mashariki" akasema Mathew na

kunyamaza baada ya sura ya Dr Fabian kubadilika

“Dr Evans nini hasa kimekuleta hapa? Umewaleta vijana hawa waje waanze kunifundisha uongozi? Akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais nadhani ungeendelea kumsikiliza Mathew Mulumbi bado hajamaliza kile anachotaka kukueleza” akasema Dr Evans

“Huu ni upotevu mkubwa wa muda wangu ..” akasema Dr Fabian huku akitaka kunyanyuka

“Sir,we’re not wasting any of your time” akasema Mathew

“Yes you are. Nimekaa nanyi hapa kwa heshima ya huyu mzee wangu lakini kumbe mambo mnayokuja kunieleza ni upuuzi mtupu”

“Si upuuzi mheshimiwa Rais” akajibu Mathew naye akasimama

“Mathew please sit down” akasema Dr Evans

“Ndiyo ni upuuzi mtupu.Unadiriki kunifundisha mimi namna ya kuongoza nchi?! Who are you?Unadiriki

kumtetea gaidi muuaji ambaye ameua watu kikatili kabisa.Wewe ni nani kuhoji maamuzi yangu?Mimi ni rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania ninayeogoza watu zaidi ya milioni hamsini ambao natakiwa kuhakikisha usalama wao wewe ni nani wa kuhoji hatua ninazozichukua? Akafoka Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais nafahamu umeumizwa na kifo cha mke wako na hata sisi sote tumeumizwa pia likini hatua zile ulizozichukua wewe na

wenzako wa Rwanda na Congo kukabiliana na suala hili si hatua sahihi.Narudia kusema tena na utanisamehe kwamba mlikurupuka ! akasema Mathew na Dr Fabian akamtazama kwa hasira

“Dr Evans ninakuheshimu sana mzee wangu na nilitegemea una kitu kikubwa unakuja kunieleza lakini kumbe umeniletea huyu mgonjwa wa akili.Narudia tena kukuuliza Mathew Mulumbi wewe ni nani wa kuhoji maamuzi ya Rais? Unadhani katika watu milioni

hamsini ninaowaongoza wewe pekee ndiye mwenye akili kubwa kuliko wote? Akauliza Dr Fabian akiwa amewaka hasira

“Dr Evans nashukuru kwa kuja kunitembelea.Tumemaliza kuna mambo mengine natakiwa kuyafanya” akasema Dr Fabian na kugeuka kuanza kuelekea mlangoni

“Mr President we’re not finished yet. You have to listen to me ! akasema Mathew

“Siongei na wagonjwa wa akili mimi ! akafoka Dr Fabian

akipiga hatua kuelekea mlangoni

“You’re not going to find James Kasai ! akasema Mathew na Dr Evans akageuka

“What ?akauliza

“Umenisikia vizuri mheshimiwa Rais.Hamtaweza kumpata James Kasai ! Mathew akasisitiza na Dr Fabian akatoa kicheko kidogo

“Dr Evans hiki kituko gani umeniletea mzee wangu? Akauliza Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais naomba umsikilize Mathew kile

anachotaka kukueleza.Ana kitu cha muhimu sana” akasema Dr Evans

“Dr Evans nakushangaa sana.Unamuaminije huyu mtu? Ameibuka kutoka kusikojulikana na halafu unamuamini? Ni vipi kama…oh my God ! akasema Dr Fabian

“Mr president I know Mathew Mulumbi and I trust him.Nisingeweza kuja naye hapa kama hana kitu cha maana cha kukueleza ! akasema Dr Evans

“Please Mr president ! akasema Dr Evans

“Kwa heshima ya huyu mzee ambaye ninamuheshimu sana nakupa dakika tatu unieleze hicho unachotaka kukisema lakini ukiendelea na upuuzi wako wa kuhoji maamuzi yangu kikao hiki kitakuwa kimefika mwisho” akasema Dr Fabian

“Thank you Mr President” akasema Mathew

“Samahani kwa maneno niliyoyatumia awali yawezekana yalikuwa makali

lakini ninaendelea kusisitiza kile nilichokisema kwamba hatua za kijeshi dhidi ya Uganda kwa kigezo cha kumsaka James Kasai hazitakuwa na manufaa yoyote badala yake zitakuwa ni kama kuongeza mafuta katika moto”

“Mathew unaniudhi mno kwa kauli hiyo ya kwamba maamuzi yetu ya kutumia nguvu za kijeshi hayakuwa maamuzi sahihi.Hatukuwa wajinga tuliofanya maamuzi haya ya kuunda kikosi cha pamoja kwenda Uganda

kumsaka James Kasai !
akasema kwa ukali Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais ninasema kwamba hayakuwa maamuzi sahihi kwa sababu hamtaweza kumpata James Kasai kwa nguvu za kijeshi”

“Kwa nini tusimpate? Wewe unafahamu sana kuliko sisi?Mimi ni Rais wa nchi na nina kila taarifa za kila kinachoendelea hapa nchini hivyo hatukukurupuka narudia tena kusema kwamba iwe mvua iwe jua lazima James Kasai apatikane ! akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais ni kweli una kila taarifa ya kila kinachoendelea hapa nchini lakini kwa bahati mbaya wewe na wenzako hamna taarifa sahihi kuhusiana na James Kasai ndiyo maana mkachukua maamuzi yale lakini kama mngekuwa na taarifa sahihi msingeandaa kikosi kwenda Uganda kumsaka”

“Wewe unazo hizo taarifa za James”

“Hicho ndicho hasa kilichonirejesha nyumbani” akasema Mathew na

kunyamaza kidogo halafu akasema

“Nimekuja kwa lengo moja tu kummaliza James Kasai na kuiokoa jumuiya yaAfrika mashariki katika hatari ya kusambaratika” akasema Mathew na Dr Fabian akatoa kicheko

“Wewe ! akasema Dr Fabian kwa mshangao

“Unataka kumuondoa James Kasai? Unajua unachokizungumza Mathew Mulumbi? Akauliza Dr Fabian na kumgeukia Dr Evans

“Dr Evans nilikwambia umeniletea mgonjwa wa akili.Hajui anachokizungumza ni kitu gani”

“Dr Fabian ninakuheshimu sana na ninakuomba uniheshimu pia.Huyu anayezungumza si mgonjwa wa akili na anajua anachokisema” akasema Dr Evans

“Mheshimiwa Rais ninamaanisha kile ninachokisema kwamba nimekuja kummaliza James Kasai na kuinusuru jumuiya ya Afrika Mashariki.Ningeweza

kumuondoa James kima kimya bila kukueleza chochote kwani ninazo taarifa zote za kuhusiana naye lakini nimekuja kwako kukueleza kuhusiana na kile ninachotaka kukifanya na kukuomba usitishe operesheni zote za kijeshi mlizopanga kuchukua kuhusu kumsaka James Kasai na vile vile uwashauri wenzako wa Rwanda na Congo waondoe majeshi yao katika mipaka ya nchi zao na Uganda" akasema Mathew na Dr Fabian akazama mawazoni kisha akauliza

“Taarifa gani unazo kuhusu James Kasai ambazo unadhani sisi hatuna?

“Mnachofahamu ni kwamba James Kasai amejificha katika misitu ya Kaskazini mwa Uganda.Siyo Sahihi.James Kasai hayuko huko”

“Kama hayuko huko msituni yuko wapi?akauliza Dr Fabian

“Siwezi kusema kwa sasa yuko wapi lakini hayuko msituni na mkipeleka kikosi msituni utakuwa ni upotevu wa muda na uchokozi kwa Uganda”

“Kama hujui mahala alipo James Kasai unataka kumuondoa vipi? Dr Evans huyu mtu anacheza na akili zetu.Anasema anao uwezo wa kumuondoa James Kasai lakini hajui mahala alipo”

“Hata kama ningekwambia usingeniamini.Umetanguliza hasira mbele unataka kulipiza kisasi kwa kifo cha mkeo bila kuzingati maslahi mapana ya nchi na jumuiya ya Afrika mashariki.James Kasai amezidi kujitanua na kwa sasa amejiunga na kundi la kigaidi la

IS ambao wanamfadhili kwa fedha na vifaa vya kijeshi na ana nguvu kubwa hivyo mnapofikiria kupambana na James Kasai mfikirie pia kuhusu kupambana na kundi la kigaidi la IS.Mheshimiwa Rais tafadhali nakuomba uniamini hiki ninachokwambia kwamba ninao uwezo wa kumuondoa James Kasai na vile vile kuuondoa mzizi wa kundi la IS ambalo kwa miaka ya karibu limeendelea kujiimarisha katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na kati.Mimi si

mwanasiasa na sina maneno matamu ya kukushawishi lakini nilichokueleza hapa ni ukweli mtupu.Ni juu yako kufanya maamuzi aidha kufuata yale niliyokushauri au kuendelea kuibomoa jumuiya ya Afrika mashariki kwa kuendelea na mipango ya kijeshi dhidi ya Uganda” akasema Mathew.Dr Evans akakohoa kidogo na kusema

“Mheshimiwa Rais kijana ameweka wazi kila kitu.Ninamfahamu Mathew Mulumbi na ninasimama

upande wake.Alichokueleza ni sahihi na maamuzi yote ni juu yako.Mimi kwa ushauri wangu badala ya kuendelea kumpinga na kumuona kama mgonjwa wa akili ungekubali kushirikiana naye kwani anahitaji sana kuungwa mkono kwa kitendo hiki cha kizalendo anachotaka kukifanya.Imekuwa ni kawaida ya Mathew kuyaweka hatarini maisha yake kwa maslahi ya taifa lake hivyo ni mtu anayehitaji kupongezwa na si kubezwa.Lakini kama bado unamuona ni mwendawazimu

basi endelea na mipango yako ya kijeshi na wenzako na utauona mwisho wake.Mimi na vijana wangu tunaondoka lakini pale maji yatakapofika shingoni usijaribu kunitafuta au kuwatafuta vijana hawa” akasema Dr Evans na kusimama

“Mheshimiwa Rais kabla hatujaondoka nataka kuuliza swali.Nani alitoa wazo la kuundwa kwa kikosi cha umoja kwenda kuivamia Uganda kumsaka James Kasai?akauliza Mathew Dr Fabian akabaki kimya

“Lilikuwa ni wazo lako mheshimiwa Rais? Dr Evans naye akauliza

“Lilikuwa ni wazo la pamoja”

“Nani aliyelileta mezani?akauliza Mathew na Dr Fabian akabaki kimya

“Ukimya huo unaonyesha kwamba si wewe uliyebuni wazo hilo la kuundwa kwa kikosi cha jeshi cha pamoja kwa ajili ya kwenda Uganda kumsaka James Kasai.Wazo hilo lilitoka aidha kwa Rais wa Rwanda au Congo.Mheshimiwa

Rais utanisamehe kwa mara nyingine tena kwa lugha ninayotumia lakini labda nizungumze kwa kiingereza they’re using you.Rwanda na Congo kila moja kwa muda mrefu imekuwa na mahusiano yasiyo mazuri na nchi ya Uganda na wanataka kutumia nafasi hii kuiadhibu Uganda.Wote wamejificha ndani ya koti lako la inaonekana kwamba ni Tanzania ndiyo inayoongoza kikosi hicho kinachoandaliwa kwenda Uganda.Mheshimiwa Rais tunao

uwezo wa kumuondoa James Kasai kimya kimya bila hata kutumia nguvu za kijeshi na kuinusuru jumuiya hii ya Afrika Mashariki kusambaratikia katika mikono yako.Kama ni kulipiza kisasi kwa kile alichokifanya James kumuua mke wako nakuahidi ninaweza kumleta akiwa hai na wewe ukamfanya kile utakacho ili kumaliza hasira yako” akasema Mathew na Dr Fabian akainamisha kichwa kafikiri kwa muda na kusema

“Mathew una hakika unao uwezo wa kumuondoa James Kasai? Akauliza Dr Fabian

“Ndiyo mheshimiwa Rais.Ninao uwezo wa kumuondoa James Kasai na ndicho ambacho nimekuja kukifanya na nitaendelea na mipango yangu hiyo hata kama hautakubaliana nami kwa sababu kwa mipango yenu hamtaweza kumuondoa James Kasai na ataendelea kuwa mtu hatari kwa eneo hili la Afrika mashariki ” akasema Mathew

“What do you need?akauliza Dr Fabian na Dr Evans akaonyesha tabasamu usoni

“Kitu cha kwanza ninachokihitaji ni kuwasiliana na marais wenzako wa Rwanda na jamhuri ya kidemokrasia ya Congo na kuwataka waondoe vikosi vyao vya jeshi katika mipaka ya nchi zao na Uganda.Tunataka kwanza kuondoa hatari ya kutokea machafuko makubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na hilo litawezekana pale ambapo

vikosi vya jeshi vitaondolewa mipakani na wewe kama mwenyekiti wa jumuiya ya Afrika Mashariki ndiye mwenye uwezo wa kulifanya hilo na si mimi wala Dr Evans” akasema Mathew na Dr Fabian akaguna

“Mathew suala hilo si rahisi kama unavyodhani.Mataifa haya mawili wote wamekwisha athirika na James Kasai.Amefanya ukatili mkubwa Congo na hata Rwanda pia na kwa muda refu nchi hizi mbili zimekuwa zikiishinikiza Uganda kumfukuza James katika misitu

ya nchi hiyo lakini Uganda imekuwa ikipuuza na kwa sasa wameamua kuchukua hatua.Nafahamu kama ulivyoeleza kuwa nchi hizi zimekuwa na migogoro yao ya muda mrefu lakini kwa sasa wote wamepata chanzo cha kutaka kuishambulia Uganda.Wazo la kuundwa kwa kikosi cha pamoja halikuwa langu bali la Rais wa Rwanda.Kwa upande Fulani ninaanza kukubaliana nawe Mathew kwamba yawezekana tuliharakisha sana kufanya

maamuzi yale ya kutumia nguvu za kijeshi kutafuta James Kasai na sasa inaniwia ugumu namna ya kuanza kuwashawishi hawa wenzangu kutokutumia nguzu za kijeshi.Lazima watajitenga nami na kujiunga wao wenyewe wakaendelea na operesheni zao.Kitu cha msingi ambacho kinaweza kunipa hata mimi nguvu ya kuwataka waondoe majeshi yao mpakani ni kama tukifanikiwa kumuua James Kasai .Hawatakuwa tena na sababu nyingine ya kuendelea na mapambano na Uganda

hivyo Mathew Mulumbi kama kweli unataka kusaidia katika jambo hili muue James Kasai na mambo yote yatakuwa yametulia”

“Ahsante mheshimiwa Rais kwa kuanza kunielewa.Narudia kukuhakikishia tena kwamba uwezo wa kumuua James Kasai ninao na nitamuondoa lakini naomba japo kwa kipindi hiki ambacho nitakuwa nikilishughulikia suala hilo operesheni zozote za kijeshi zisifanyike nchini Uganda ili kutokuharibu mambo”

“Ninakupa siku saba Mathew uwe umempata James Kasai na kama ukishindwa ndani ya siku hizo saba basi kikosi cha umoja kitaendelea na kazi yake bila kujali athari zitakazojitokeza kwani hatuwezi kuendelea kumuacha huyu mtu mmoja aendelee kuua watu hovyo wakati uwezo wa kumuondoa tunao.Ninakuruhusu ukafanye operesheni yako ndani ya siku saba uwe tayari umempata James”

“Ahsante mheshimiw Rais.Nakuahidi kabla ya siku hizo saba hazijamalizika nitakuwa nimempata James Kasai”

“Kitu gani unahitaji nikusaidie?akauliza Dr Fabian

“Kitu cha kwanza ninachokihitaji ni kuunda timu ambayo tutaifanya hiyo operesheni.Tayari ninaye Austin.Nilimtegemea Gosu Gosu lakini kwa bahati mbaya amepigwa risasi lakini tayari tumekwisha pata vijana wengine wawili ambao

tutasaidiana nao vile vile ninamuhitaji Ruby”

“Ruby? Akauliza Dr Fabian

“Ndiyo.Ninamuhitaji sana Ruby katika operesheni hii”

“Ruby nimemuita hapa nchini kwa ajili ya kazi nyingine kabisa.Operesheni hiyo ni hatari na siwezi kuruhusu akajiunga na timu hiyo na kuhatarisha maisha yake” akasema Dr Fabian

“Ninamuhitaji Ruby pamoja na idara anayokuja kuiongoza” akasema Mathew

“SNSA? Unaifahamu idara hiyo?akauliza Dr Fabian

“Ndiyo ninaifahamu vyema” akasema Mathew

“Ruby bado sijamkabidhi rasmi nafasi ya ukurugenzi wa SNSA na nimempa nafasi ya kupumzika kwa wiki moja kabla ya kuanza kazi rasmi” akasema Dr Fabian

“Mheshimiwa Rais hii ni vita na hakuna muda wa kupumzika.Ruby anatakiwa aanze kazi mara moja.Tunaihitaji ile idara ikiwa chini yake.Nakuomba

ikiwezekana hata kesho ukamkabdhi ofisi.Ruby ni mchapkazi hachoki hata ukimuita hapa sasa hivi na kumkabidhi ofisi ataanza kazi hivyo hakuna haja ya kumpa mapumziko ya wiki nzima”akasema Mathew

“Mathew unanilazimisha kufanya jambo ambalo sikuwa nimelikusudia.Ruby amepitia mambo mazito hadi kufika hapa ndiyo maana nimempa muda wa kupumzisha akili yake”

“Mheshimiwa Rais najua unalo tatizo la kuamini watu

lakini nakuomba katika hili ujaribu kuniamini”

“Mheshimiwa Rais hata mimi nakusisitiza kwamba mtimizie Mathew kila anachokitaka na hutajutia” akasema Dr Evans

“Kwa ajili yako Dr Evans nitafanya lakini roho yangu haitaki kabisa” akasema Dr Fabian na Mathew akainuka

“Mheshimiwa rais ahsante kwa kulikubali ombi langu.Sina kingine ninachohitaji toka kwako.Ninachoomba kwa sasa ni kuonana na Ruby” akasema

Mathew na Dr Evans akamuita mmoja wa wasaidizi wake akamtaka awapeleke akina Mathew katika nyumba yake aliko Ruby.Mathew na Austin wakawaaga Dr Fabian na Dr Evans wakaondoka kuelekea anakoishi Ruby.

“Dr Evans nini hiki umenifanyia leo? Sikutegemea kabisa ! akasema Dr Fabian baada ya akina Mathew kuondoka

“Fabian leo umefanya kitu kibaya sana.Umeonyesha dharau kubwa kwa Mathew

Mulumbi.Sikutegemea kabisa.Taifa linamuhitaji sana Mathew kwa wakati huu na ninaweza kusema kwamba ni Mungu ndiye aliyemleta.Hukupaswa kumtamkia maneno kama yale” akasema Dr Evans

“Utanisamehe mzee wangu lakini Yule kijana aliniudhi sana.Kuibuka kutoka kusiko julikana halafu anaanza kuhoji maamuzi yangu.Anataka kunifundisha namna ya kuongoza nchi.Sikupenda jambo lile”

“Hakuwa anakufundisha kuongoza bali alikuwa anasema kitu cha kweli.Makosa makubwa yamekwisha fanyika Fabian japokuwa hamtaki kukubali na ulipaswa kushukuru kwani Mathew Mulumbi ndiye ambaye amekuja kurekebisha pale ulipokosea.Hakukosea kusema kwamba mliongozwa na hasira kufanya maamuzi yale ya kuandaa kikosi cha jeshi kumsaka James Kasai.Alitumia lugha kali kidogo ya kukurupuka na mimi ninarudia

kusema kwamba mlikurupuka.Fabian kinachoendelea hivi sasa Afrika mashariki kinawafanya mabeberu wafungue chupa za shampeni wakifurahia.Muache Mathew Mulumbi akamuondoe James Kasai.Mpe kila anachokihitaji na utaona matokeo yake" akasema Dr Evans.

Walikuwa na mazungumzo marefu kisha Dr Evans akaaga na kuondoka

****

Mathew na Austin waliwasili katika nyumba ya Rais anakoishi Ruby.Walikaribishwa ndani kisha mmoja wa watumishi akaenda kumjulisha Ruby kwamba kuna wageni wake wamekuja kumtembelea.Ruby hakupoteza muda akatoka chumbani kwake na kuelekea sebuleni huku akijua wageni wale lazima watakuwa wametumwa na Rais.Alipoingia

sebuleni mtu wa kwanza kumuona alikuwa ni Austin

“Austin ! akasema kwa sauti ndogo ya mstuko na kuanza kupiga hatua ndogo mara akapawa na mstuko wa mwaka baada ya kugonganisha macho na Mathew.Mstuko alioupata ulikuwa mkubwa akataka kuzungumza kitu sauti haikutoka midomo ikamtetemeka.

“Hallo Ruby ! akasema Mathew lakini Ruby hakujibu kitu alishindwa kuzungumza

“Ruby it’s me Mathew.Please say something ! akasema Mathew

“I…I…I.don…I don’t kn……..”akasema Ruby akitetemeka mdomo kisha akajikuta ameangukia mikononi mwa Mathew nakuanza kulia machozi mengi

“Nyamaza Ruby” akasema Mathew

“Why Mathew ?!! Why ?!! akauliza Ruby huku akiendelea kumwaga machozi

“Ruby please.I know this is a surprise to you and you have

so many question to ask but right now you and I we need to go somewhere" akasema Mathew na Ruby akainua kichwa akafuta machozi na kumtazama Mathew

"Oh my God ! Why Mathew?Kwa nini umenitesa namna hii?akauliza Ruby na kukilaza kichwa chake kifuani kwa Mathew akiendelea kulia

"Ruby tutazungumza nitakueleza kila kitu lakini kwa sasa nakuomba ujiandae tuondoke"

“Sina haja ya kujiandaa Mathew.Twende kokote unakotaka hivi hivi nilivyo” akasema Ruby kisha wakainuka na kuelekea katika gari wakaondoka.Ndani ya gari bado Ruby aliendelea kumwaga machozi hadi walipofika nyumbani kwa Mathew ambako walishuka kisha akampa Austin maelekezo kadhaa na kumuachia gari akaondokanalo wao wakaingia ndani na kuelekea moja kwa moja hadi chumbani kwa Mathew.

“Ruby there is only one thing I need right now ! akasema Mathew na kumkumbatia Ruby akaanza kumbusu.Ruby alisisimka unyayo hadi unyweleni.Hatimaye mwanaume Yule aliyempenda kwa moyo wake wote leo hii ametua tena katika mikono yake.Bado Ruby alijihisi kama yuko ndotoni.Kadiri sekunde zilivyozidi kwenda ndivyo alivyozidi kuona mabadiliko katika mwili wake na kugundua kile ambacho kilikuwa

kinaendelea.Akamkumbatia Mathew kwa nguvu na kuanza kumporomoshea mabusu mengi.Mathew akaivua fulana akaitupa na Ruby akastuka baada ya mkono wake laini kukutana na makovu makubwa ya vidonda mgongoni kwa Mathew

“Mathew what’s this?akauliza

“Utauliza baadae..” akasema Mathew huku akiendelea na zoezi.Ruby alishindwa kuvumilia zaidi akamtaka Mathew kuanzisha

mpambano.Filimbi ikapulizwa na mpambano wa kukata na shokaa ukaanza.

****

“Mathew is this real?Au niko ndotoni?akauliza Ruby akiwa amemkumbatia Mathew baada ya kumaliza mzunguko mmoja

“Ruby hii si ndoto.Ni kweli tuko wote” akasema Mathew

“Mathew ninashindwa niseme nini ndiyo maana ninabaki tu ninalia”

“Usilie Ruby ni mimi Mathew Mulumbi Yule Yule unayemfahamu.Usiwe na wasiwasi wowote” akasema Mathew

“Ulikuwa wapi?What happened to you? Nimelia machozi mengi sana kwa ajili yako Mathew lakini leo Mungu amesikia kilio changu na amekuleta tena.Naamini haya ni maongozi ya Mungu kwani nimepitia magumu mengi hadi kufika hapa Tanzania lakini kumbe yale yote niliyokuwa nayapitia ni kwa ajili ya kuja

kukutana tena nawe Mathew” akasema Ruby na machozi yakaanza tena kumtoka

“Ruby huu si muda wa kulia”

“Mathew niache nilie tafadhali nimeteseka sana,nimelia sana baada ya kupata taarifa ya kufariki kwako.Nashindwa hata nikueleze vipi” akasema Ruby

“Naelewa Ruby.Hata mimi haukuwahi kubanduka katika mawazo yangu.Ruby kuna mengi ya kuzungumza.Naamini unataka sana kujua nini

kilinitokea na nilikuwa wapi.Mimi pia nina hamu sana ya kutaka kufahamu mengi kuhusu wewe katika kipindi hiki chote ambacho sikuwepo lakini hayo ni baadae kwa sasa kuna kitu cha muhimu nataka kukufahamisha” akasema Mathew

“Niambie Mathew” akasema Ruby

“Kuna misheni nzito imenirudisha hapa nyumbani na ninakuhitaji sana katika misheni hiyo muhimu” akasema

Mathew na Ruby akaonyesha mstuko kidogo

“Mathew hata baada ya masahibu yote kukutokea bado unaendelea na hizi kazi?akauliza Ruby

“Ni misheni muhimu sana kwa nchi Ruby”

“Misheni ipi hiyo? Akauliza Ruby

“Nadhani Rais amekwisha kufahamisha kuhusiana na kile kilichotokea hapa nchini siku chache zilizopita”

“Ndiyo nilikutana na Rais jana ikulu tukawa na

mazungumzo marefu kuhusiana na kazi aliyoniita nije kuifanya.Rais ameniita hapa nyumbani kwa ajili ya kuiongoza idara ya siri ya mambo ya ndani ya nchi ile ambayo alikuwa anaiongoza Devotha" akasema Ruby

"Ninafahamu.Austin amekwisha nieleza kila kitu na Rais pia ameniambia hivyo"

"Umeonana na Rais tayari?

"Ndiyo nimeonana na Rais.Nilitoka ikulu kuonana naye ndipo nikakufuata"

"Umekuja lini hapa nchini?

“Nimekuja juzi usiku” akajibu Mathew

“What a coincidence” akasema Ruby

“Nadhani utaona namna sote wawili tulivyorejeshwa nyumbani katika muda ulio karibu sawa.Sikujua kama nitakutana nawe huku na wewe hukujua kama utakutana nami.Kukutana huku kuna sababu kubwa.Nchi yetu kwa sasa inapitia kipindi kigumu sana kufuatia shambulio lile lililotokea hivi majuzi na kuua wake watatu wa

marais,mabalozi na raia wengine.Sitaki kurudia kwani Rais amekwisha kueleza kila kitu”

“Ndiyo amenieleza kila kitu jana.Ni tukio baya kabisa kutokea”akasema Ruby

“Aliyefanya tukio lile anaitwa James Kasai ambaye ameshirikiana na kundi la kigaidi la IS na kuleta mvurugano mkubwa katika nchi za jumuiya ya Afrika mashariki.Hivi sasa nchi hazielewani na nyingine zinashambuliana.Huu ni

mpango mkubwa kuisambaratisha jumuiya ya Afrika Mashariki ulioandaliwa na nchi kubwa na lengo kuu la kufanya hivyo wanailenga jamhuri ya kidemokrasia ya Congo.Shambulio lile ulikuwa ni mtego kwa nchi za Afrika mashariki na kwa bahati mbaya nchi zetu zimenasa katika mtego huo na hivi sasa amani imeanza kutoweka na jumuiya ya Afrika mashariki iko hatarini kusambaratika na mabeberu wanaelekea kupata ushindi.Misheni iliyonileta ni

kumuondoa James Kasai na kuutegua mtego wa mabeberu wa kuisambaratisha jumuiya ya Afrika Mashariki.Vile vile nimekuja kuung'oa mzizi wa IS uliopo hapa nchini.Ni misheni kubwa na nzito ndiyo maana ninakuhitaji sana uuungane nami katika misheni hiyo" akasema Mathew

"Mathew Mulumbi sijawahi kusema hapana kila pale uliponiita kwa ajili ya misheni yoyote toka tumefahamiana na hata sasa siwezi kusema hapana.Lakini Mathew huyu

James Kasai anaongoza kundi kubwa la waasi na wanaishi msituni.How are we going to end him?Rais Dr Fabian na wenzake wa Rwanda na Congo tayari wameandaa kikosi cha jeshi ambacho kitakwenda kumsaka James Kasai msituni na kuhakikisha kinamtia nguvuni”

“Huo ndio mtego ambao viongozi wetu hawa walitegewa na wamenasa.Kutuma kikosi cha jeshi Uganda ni kosa kubwa wanataka kulifanya kwani kutaongeza machafuko badala

ya kumsaka James.Uganda tayari imekiita kitendo hicho ni uchokozi mkubwa na imeahidi kukisambaratisha hicho kikosi endapo kitakanyaga ardhi yake na huo utakuwa ni mwanzo wa machafuko makubwa sana na hicho ndicho mabeberu wanakihitaji.Ninasema kwamba nguvu za kijeshi hazitafaulu kwa kuwa James Kasai haishi msituni kama inavyodaiwa bali anaishi maisha ya kifahari sehemu Fulani jijini Kampala”

“James Kasai haishi msituni? Ruby akashangaa

“Ndiyo.James haishi msituni.Kwa muda mrefu serikali ya Uganda imekuwa ikimfadhili James katika mapambano yake dhidi ya serikali ya Congo na wakati dunia nzima wakifahamu James anaishi msituni lakini ukweli ni kwamba James anaishi kifahari jijini Kampala.Watu wengi hata ndani ya Uganda yenyewe hawajui kama James Kasai anaishi kifahari katika ardhi yao” akasema Mathew

“Unafahamu anakoishi James ?Ruby akauliza

“Nitafahamu muda si mrefu mahala alipo na ndiyo maana nilimfuata Rais leo na kumtaka asitishe mipango yote ya kijeshi ya kumsaka James Kasai kwani nimerejea nyumbani kwa ajili ya kazi hiyo”akasema Mathew

“Rais amekubali?

“Amenipa siku saba niwe nimefanikiwa kumpata James Kasai au atapeleka kikosi cha jeshi cha umoja ambacho kinaendelea na mazoezi hivi sasa.Tayari nimeandaa timu kwa ajili ya operesheni hiyo.Mimi,Austin vile vile

tutawaongeza vijana wawili.Gosu Gosu hatakuwepo kwa kuwa yuko hospitali amepigwa risasi na watu wasiojulikana” akasema Mathew

“Gosu Gosu amepigwa risasi?! Ruby akashangaa

“Ndiyo.Hali yake si nzuri.Kwa hivi sasa anapumua kwa msaada wa mashine”

“Oh jamani” akasema Ruby kwa masikitiko

“Nimezungumza na Rais tumekubaliana kwamba kesho ataenda kukukabidhi rasmi ofisi

ili kazi ianze mara moja.Tutaihitaji sana ofisi ile kwani ina msaada mkubwa kwetu katika misheni hii.Baada ya kumaliza misheni ya James Kasai tutaingia katika misheni nyingine ya kuung'oa mzizi wa IS hapa nchini" akasema Mathew

"Mathew kama nilivyokwambia awali kwamba siwezi kusema hapana.Niko nawe katika misheni hii.Ninakuahidi kufanya kila niwezalo kukusaidia kuweza kufanikisha misheni hii"

“Ahsante sana Ruby” akasema Mathew na kuanza tena maandalizi kwa ajili ya kuingia katika mzunguko wa pili.

KAMPALA – UGANDA

Saa moja za jioni,katika makazi ya Rais wa Uganda yaliyo ndani ya kambi ya jeshi,kulikuwa na kikao kinaendelea kati ya Jenerali Akiki Rwamirama Rais wa Uganda.James Kasai na Melanie Davis

“Mheshimiwa Rais jana nilikutana na James.Nilimuita mimi na kubwa nililomuitia ni kujadili kwa kina kuhusiana na ule mpango wetu niliouleta kwenu wa kumuua Rais Patrice Eyenga.Tulipokutana mara ya mwisho ulituahidi kutupa mrejesho baada ya kuzungumza na mkuu wa majeshi wa Congo lakini baada ya kutafakari sana nikaona kuungana na wanajeshi wa Congo kutakuwa na changamoto kubwa ambayo ni kuchelewa kwa mpango wenyewe ambao mimi nataka

ufanyike haraka.Baada ya kukutana na James tumekuja na mpango mpya” akanyamaza kidogo na kusema

“Utampigia simu Rais wa Tanzania na kumtaka aitishe kikao kati yako na Rais wa Congo kwa ajili ya mazungumzo ya kutafuta muafaka kwa njia ya amani.Naamini Rais Patrice Eyenga lazima atakubali kukutana kwa ajili ya mazungumzo hayo.Atakapokuwa Dar es salaam wakati mazungumzo yakiendelea bomu litawekwa

katika ndege yake na atakapoondoka kurejea Kinshasa bomu hilo litalipuliwa na utakuwa ni mwisho wa Patrice atakuwa amebaki mtu mmoja katika orodha yangu Dr Fabian Kelelo” akasema Melanie.Baada ya kutafakari kidogo Jenerali Akiki akasema

“Ni mpango mzuri na mimi ninauunga mkono lakini ugumu wa mpango huo ni namna ya kuliingiza bomu katika ndege hiyo ya Rais” akasema Jenerali Akiki

“Kwa upande huo hakutakuwa na ugumu wowote.Mimi nitalishughulikia suala hilo.Ninao mtandao mpana jijini Dar es salaam hivyo hakutakuwa na tatizo katika kuingiza bomu hilo ndani ya ndege ya Rais” akasema Melanie

“Mimi nina wazo lingine lakini halijaenda mbali na mpango huo wa kumuua Patrice Eyenga.Badala ya kupandikiza bomu ndani ya ndege ya Rais,kwa nini tusiandae shambulio la kujitoa mhanga na

kuwamaliza marais hao wote wawili kwa wakati mmoja yaani Rais Patrice Eyenga na Rais Dr Fabian Kelelo? Kwa kuwa tayari unao mtandao mkubwa tunaweza kumuandaa mtu atakayebeba bomu na pale Rais Fabian atakapokuwa anamsindikiza Rais Patrice basi mtu huyo atajilipua na kuwauwa marais hao wote wawili kwa mara moja na orodha yako itakuwa imekamilika utaendelea na maisha yako kama kawaida" akasema James Kasai

“Huu nao unaonekana ni mpango mzuri sana James” akasema Melanie

“Hata mimi naona huu ni mpango mzuri” akasema Jenerali Akiki

“Kama nyote mnakubaliana na mpango huu nitazungumza na watu wa IS ili wanipatie mtaalamu wa kuunda mabomu ya kujitoa mhanga ambaye atakuja Dar es salam kwa ajili ya kutengeneza bomu hilo hivyo basi Melanie unatakiwa ufanye mpango ili niweze kuingia Dar es salaam kwa ajili ya jambo

hilo.Unao mtandao mkubwa na nina imani kwa mimi kuingia Dar es salaam hakutakuwa na tatizo” akasema James

“Ndiyo ninao mtandao mkubwa na unaweza ukaingia na kutoka Dar es salaam bila matatizo yoyote.Kuna idara inaitwa SNSA.Hii ni idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi.Mkurugenzi wa idara hii yupo katika mtandao wangu na amewekwa pale makusudi kabisa kwa ajili ya kunisaidia mimi kufanikisha operesheni zangu hivyo basi kwa kumtumia

yeye na idara yake utaingia Tanzania na kutoka salama” akasema Melanie

Waliendelea na kikao na kukubaliana namna watakavyofanikisha suala lile kisha James akamrejesha Melanie mahala alikofikia na yeye akaondoka kuelekea katika makazi yake.Nusu saa baada ya Melanie kurejea mahala alikofikia,Jenerali Akiki akawasili

“Mheshimiwa Rais” akasema Melanie kwa mshangao kidogo hakuwa

ametarajia kama Jenerali Akiki angeweza kumfuata usiku ule.

“Melanie siwezi kupitisha usiku huu bila kuwa nawe ndiyo maana nimekuja.James hajagundua chochote kama mimi nawe tulionana na tukazungumza?

“Hajafahamu chochote”

“Vizuri sana.Naomba usihofu kila kitu kitakwenda sawa kabisa .Pale mtakapokuwa mmekamilisha mipango yote kuhusiana na hilo bomu basi mtanijulisha na mimi nifanye yala ya upande wangu yaani

kuwaita mezani marais hao wanaotakiwa kuuawa.Nitakuunga mkono Melanie katika kila unachotaka kukifanya.Hata hivyo nina wazo moja kwa nini usiingie katika siasa? Mimi nitakupigania na utafika mbali sana.Unaweza hata kuwa Rais” akasema Jenerali Akiki

“Hapana mheshimiwa Rais.Sitaki kuwa mwanasiasa.Nina mipango mingine kabisa”

“Mipango ipi? Akauliza Jenerali Akiki

“Siwezi kuisema kwa sasa ngoja kwanza nimalize mpango wangu wa kulipiza kisasi halafu nitakwambia nini kinafuata” akajibu Melanie

DAR ES SALAAM – TANZANIA

Mathew na Ruby walirejea nyumbani kwa Mathew baada ya kutoka hospitali kufuatilia maendeleo ya Gosu Gosu ambaye bado hali yake haikuwa na mabadiliko.Ruby alipitiliza moja kwa moja bafuni kisha Mathew akafungua kasiki akatoa kompyuta yake na

kuelekea katika chumba cha ofisi akamtafuta Habiba Jawad mtandaoni na kumpigia

“Mathew Mulumbi habari za Dar es salaam?

“Huku kwema mama.Mnaendeleaje huko?akauliza Mathew

“Huku tuko salama.Vipi wewe maendeleo yako? Mipango yako inakwendaje?

“Leo nimekutana na Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania nikazungumza naye nikamueleza kuhusu misheni yangu ya kumuondoa James

Kasai nikamtaka asitishe operesheni zozote za kijeshi wanazotaka kuzifanya nchini Uganda kumsaka James.Hakuonekana kufurahishwa na ombi langu hilo ila amenipa siku saba niwe nimempata James Kasai ama sivyo wataendelea na operesheni zao za kijeshi kama walivyopanga.Tayari nimeunda timu maalum kwa ajili ya operesheni hiyo na sasa ninasubiri maelekezo yako mama ili kazi ianze mara moja” akasema Mathew

“Vizuri sana” akasema Habiba na kunyamaza kidogo

“Usiku huu nimepata taarifa kwamba kuna mtu anaitwa Khalid Sultan Khalid.Huyu anatokea nchini Syria.Ni mtaalamu mkubwa sana wa milipuko.Taarifa niliyoipata ni kwamba Khalid anakuja Tanzania.Ameelekezwa na viongozi wa IS kwenda Tanzania na kwa taarifa nilizozipata ni kwamba Khalid anakuja kukutana na James Kasai jijini Dar es salaam”

“James Kasai anakuja Dar es salaam?

“Ndiyo anakuja kukutana na Khalid.Inaonekana IS kwa kushirikiana na James Kasai wanataka kufanya shambulio lingine kubwa jijini Dar es salaam.Kazi yako ni kuhakikisha mipango hiyo haifanikiwi na uhakikishe unamuua Khalid na James Kasai.Mathew kama kuna shambulio linaandaliwa basi litakuwa ni kubwa sana kwani Khalid hushiriki katika mashambulio makubwa

makubwa.Taarifa hiyo nimekupa ni jukumu lako wewe na timu yako kuhakikisha mnafahamu ni kitu gani Khalid na wenzake wanakipanga na kama ni shambulio basi mhakikshe halifanyiki na mwisho kabisa Khalid na James Kasai hawapaswi kutoka hai nchini Tanzania.Umenielewa Mathew? Akauliza Habiba

“Nimekuelewa mama.Nitatekeleza kama ulivyoagiza .Lini Khalid anatarajiwa kuingia nchini? Akauliza Mathew

“Khalid anatumia hati ya kusafiria ya Saudi Arabia yenye jina Nassor Khalid.Kwa taarifa nilizonazo Khalid ataingia nchini Tanzania kesho kutwa.Nitakupa taarifa zote kuhusiana naye kesho usiku”

“Vipi kuhusu James Kasai amekwisha ingia Tanzania? Au anatarajiwa kuingia nchini lini na kwa njia gani?akauliza Mathew

“Bado sijajua.Mathew siwezi kujua kila kitu.Ni jukumu lako sasa kutafuta James Kasai ataingiaje nchini Tanzania

lakini nitakapofahamu chochote nitakujulisha.Nitakutumi vile vile picha za Khalid Khalid ili uanze kumfuatilia” akasema Habiba

“Sawa mama nashukuru sana kwa taarifa hizi ulizonipa.Nitaanza kuzifanyia kazi mara moja” akasema Mathew akaagana na Habiba Jawad akaifunika kompyuta yake

“Mambo yameanza kupamba moto.IS na James Kasai wanapanga tena shambulio lingine.Safari hii

wameliekeza wapi hilo shambulio? Akajiuliza Mathew.

“James Kasai ni mtu mweye roho ya jiwe.Pamoja na kujua kwamba anatafutwa sana na serikali ya Tanzania kufuatia shambulio kubwa alilolifanya siku chache zilizopita lakini bado anataka kuingia nchini na kupanga tena shambulio lingine.Kwa nini anajiamini kiasi hiki? Akajiuliza

“James hawezi kuingia hapa nchini kama hakuna watu wanaomsaidia.Lazima anao mtandao wake wa watu ambao

wanamuwezesha kuingia nchini na kutoka atakavyo.Hana wasi wasi hata kidogo kama anaweza akakamatwa.Lakini ni nani hao wanaomuwezesha kuingia nchini mtu kama huyu?akajiuliza

“Ameungana na kundi la kigaidi la IS.Kwa namna yoyote ile hawa ndio wanaomuwezesha kuingia hapa nchini na kutoka bila wasiwasi.Lazima IS wana mtandao mrefu sana hapa nchini na ndiyo maana Habiba alinitaka nije

niung’oe.Nakumbua wakati ule hadi waziri mkuu wa jamhuri ya muungano wa Tanzania alikuwa ni mmoja wa watu wao hii inaonyesha ni namna gani hawa jamaa walivyodhamiria kujijenga katika ukanda huu wa Afrika Mashariki”akawaza Mathew na kuvuta pumzi ndefu

“Mwisho wa James Kasai umewadia.Atakapoingia nchini hatatoka salama” akawaza Mathew na kuifungia kompyuta yake katika droo kisha akarejea chumbani na kumkuta Ruby akiwa amejilaza kitandani.

“Are you okay Mathew?akauliza Ruby

“Kuna taarifa nimeipata kwamba James Kasai anakuja hapa Dar es salaam”

“James anakuja Dar es salaam? Ruby naye akashangaa

“Ndiyo anakuja Dar es salaam”

“He mus be crazy.Anawezaje kuthubutu kuja Dar es salaam huku akijua kwamba anatafutwa kwa nguvu zote kufuatia shambulio lile alilolifanya?akauliza Ruby

“Hata mimi nashangaa anajiamini nini”

“Taarifa hiyo uliyopata imetoka katika chanzo kinachoaminika?Ruby akauliza

“Ndiyo ni chanzo cha kuaminika sana.Si James Kasai pekee anayekuja Tanzania bali pia kuna mtu anaitwa Khalid Sultan Khalid ambaye ni mtaalamu wa milipuko mikubwa ndani ya kundi la IS naye anakuja Tanzania na anakuja kuonana na James Kasai hapa Dar es salaam.Inaonekana kuna

shambulio lingine kubwa linaandaliwa na hawa jamaa ndiyo maana wanakuja kukutana hapa Dar es salaam” akasema Mathew na kukumbuka kitu

“Habiba alinituma Dubai kushuhudia IS wakisaini makubaliano ya kumtumia James Kasai kiasi kikubwa cha fedha ambacho kilitoka kwa Habiba ndiyo maana Najma alikuwepo kumuwakilisha.Sikumbuki jina la Yule mwanamke mrembo aliyemuwakilisha James lakini

nakumbuka alitokea Tanzania.Sura yake bado haijanitoka kichwani,bado ninamkumbuka. Fedha ambazo IS wanampatia James zinapita Tanzania kwa Yule mwanamke.Nina uhakika mkubwa kama James anakuja Tanzania lazima ataonana naye hivyo tukimpata Yule mwanamke tutakuwa tumempata James Kasai" akawaza Mathew na kutoa tabasamu

"Sasa nimepata picha kwa nini Habiba Jawad alinituma

Dubai nikashuhudie makubaliano yale kati ya IS na James Kasai.Yule mwanamama ana akili sana” akawaza Mathew na kutoka akaelekea katika ofisi yake akachukua kalamu na karatasi Akakaa mezani na kuanza kuikumbuka sura ya Yule mwanamke ambaye alimuwakilisha James Kasai Dubai huku akiichora katika karatasi.

“Namshukuru Mungu aliyenipa pia kipaji kikubwa cha uchoraji’akawaza Mathew wakati akiendelea kuichora

sura ya Yule mwanamke.Alipomaliza akaitazama picha ile na kutabasamu.

“Alikuwa hivi hivi” akawaza Mathew kisha akatoka na kurejea chumbani

“Ruby kuna kazi ambayo nahitaji unisaidie” akasema na kumpa Ruby ile picha aliyoichora

“Huyu ni nani? Ruby akauliza

“Ninataka unisaidie kumfahamu mwanamke huyu ni nani.Kesho utakapokwenda

SNSA kitu cha kwanza ambacho ningetaka ukifanye ni kuingia katika kumbu kumbu zote za usajili hapa Tanzania na umtafute mwanamke huyu.Ni muhimu sana” akasema Mathew

“Anahusiana na James Kasai?akauliza Ruby

“Nitakueleza hapo kesho tutakapokuwa tumepata taarifa zake ndiyo maana nilimtaka Rais akukabidhi ofisi kesho kwani ukiwa ndani ya SNSA una uwezo wa kupata kila aina ya

taarifa tunayohitaji” akasema Mathew

****

Sa kumi na mbli za asubuhi tayari Mathew alikuwa amefika katika nyumba ya Rais alikofikia Ruby akimrejesha baada ya usiku mzima kuwa naye nyumbani kwake.Waliagana kwa miadi ya kuonana tena baadae kisha moja kwa moja akaelekea hospitali alikolazwa Gosu Gosu.Mara tu alipofika hospitali alikutana na Austin

ambaye alikuwa na sura yeye tabasamu kubwa

“Austin tabasamu hili la asubuhi nashindwa kulielewa” akasema Mathew

“Hali ya Gosu Gosu imebadilika ghafla usiku wa leo na kwa sasa ameondolewa katika ile mashine ya kumsaidia kupumua.Madaktari wanasema mifumo yake yote imeanza kufanya kazi vyema na sasa anapumua kama kawaida”

“Ahsante Mungu” akasema Mathew na kugonganisha mikono na Austin kisha

akaingia katika chumba alichokuwa amelazwa Gosu Gosu.Hakuwa amerejewa na fahamu bado lakini kwa mujibu wa madaktari hali yake ilikuwa inaendelea vizuri na walitegemea haingechukua muda mrefu kabla hajarejewa na fahamu zake

“Ahsante sana Papi kwa hatua hii nzuri.Umezifanya nyuso zetu zitabasamu asubuhi ya leo.Naamini muda si mrefu utafumbua macho.Natamani sana tuonane uso kwa uso

Papii” akasema Mathew na kunyamaza kidogo

“Mambo yameanza Gosu Gosu.Mji unakwenda kuwaka moto natamani sana ugekuwepo ndugu yangu lakini usijali ninakuhitaji sana katika misheni nyingine zinazokuja.Endelea kupambana,nataka nitakapokuja tena hapa jioni ya leo nikukute ukiwa tayari umefumbua macho na tuzungumze” akasema Mathew kisha akatoka na kumfuata Austin

“Mathew nilikuona jana ukimtamkia Gosu Gosu maneno Fulani kwa hisia kubwa.Naamini amekusikia” akasema Austin

“Tumshukuru Mungu kwa maendeleo haya mazuri ya Gosu Gosu” akasema Mathew na kumtaka Austin waelekee garini

“Ulifanikisha maelekezo yangu ya jana?akauliza Mathew

“Ndiyo Mathew.Jana tulipoachana nilikamilisha kila kitu” akasema na kushuka katika gari la Mathew akaenda katika gari lake akachukua

mkoba mdogo na kurejea kwa Mathew

“Nilifanikiwa kusajili laini tatu za simu kama ulivyokuwa umeelekeza” akasema Austin na kumpatia Mathew simu tatu

“Good.Mimi nitakuwa na moja,wewe pia utakuwa na moja na itakayobaki atatumia Ruby.Mambo yameanza Austin.Kwa taarifa nilizo nazo ni kwamba James Kasai anatarajia kuingia hapa nchini sijafahamu lini na ataingia vipi ” akasema Mathew

“James Kasai anakuja Dar es salaam? Austin naye akashangaa

“Ndiyo Austin.James Kasai anakuja Dar es salaam.Anakuja kuonana na mtu anaitwa Khalid Sultan Khalid ambaye ni mtaalamu mkubwa wa milipuko kutoka katika kundi la IS.Kuna shambulio lingine wanakuja kulipanga hapa Dar es salaam” akasema Mathew

“Nimeshangaa sana kusikia huyu gaidi ana mpango wa kuja Tanzania wakati bado vidonda vya shambulio alilolifanya hivi

majuzi havijapona” akasema Mathew

“Kwa bahati nzuri atakapokuja hatarejea tena Uganda.Utakuwa ndio mwisho wake na kama ananisikia huko aliko labda aahirishe safari lakini kama akija Tanzania ndipo roho yake itakapoachana na mwili” akasema Mathew

“Tatizo ni kufahamu ni namna gani ataingia nchini.Je atakuja kwa ndege,atapita kiwanja gani?Hivi sasa video yake imesambaa kila mahala na

kila mtu anamjua ni gaidi atapita wapi?Austin akauliza

“James anao mtandao wake katika nchi hizi za Afrika Mashariki ndiyo maana mpaka leo imeshindikana kumkamata anaweza akaingia katika nchi yoyote na kutoka vile atakavyo lakini safari hii kiama chake kimefika hatatoka salama”akasema Mathew na kumtaka Austin akawachukue wale vijana wawili waliopanga kuwa nao katika operesheni ile na kupanga wakutane

nyumbani kwake ambako ndiko kutakuwa ofisi kuu

****

Msafara wa Rais wa jamhuroi ya muungano wa Tanzania uliwasili katika jengo la makao makuu ya idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi.Hakuwa ametoa taarifa kama atafika pale hivyo kufika kwake ulikuwa ni mshangao kwa kila mtu.Edwin Mbeko mkuu wa idara ile alitoka mara moja ofisini kwake na kwenda

kumpokea Rais akamkaribisha ndani.Rais hakuwa peke yake alikuwa ameambatana na Ruby wakaingia ndani na wafanyakazi wote wakaacha kazi zao wakasimama mara Rais alipoingia.Akawasalimu kisha akaongozana na Edwin hadi katika ofisi yake

“Karibu sana mheshimiwa Rais” akasema Edwin

“Nashukuru sana Edwin.Utanisamehe kwa kuja bila taarifa”

“Usijali mheshimiwa Rais hapa ni nyumbani kwako huna

haja ya kubisha hodi” akasema Edwin

“Edwin sitaki kuchukua muda mrefu sana.Nimekuja kwa jambo moja tu la muhimu” akasema na kumgeukia Ruby

“Huyu mwanamama niliyeongozana naye anaitwa Annabel Jones.Nimemteua kuwa mkurugenzi mpya wa idara hii kuanzia leo na wewe utaendelea kuwa msaidizi wake.Atatumia ofisi iliyokuwa ya Tamar kwa muda wakati ofisi yake mpya ikiandaliwa.Ahsante sana kwa

kukaimu nafasi hii muda mrefu umefanya kazi nzuri na sasa nimempata mtu ambaye atachukua nafasi ya ukurugenzi.Natagemea utampa ushirikiano mkubwa” akasema Dr Fabian na Edwin akajenga tabasamu

“Karibu sana mama Annabel.Mimi ni Edwin Mbeko kama alivyosema mheshimiwa Rais nimekuwa nikikaimu nafasi hii ya ukurugenzi kwa zaidi ya miaka mitatu.Ninamshukuru sana Rais kwa kukuteua na ninakuahidi

ushiriano mkubwa kutoka kwangu na kwa wafanyakazi wote” akasema Edwin.Baada ya kumaliza kile kilichompeleka pale Dr Fabian akaondoka zake.Baada ya Rais kuondoka Edwin akawataka wafanyakazi wote wakusanyike katika ukumbi mkubwa kisha akaenda kumtambulisha Ruby kama mkurugenzi mpya wa idara ile.Baada ya utambulisho ule akaenda kumfungulia Ruby ofisi ambayo ataitumia na Ruby akaanza rasmi kazi kama mkurugenzi mkuu wa SNSA.

Wakati Ruby akiwa ofisini kwake Edwin akatoka na kwenda sehemu ambako alitoa simu na kumpigia simu Devotha

“Edwin habari za Tanzania?akauliza Devotha

“Habari za huku ni njema lakini kuna jambo limetokea asubuhi hii nimeona nikujulishe mara moja”

“Kumetokea nini?akauliza Devotha

“Mheshimiwa Rais ametoka hapa muda si mrefu”

“Amekuja kutafuta nini?

“Amemleta mkurugenzi mpya wa SNSA”

“Mkurugenzi mpya?

“Ndiyo Devotha”

“Kwa nini amekuacha wewe ambaye umekaimu kwa muda huu wote na akamteua mtu mwingine?

“Sifahamu hayo ni maamuzi yake.Nimekupigia kukujulisha kwamba kuna baadhi ya mambo ambayo nitashindwa kuyatekekeleza kwa kuwa sintakuwa na nguvu niliyokuwa nayo awali”

“Usijali kuhusu hilo.Tuko karibu sana kumaliza misheni yetu.Umewasiliana na Melanie?

“Ndiyo nimewasiliana naye na amenitaka nifanye maandalizi jioni ya leo niende kumpokea kwani anakuja na James Kasai.Tayari nimekwisha fanya maandalizi yote ndege yetu ndogo iko tayari na baadae leo nitaelekea Bukoba kumpokea”akasema Edwin

“Una hakika ujio wa huyo mkurugenzi mpya hautaathiri kitu chochote katika mipango yetu?akauliza Devotha

“Hapana haitaathiri kitu chochote.Bado ni mgeni na hafahamu kitu chochote”

“Vizuri.Tunakutegemea sana Edwin na hakikisha hakuna kitu kitakachoharibika hata kama amekuja mkurugenzi mpya lakini endapo utaona anakuwa ni kikwazo katika kufanikisha mambo yetu basi hakuna haja ya kumchelewesha tumuondoe mara moja” akasema Devotha

“Usiwe na hofu Devotha hakuna kitu kitakachoharibika” akasema Edwin

“Muda wowote kama kuna tatizo lolote nijulishe haraka sana” akasema Devotha na kuagana na Edwin.

****

Austin aliwasili katika makazi ya Mathew akiwa aeongozana na vijana wawili Tom Denzel na na Aidan Kengele.Mathew aliyekuwa akiwasubiri kwa hamu akawakaribisha na kuwapeleka moja kwa moja katika ofisi yake

“Karibuni sana Ton na Aida.Mimi naitwa Mathew Mulumbi.Naamini tayari kiongozi wenu Austin amekwisha wajulisha mimi ni nani hivyo naomba tuokoe muda na tuelekee moja kwa moja katika suala la msingi” akasema Mathew kisha akaenda mezani kulikokuwa na makaratasi mengi pamoja na picha akaichukua picha moja akaenda kuibandika katika ubao

“Mtu anayeonekana pichani anaitwa James Kasai.Huyu ana

umri wa miaka arobaini na nne.Ni mzaliwa wa Kivu Kaskazini na amepata elimu yake ya msingi,sekondari hadi chuo kikuu nchini Congo.Ana shahada ya sheria kutoka chuo kikuu cha Kinshasa.Baada ya kumaliza chuo kikuu alijiunga na jeshi.Baba yake pia alikuwa mwanajeshi katika jeshi la serikali mwenye cheo cha Jenerali lakini baadae aliasi na kuanzisha kundi lake ambalo lilianza kupambana na serikali.Jenerali Kasai baba yake James aliuawa na majeshi ya

serikali na ndipo James alipochukua uongozi wa kukiongoza kikundi cha waasi kilichoanzishwa na baba yake.Baada ya makundi yote ya waasi kukubali kuweka silaha chini na kumaliza machafuko yaliyodumu kwa miaka mingi,ni James Kasai pekee aliyegoma kuweka silaha chini hivyo akatimuliwa kutoka katika misitu ya Congo na kukimbilia nchini Uganda ambako inadaiwa amekuwa akiishi katika misitu iliyo Kaskazini mwa Uganda.Hivi majuzi James

Kasai amefanya shambulio hapa nchini na kuua wake za marais wa Tanzania,Congo na Rwanda.Huyu ndiye mtu ambaye tunamsaka.It's a capture or kill mission" akasema Mathew akawatazama watu wale waliokuwa wakimsikiliza kwa makini sana kisha akaendelea

"James Kasai haishi msituni kama inavyodaiwa bali anaishi jijini Kampala.Kwa muda mrefu amekuwa akifadhiliwa na serikali ya Uganda na kwa miaka ya hvi karibuni hali yake

kifedha haikuwa nzuri hivyo alilazimika kuingia makubaliano na kundi la kigaidi la IS ambao wanamfadhili kwa fedha na zana za kijeshi.Kwa nini IS wameingia makubaliano na James Kasai na si mtu mwingine?akauliza Mathew

“IS wana mpango wa kujitanua barani Afrika na wamechagua kujikita katika eneo la Afrika Mashariki na kati.Kwa sasa wanataka kupata sehemu ya kuweka kambi yao ya mafunzo ya ugaidi na wamekusudia kuweka kambi

hiyo katika misitu ya Kaskazini mwa Congo ndiyo maana wanamuhitaji James Kasai.Wanamuwezesha kwa fedha na zana za kijeshi ili aweze kurejea katika misitu ya Congo na kudhibiti eneo hilo.Wataweka kambi yao ya mafunzo ya kigaidi kati kati ya misitu ambayo itakuwa inadhibitiwa na James Kasai na ambaye ndiye atakayekuwa akiwalinda hivyo basi James Kasai ni mtu hatari sana kwa eneo zima la Afrika mashariki.Endapo IS

watafanikiwa kujenga kambi yao ya mafunzo ya kuwandaa magaidi basi eneo zima la Afrika Mashariki na kati halitaweza kukalika litakuwa katika hatari kubwa ya mashambulio ya kigaidi hivyo basi kwa namna yoyote ile lazima James Kasai akamatwe au auawe”

“Umesema James Kasai haishi msituni bali anaishi jijini Kampala,unafahamu anapoishi? Iwapo tutalazimika kwenda Kampala Uganda kumfuata James ni vipi endapo serikali ya Uganda watagundua kwamba

tunafanya operesheni ndani ya Uganda hivyo tukawa tumeanzisha mgogoro? Akauliza Tom Denzel

“Swali zuri Tom.Hatuna haja ya kwenda Kampala kumfuata James kwani anakuja hapa hapa nchini”

“James anakuja nchini?akauliza Aidan

“Ndiyo anakuja hapa nchini.Anakuja kukutana na huyu mtu” akasema Mathew na kuchukua picha nyingine akaibandika ubaoni

“Anaitwa Khalid Sultan Khalid.Huyu ni mtaalamu wa milipuko katika kundi la kigaidi la IS.Kukutana kwao jijini Dar es salaam ni kiashiria kwamba kuna shambulio lingine kubwa wanaliandaa kwani Khalid hushirikishwa pale panapotakiwa kufanyika shambulio kubwa” akasema na kunyamaza kidogo

“Naamini mtakuwa mnajiuliza James Kasai anafahamu kabisa kwamba anatafutwa kwa shambulio lile alilolifanya kwa nini haogopi

kuja Tanzania?Jibu ni kwa sababu tayari anao mtandao wake hapa Tanzania.Fedha ambazo James anapewa na kundi la IS zinapita hapa Tanzania.Kwa sasa mwenzetu mmoja anaitwa Ruby ambaye ameanza kazi leo katika idara moja nyeti ya serikali anashughulikia kumtambua mtu huyo ambaye ndiye IS wanapitishia kwake pesa kwenda kwa James Kasai.Pale atakapokuwa amepata chochote basi atatujulisha.Tom na Aidan nimeambiwa na kiongozi wenu

hii itakuwa ni misheni yenu ya kwanza toka mmemaliza mafunzo.Naomba niwaweke wazi wadogo zangu kwamba hii si misheni rahisi hata kidogo.Ni misheni ngumu na ya hatari kwani watu tunaowatafuta ni hatari pia.Kabla ya misheni kuanza rasmi ninawataka kama kuna yeyote anataka kutoendelea na misheni hii awe wazi ili tutafute mtu mwingine wa kushika nafasi yake.Remember we're doing this for our country" akasema Mathew na vijana wale

wakamuhakikishia kwamba wako tayari kuendelea na misheni ile kisha Mathew akawataka wakaanze kujiandaa kwani muda wowote wanaweza wakahitajika.Tom na Aidan wakaondoka kwa kutumia gari la Austin.

Dakika chache baada ya akina Tom kuondoka Mathew akajulishwa na walinzi kwamba kuna mgeni wake getini.Akatazama katika runinga iliyounganishwa na Kamera akaliona gari jeusi aina ya Mercedece benz.Hakujua

nani alikuwa ndani ya gari lile akaruhusu liingie kisha akashuka kwenda kumtazama mgeni Yule ni nani.Gari lile lilifika hadi karibu na kibaraza kisha mlango ukafunguliwa akashuka Ruby.

“Ruby ! akasema Mathew na kuachia tabasamu.Ruby akamfuata akamkumbatia

“Karibu sana.Sikutegemea kama ungekuja mida hii”akasema Mathew

“Imenilazimu nije kuna kitu cha muhimu” akasema Ruby

kisha Mathew akamuongoza wakaelekea ndani

“How’s your first day at work?Mathew akauliza

“Kikubwa nilichokifanya baada ya kupewa ofisi ni kujikita katika misheni yetu.Masuala mengine yatafuata baadae.Vipi nyie mnaendeleaje?Vipi Gosu Gosu?akauliza Ruby

“Mungu mkubwa kwani hali yake imebadilika usiku na sasa mifumo yake yote ya mwili inafanya kazi vyema amekwisha ondolewa katika mashine ya

kumsaidia kupumua” akasema Mathew

“Ahsante Mungu.Namuombea apone kwa haraka” akasema Ruby

“Tunamuhitaji sana” akasema Mathew na kuufungua mlango wa ofisi ambamo alikuwemo Austin akasalimiana na Ruby

“Ruby karibu sana.Muda mfupi uliopita tulikuwa na vijana ambao tutashirikiana nao katika misheni hii nikijaribu kuwapa picha ya misheni itakavyokuwa.Vijana

wameelewa na wako tayari kwa misheni.Kwa upande wako kuna taarifa gani?akauliza Mathew

“Nilipokabidhiwa ofisi nilianza mara moja kushughulikia ile picha uliyoichora.Sijafanikiwa kumpata mwenye ile picha lakini nimefanikiwa kuipata picha ya mtu mwingine ambaye anafanana mno na hii picha uliyoichora.Mwanzoni niliamini ni mwenyewe lakini baada ya kuichunguza hii picha uliyonipa na hii niliyoipata nimekuta

kuna utofauti.Picha hii ambayo nimeipata ni ya mwanamke anaitwa Melanie Chuma ambaye ni mfanya biashara.Hana taarifa nyingi na haionyeshi anaishi wapi wala biashara gani anayoifanya.Picha ya Melanie chuma inamuonyesha akiwa na kidoti chesi chini ya jicho na ana kovu katika kidevu chake.Hizo ni tofauti nilizozipata katika picha hizi mbili lakini sura ni ile ile.Mathew kwa kuwa wewe ndiye unayemfahamu vyema huyo mwanamke jaribu

kuitazama vyema picha hii ya Melanie Chuma na uthibitishe kama kweli ni yeye.Yawezekana katika mchoro wako ulisahau kuweka vitu hivyo viwili nilivyovitaja” akasema Ruby na kutoa picha katika mkoba wake akampatia Mathew akaitazama picha ile halafu akafumba macho kama vile kuna kitu anakikumbuka “What’s goig on here.Sura hii ni ile ile ya Yule mwanamke niliyemuona kule Dubai akimuwakilisha James Kasai lakini kama Ruby yuko sahihi kuna

utofauti.Ninaikumbuka vyema sana sura ya yule mwanamke na hakuwa na kidoti cheusi kwenye jicho lake wala hakuwa na kovu kidevuni vitu ambavyo huyu Melanie Chuma anavyo.Je wawili hawa ni mapacha? Akawaza Mathew na kustuliwa na Ruby

“Mathew ! akaita Ruby

“Najaribu kuvuta kumbu kumbu zangu kama nilikosea katika ile picha niliyochora lakini sikukosea.Mwanamke Yule niliyemchora hakuwa na

kidoti wala kovu” akasema Mathew

“Ni vipi kama alifuta kidoti hicho na hilo kovu kwa kutumia poda wanazopaka akina mama” akasema Austin huku akimtazama Ruby

“Make up” akasema Ruby

“Exctly.Ni vipi kama atakuwa amefunika alama hizo kwa make up? Austin

“Kwa nini afanye hivyo?Kuna sababu yoyote inayoweza kumfanya afunike alama hizo kwa make up?Ruby akauliza

“Hata kama angetumia make up kufunika hizo alama alizonazo lazima hili kovu la kidonda lingeonekana kwani linaonekana ni kovu kama la kuungua lakini sikuona kovu lolote usoni kwake.Ngozi yake ilikuwa nyororo kama malaika.Kila kitu unachokiona katika picha hii ni yeye isipokuwa alama hizo mbili.It’s real confusing” akasema Mathew na kuiweka picha ile mezani Austin akaichukua akaitazama na kupatwa na mshangao mkubwa.

“Nini Austin?Mbona umestuka?akauliza Mathew

“Huyu ndiye mchumba wa Gosu Gosu ! akasema

“What?

“Huyu ndiye mchumba wa Gosu Gosu.Alijitambulisha kwangu anaitwa Melanie” akasema Austin

“Austin are you sure?akauliza Mathew

“Ndiyo.Nimekutana naye zaidi ya mara moja ni huyu huyu lakini……” akasema Austin na kusita kidogo

“Lakini nini Austin?Mathew akauliza

“Nikijaribu kuvuta picha ya sura yake hana hili kovu linaloonekana pichani wala hiki kidoti chini ya jicho.Lakini naye alijitambulisha kwangu kwa jina la Malanie ila hakunitajia jina la ukoo wake lakini kila kitu ni hivi hivi”akasema Gosu Gosu

“Austin mtazame vizuri kama kweli huyu ndiye mchumba wa Gosu Gosu” akasema Austin

“Mathew sina shaka hata kidogo.Nimekutana naye zaidi

ya mara moja hivyo siwezi kumpotea.Ni mwenyewe kabisa isipokuwa hizi alama sijawahi kumuona nazo”akasema Austin

“Huyu Melanie Chuma ni nani hasa? Je ni ndugu na huyu mwanamke ambaye niliichora sura yake? Akauliza Mathew

“Kuna taarifa chache sana kuhusiana na Melanie Chuma ambazo nimezipata” akasema Ruby na kutoa karatasi akampa Mathew akalisoma kisha akalitupa mezani

“Taarifa ni chache sana kama alivyosema Ruby ambazo

haziwezi kuwa na msaada wowote kwetu.Kwa nini amekuwa na taarifa chache namna hii? Akauliza Mathew lakini hakuna aliyekuwa na jibu.Baada ya muda Ruby akauliza

“Mathew huyu mwanamke uliyemchora sura yake ambaye anafanana na Melanie Chuma umekutana naye wapi? Anaingia vipi katika misheni hii? akauliza Ruby.Mathew akainamisha kichwa akafikiri kidogo na kusema

“Nimewaeleza akina Austin kwamba James Kasai baada ya kufurushwa kutoka katika misitu ya Congo hali yake ya kifedha si nzuri na alihitaji kukiimarisha kikosi chake kabla ya kurejea tena msituni kupambana hivyo akaingia makubaliano na kundi la kigaidi la IS na katika makubaliano hayo IS walimuahidi kumpa fedha nyingi pamoja na silaha za kisasa kuimarisha kikosi chake.IS wanataka kumtumia James Kasai kwa ajili ya kupata sehemu ya kuweka kambi yao

ya mafunzo ya kigaidi katika misitu ya kaskazini mwa Congo.Huyu mwanamke ambaye nimeichora picha yake na kumtaka Ruby amtafute tumfahami ni nani na yuko wapi ndiye alisaini makubaliano ya fedha kati ya IS na James Kasai na fedha kutoka kwa IS zinapita kwake kabla ya kufika kwa James Kasai.Ninaamini kama tungeweza kumpata huyu mwanamke tungepata mambo mengi kuhusiana na James Kasai lakini sasa naona mambo yamejichanganya.Amejitokeza

mwanamke ambaye anafanana kwa kila kitu na huyu muwakilishi wa James Kasai lakini kuna tofauti ndogo” akasema Mathew

“Mathew kuna kitu ambacho kinazunguka kichwani kwangu.Unasema huyu mwanamke uliyeichora sura yake ndiye anayepokea fedha kutoka IS kwa niaba ya James Kasai? Akauliza Ruby

“Ndiyo” akajibu Mathew

“Kwani umemfahamu vipi huyo mwanamke? Ruby

akauliza.Mathew akatafakari kidogo halafu akasema

“ I was there and I witnessed everything” akasema Mathew.Austin na Ruby wakabaki wanamtazama

“I don’t understand Mathew.You witnessed what? Akauliza Ruby

“Guys” akasema Mathew na kuvuta pumzi ndefu

“Hamtaweza kunielewa kwa sasa.Ukweli ni kwamba nilikuwepo na nkashuhudia kila kitu wakati mwanamke huyu Melanie Chuma akisainiana

makubaliano na wawakilishi kutoka kundi la IS ya kupokea fedha kwa niaba ya James Kasai.Tafadhali naomba nisiulizwe maswali ilikuaje nikashuhudia jambo kama hilo" akasema Mathew

"So you knew about James Kasai and yet you let him do what he did? Akauliza Ruby

"Yes I did ! akajibu Mathew

"Why Mathew? That's not Mathew Mulumbi we all know.Mathew Mulumbi katu hawezi kukubali magaidi

wakafanikiwa mipango yao ! akasema Ruby

“Ndiyo maana nikasema kwamba hamtaweza kunielewa” akasema Mathew

“Make us understand ! akasema Ruby

“Let’s not talk about that okay? Akasema Mathew na ukimya ukapita

“Mathew mahala tulipofika tumekwama na wewe unazo taarifa ambazo zinaweza kutukwamua.Tafadhali tushirikishe na sisi pia kile unachokifahamu ili tusaidiane

mawazo namna ya kuweza kulikabili jambo hili linalozidi kuwa gumu” akasema Austin

“I didn’t do anything because I was undercover.Please don’t ask me more okay?akasema Mathew

“Austin unasema kwamba mchumba wa Gosu Gosu ambaye alijitambulisha kwako kwa jina la Melanie hana alama hizi alizonazo Melanie Chuma? Mathew akauliza

“Ndiyo hana alama hizi alizo nazo Melanie Chuma.Nimekutana naye zaidi

ya mara moja na sijawahi kumuona na alama hizi japo sura na kila kitu ni Melanie Chuma” akasema Austin

“Mwanamke Yule ambaye nilimuona Dubai akisaini makubaliano na IS naye anafanana kwa kila kitu na Melanie Chuma isipokuwa ni hizo alama.Kwa hiyo yawezekana huyo mchumba wa Gosu Gosu ndiye Yule mwanamke ambaye anashirikiana na James Kasai” akasema Mathew

“Kwa maelezo haya uliyoyatoa hata mimi naweza kuamini hivyo” akasema Austin

“Kama ikiwa hivyo je kupigwa risasi Gosu Gosu kuna mahusiano yoyote na James Kasai?Kuna kitu alikigundua ndiyo maana wakataka kumuua?Mathew akauliza

“Lakini mwanamke Yule alionekana kuguswa sana na kitendo kile cha GosuGosukutaka kuuawa.Ni rahisi kumtambua mtu anayeigiza au anayeumia kutoka moyoni,Melanie

alionekana kuumia kutoka moyoni.Anaonekana kumpenda Gosu Gosu” akasema Austin

“Gosu Gosu alikutana vipi na huyo mwanamke? Mathew akauliza

“Kwa maelezo aliyoyatoa Lucy ambaye anaishi humu ndani na Gosu Gosu anadai kwamba Gosu Gosu alikwenda Ufaransa na aliporejea ndipo alipoanza kuonekana na huyo mwanamke.Swali linalokuja ni kwamba je alikutana nae Ufaransa?Je walikuwa na mahusiano kabla ya hapo?

Mwenye majibu ya maswali haya ni Gosu Gosu ambaye bado yuko hospitali na hawezi kutujibu maswali yetu” akasema Austin ukapita mfupi ukapita halafu Mathew akatoka akamuita Lucy mtumishi wa ndani

“Lucy samahani kwa kukusumbua.Nilikupa kazi ya kuchunguza katika chumba cha Gosu Gosu kutafuta picha ya mpenzi wake je umeipata?akauliza Mathew

“Hapana kaka sijafanikiwa kupata chochote.Hakuna picha

yoyote ya Yule mwanamke chumbani kwa Gosu Gosu”

“Unaweza ukakumbuka lini ilikuwa mara ya mwisho kwa Yule mwanamke kufika hapa nyumbani?

“Alifika hapa nyumbani asubuhi ya siku ile ambayo Gosu Gosu alipigwa risasi.Siku hiyo Gosu Gosu hakwenda kabisa kazini walijifungia chumbani baadae mwanamke huyo akaondoka.Ilipofika jioni Gosu Gosu akaondoka lakini hakuniambia anakwenda wapi hadi baadae nilipopata taarifa

za kuwa amepigwa risasi” akasema Lucy

“Ahsante Lucy unaweza kwenda” akasema Mathew

“Lucy ameweka wazi kwamba siku ya Gosu Gosu kushambuliwa mwanamke huyo alifika hapa asubuhi.Kuna kamera za ulinzi tupitie kumbu kumbu tujue gari alilotumia ili tuanze kulifuatilia” akasema Mathew na kuanza kupitia kumbu kumbu za kamera katika siku ambayo Gosu Gosu alipigwa risasi.

Gari moja la kifahari lenye rangi nyekundu lilionekana likiingia katika geti na Mathew akasimamisha picha ile ili waweze kuipata namba ya gari.Ruby akaiandika namba ile kisha akaitoa kompyuta yake katika mkoba na kuanza kazi.Mathew akahamia katika kamera iliyo mbele ya nyumba.Gari lile likaenda hadi mbele ya nyumba ile na kusimama kisha mwanamke mmoja akashuka.Aliinamisha sura yake chini wakati akielekea ndani

“Inaonekana alifahamu kuna kamera hapa ndiyo maana akainamisha kichwa ili asiweze kuonekana.She’s very smart ! akasema Mathew

“Ruby kuna chochote umekipata kuhusiana na hilo gari?akauliza Mathew na Ruby akaguna kidogo

“Kuna tatizo hapa.Namba hii imesajiliwa kwa jina la Stella kasamaki lakini jina hili halipo sehemu yoyote.Namaanisha halijasajiliwa katika taasisi yoyote ile” akasema Ruby

“Kwa lugha rahisi tunasema ni jina hewa” akasema Austin

“Exactly ! Ni hewa.Halipo” akasema Ruby na wote wakatazamana.Mara simu ya Austin ikaita akaipokea akazungumza na aliyempigia na mara sura yake ikabadilika

“Austin kuna nini?akauliza Mathew

“Gosu Gosu ! akasema Austin kwa wasi wasi

“Kafanya nini Gosu Gosu?akauliza Mathew

“Aliyenipigia simu ni kijana ambaye nimemuweka pale

hospitali kumlinda Gosu Gosu.Anasema hali ya Gosu Gosu imebadilika ghafla na ameondolewa haraka katika chumba alimokuwa amelazwa muda mfupi uliopita na hana uhakika kama ni mzima” akasema Austin

“Nini kimetokea tena?Mbona hali yake tayari ilikwisha kuwa nzuri?akauliza Mathew na wote wakatoka haraka wakaingia katika gari la Mathew wakaondoka kuelekea hospitali.Ukimya mkubwa ulitawala ndani ya gari.

“Listen to me guys” akasema Mathew

“Chochote kinaweza kutokea kwa Gosu Gosu hivyo nawaomba muwe na moyo mgumu.Kumbukeni tunayo kazi kubwa mbele yetu tujielekeze huko.Bado tunaendelea kumchunguza huyu mwanamke ambaye anashirikiana na Jame Kasai.Kabla ya kupata taarifa ya Gosu Gosu tulikuwa tumepata watu wawili wanaofanana karibu kwa kila kitu isipokuwa alama mbili.Mmoja anaitwa Melanie Chuma ambaye ana

alama tofauti na mwenzake ambaye naye jina lake ni Melanie lakini hana alama kama za Melanie Chuma.Kiwango cha kufanana cha watu hawa ni kikubwa sana hivyo kunifanya nihisi yawezekana wakawa ni mapacha lakini huyu Melanie mchumba wa Gosu Gosu nashawishika kuamini kwamba ndiye Yule hasa tunayemtafuta kwani yeye hana alama hizi alizonazo Melanie Chuma.Lakini wapi pa kuanzia kumtafuta?Hapo ndipo tumekwama" akasema Mathew

akiwa amekaa kiti cha nyuma na Ruby huku Austin akiwa katika usukani

“Mathew kuna kitu ninajiuliza.Ni vipi kama huyu ni mtu mmoja?akauliza Ruby

“Una maanisha nini Ruby?Austin akauliza

“Ninamaanisha ni vipi kama huyu Melanie mchumba wa Gosu Gosu na Melanie Chuma ni mtu mmoja?Kama alivyosema Mathew kiwango cha kufanana kwao ni kikubwa sana isipokuwa tofauti hizo mbili.Ninawaza yawezekana

akawa ni mtu mmoja ambaye anatumia majina tofauti ili kutuchanganya” akasema Ruby

“Hilo linawezekana kabisa.Hata mimi ninahisi hivyo yawezekana huyu Melanie ndiye huyu huyu Melanie Chuma.Wamefanana karibu kila kitu na hata majina yao ni Melanie.Yawezekana kama alivyosema Ruby akawa ni mtu mmoja lakini mwenye sura mbili tofauti”akasema Mathew

“Gosu Gosu angeweza kuzungumza angeturahisishia

sana kulifumbua fumbo hili” akasema Austin

“Gosu Gosu is not here.Tunatakiwa kujitahidi sisi wenyewe kuhakikisha tunampata huyu mwanamke” akasema Mathew na kunyamaza kidogo

“I have an idea.Ninaikumbuka tarehe ambayo Yule mwanamke aliwekeana saini na IS makubaliano ya kupokea fedha kwa niaba ya James Kasai.Ingia katika kumbu kumbu za wasafiri waliosafiri kupitia

uwanja wa ndege wa Julius Nyerere kati ya tarehe hizi tuone kama tunaweza kupata chochote” akasema Mathew na kumpatia Ruby tarehe ambazo alitaka achunguze wasafiri waliosafiri kupitia uwanja wa ndege wa Julius Nyerere.

“Ninaamini kama alisafiri kutokea Dar es salaam kwenda Dubai basi lazima itakuwa ni katika terehe hizo na lazima alipita katika uwanja huu” akasema Mathew na Ruby akiwa na kompyuta yake

akaanza kufanya kile alichoelekezwa na Mathew

Austin akiwa katika usukani alijitajidi kupita njia ambazo hazikuwa na msongamano mkubwa wa magari ili wawahi kufika hospitali

“Aaaaghhh !! akasema Austin kwa hasira baada ya kusimama katika taa za barabarani

“Relax Austin.”akasema Mathew

“Tunatakiwa kufika haraka hospitali kujua kilichomtokea Gosu Gosu” akasema Austin

“Hatuwezi kubadilisha chochote hata kama tukiwahi kufika.Ruby umepata chochote?

“Nisubiri kidogo.Mtandao unasumbua” akasema Ruby.Taa zikawaka na safari ikaendelea.Walipokaribia kufika hospitali Ruby akasema

“Tayari nimeipata orodha ya wasafiri waliosafri katika tarehe hizi kupitia uwanja wa ndege wa Julius Nyerere kuelekea nchi

mbalimbali.Nataka niipitie orodha hii kujua wale waliosafiri kwenda Dubai” akasema Ruby

“Good job Ruby.Keep looking” akasema Mathew wakati wakivuka geti la hospitali na kuelekea katika maegesho.Wote wakashuka na kukimbia kuelekea katika jengo la wagonjwa mahututi na kukutana na Yule jamaa ambaye Austin alimuweka kumlinda Gosu Gosu

“Jerry nini kimetokea?akauliza Austin

“Hata mimi nashangaa.Mgonjwa alikuwa anaendelea vizuri kabisa na tayari alikwisha fumbua macho.Timu ya madaktari walifika wakampima na kusema anaendelea vizuri wakashauri asisumbuliwe tumuache aendelee kupumzika ili arejewe na fahamu kamili.Baada ya kama nusu saa hivi akaja daktari mmoja akampima na kuchoma sindano katika chupa ya maji aliyotundikiwa halafu akatoka.Dakika chache baada ya kutoka nilisikia king’ora kikilia

katika chumba cha mgonjwa nikaingia ndani hakukuwa na muuguzi nikakimbia kwenda kuwatafuta wauguzi wengine wakaja mbio na madaktari na kumkuta mgonjwa akitapa tapa kitandani na mara akatulia wakasema moyo wake umesimama.Wakatumia mashine ya umeme ya kuustua moyo na mapigo ya moyo yakarejea halafu wakamuondoa ndani ya kile chumba na kumuingiza katika chumba hiki na mpaka sasa hawajatoka kunipa majibu yoyote.Nawaona

wakikimbia wakiingia na kutoka” akasema Jerry

“Ee Mungu tafadhali msaidie Gosu Gosu” akasema Ruby kwa masikitiko

“Okay guys let’s not panic.Hatujui kilichomtokea mwenzetu na hatujui kinachoendelea kuhusu hali yake.Tusubiri madaktari watakapomaliza kazi yao ya kuokoa uhai wake watatueleza nini kimetokea na vile vile tuwe tayari kupokea taarifa zozote ziwe nzuri au mbaya kwa sababu kwa hatua hii chochote

kinaweza kutokea.Tumshukuru Mungu kwa chochote kitakachotokea” akasema Mathew na kugeuka kutazama watu wakikimbia kuelekea sehemu Fulani

“Nini kimetokea kule watu wanakokimbilia?akauliza Mathew na mara mlango ukafunguliwa na madaktari watatu wakatoka wakikimbia nao wakielekea kule ambako watu walikuwa wanakimbilia.

“Kuna nini?Mbona wote wanakimbilia huko?akauliza Ruby.Wakati wakijiuliza

akatokea muuguzi akitokea upande ule watu waliokuwa wakikimbilia Mathew akamsimamisha na kumuuliza kumetokea nini kule ambako watu wanakimbilia

“Kuna mfanyakazi mwenzetu amejirusha ghorofani amefariki dunia”

“Nini sababu ya kujirusha? akauliza

“Hakuna anayejua” akasema Yule muuguzi aliyeonekana kuwa na haraka.

“Wakati tunaendelea kusubiri taarifa ya madaktari

Ruby tuendelee na lile zoezi” akasema Mathew na Ruby akaikunjua kompyuta yake akaendelea na kazi .Baada ya dakika tano akamuita Mathew aliyekuwa amesimama mbali kidogo na Austin wakizungumza.Wote wakaja mbio

“Kuna kitu nimekipata” akasema Ruby

“Nimempata mtu anaitwa Melanie Davis .Huyu aliondoka tarehe hii na ndege ya shirika la ndege la Emirates kuelekea Dubai”

“Melanie Davis ! Who is she ?Mathew akauliza na Ruby akaendelea kubofya kompyuta yake halafu akasema

“Huyu anatumia hati ya kusafiria ya Ufaransa” akasema Ruby

“Ni raia wa Ufaransa?Mathew akauliza

“Ili kulijua hilo natakiwa kuingia katika mtandao wa GCHQ na kudukua taarifa za Ufaransa kumtafuta huyu Melanie Davis ili kujua kama ni raia wa Ufaransa”akasema Ruby

“Hilo ni jambo la hatari sana Ruby.Hawa jamaa wanaamini tayari umekwisha fariki katika ajali ya ndege itakuwa ni hatari kubwa kwako wakijua kama uko hai bado” akasema Mathew

“Mathew usemacho ni kweli.Ninachotaka kufanya ni kitu cha hatari lakini tunahitaji sana kupata taarifa za Melanie Davis hivyo hatuna ujanja lazima nifanye hivyo”

“Unadhani hakutakuwa na tatizo kwa upande wako? Mathew akauliza

“Nitajaribu kutumia njia ambayo hawataweza kunigundua” akasema Ruby

“Sawa fanya hivyo” akasema Mathew na Ruby akaanza kucheza na kompyuta yake huku Mathew na Austin wakishuhudia.Wakati Ruby akiendelea na zoezi lile,madaktari wawili wakatoka akina Mathew wakawafuata.Wakajitambulisha kwamba wao ni ndugu za Gosu Gosu.Daktari mmoja aliyevaa kitambulisho kilichomuonyesha anaitwa Dr Masawe akawataka

waelekee sehemu kwa ajili ya mazungumzo.Ruby akakunja kompyuta yake akaongoza na akina Mathew hadi katika chumba maalum kwa ajili ya mikutano.Madaktari wakaongezeka na kufika wanne.Dr Masawe akasema

“Vijana wangu tumewaiteni hapa kuwapeni taarifa za kuhusiana na maendeleo ya mgonjwa wenu na kile kilichotokea.Usiku wa kuamkia leo hali yake ilibadilika na kuwa nzuri mifumo yake yote ilianza kufanya kazi vizuri kama

kawaida hivyo tukamuondoa katika mashine ya kumsaidia kupumua.Saa tano na dakika ishirini na moja tulijulishwa kwamba mgonjwa amefumbua macho tukaenda kumpima alikuwa anaendelea vyema tukatoa maelekezo aendelee kupumzishwa.Muda mfupi baadae tukaitwa tena kwamba hali ya mgonjwa imebadilika.Tukawahi na kumkuta akiwa ana hali mbaya na tukiwa pale moyo wake ukasimama ikatulazimu kuustua kwa kutumia mashine

ya umeme na kwa bahati nzuri ukaanza kufanya kazi tena.Tukamuondoa na kumpeleka katika chumba maalum tukaanza kumchunguza nini kimesababisha hali ile na tumegundua mgonjwa alichomwa sindano ya sumu kali" akasema daktari Yule na akina Mathew wakatazama

"Bado hatujajua ni sumu gani ,sampuli ya damu iko maabara hivi sasa ikichunguzwa kujua ni aina gani ya sumu alichomwa.Aliyefanya

kitendo hiki ni dhahiri alidhamiria kumuua kwa haraka lakini tunashukuru tuliwahi na tukaokoa maisha yake”

“Thank you lord ! akasema Mathew kwa sauti ndogo

“Suala hili tayari tumelifikisha katika kitengo cha usalama hapa hospitali wameanza kulifanyia kazi ili tujue nani aliyemchoma mgonjwa sindano yenye sumu.Tutawajulisheni kila hatua itakayochukuliwa”

akasema daktari na Mathew akasimama

“Daktari kwanza kabisa tunashukuru sana kwa jitihada kubwa ambazo mmekuwa mkizifanya kuokoa maisha ya ndugu yetu.Kuhusiana na tukio la leo tunaye kijana wetu ambaye tulimuweka hapa kwa ajili ya ulinzi wa mgonjwa wetu ambaye ametueleza kwamba muda mfupi baada ya timu ya madaktari kutoka kumpima mgonjwa na kuelekeza apumzike, aliingia dakari mwingine na kuchoma sindano

katika chupa ya maji aliyokuwa ametundikiwa mgonjwa na muda mfupi baadae ndipo hali ile ikajitokeza.Kama mtaruhusu tunaweza kumuita akaeleza nini kilitokea” akasema Mathew na daktari akaruhusu kijana Yule aitwe.Austin akatoka haraka akaenda kumchukua Jerry akamleta katika kile chumba.Jerry akaeleza ilivyokuwa na kueleza muonekano wa daktari huyo.Ikalazimu mtu anayeshughulika na masuala ya wafanyakazi wote wa hospitali

ile aitwe akafika na kompyuta yake na Jerry akamuelezea muonekano wa huyo daktari aliyemchoma GosuGosu sindano ya sumu

“Kuna wafanyakazi mia nne na ishirini katika hospitali hii.Siwezi kuwafahamu wote labda tujaribu kukaa na kupitia mfanyakazi mmoja mmoja ili aweze kumtambua huyo daktari aliyefanya huo uhalifu” akasema Yule meneja

“Kuna njia rahisi ya kuweza kumtambua huyo daktari” akasema Mathew na

kuomba apewe karatasi na kalamu akaanza kuchora picha ya huyo daktari aliyemchoma sindano Gosu Gosu kwa kufuata maelezo ya Jerry.Baada ya dakika kumi picha ikawa tayari Mathew akamuonyesha Jerry ile picha

“Mungu wangu ! akasema Jerry kwa mshangao mubwa.Hakuamini kile alichokiona

“Ni huyu huyu ambaye aliingia na kumchoma sindano mgonjwa” akasema Jerry.Mathew akawaonyesha

madaktari wale picha ile aliyoichora na wote wakabaki na mshangao mkubwa.

“Dr Sebastian Makebu” akasema Dr Masawe.

“Huyu ni daktari wetu anayehusika na dawa za usingizi.Kijana una uhakika ni huyu?akauliza DrMasawe

“Ni yeye”akajibu Jerry bila woga

“Kwa nini Dr Seba akafanya kitendo kama hiki?akauliza Dr Masawe na kupiga simu katika idara ya usalama pale hospitali na kuagiza Dr Sebastian

Makebu kutafutwa haraka sana na kukamatwa kama yuko katika maeneo ya pale hospitali

“Dr Masawe kuna kitu kingine ninataka kuuliza.Karibu muda wote huwa hapakosekani muuguzi katika chumba kile cha Gosu Gosu.Nini kimetokea leo hadi daktari huyu akaweza kuingia na kufanya kile alichokifanya? Mathew akauliza

“Ni kweli.Mgonjwa wenu ni mmoja wa wagonjwa wanaopewa kipaumbele kikubwa sana hapa hospitali kwani Rais alipiga simu na

kuagiza kwamba kila juhudi zifanyike kuhakikisha mgonjwa huyu anahudumiwa vizuri na maelekezo yakatolewa kusikosekane muuguzi katika chumba chake na ndivyo inavyokuwa kila siku toka ameletwa hapa.Hata mimi nashangaa leo kumetokea nini kusiwe na muuguzi mle chumbani hadi akaingia huyu kijana na kufanya hiki alichokifanya.Kuna mtu mmoja ambaye tungeweza kumuuliza nini kimetokea hadi chumbani kwa Gosu Gosu kusiwe na

muuguzi lakini kwa bahati mbaya wakati tukiendelea kumuhudumia mgonjwa wenu tukapokea taarifa kwamba mkuu wa wauguzi hapa hospitali amejirusha ghorofani na kufariki dunia.Sijui nini kinaendelea hapa" akasema Dr Masawe na simu yake ikaita akaipokea akazungumza halafu akawatazama akina Mathew.Sura yake ilionyesha wazi kuna kitu hakiko sawa

"Nimetaarifiwa na idaraya ulinzi kwamba Dr Sebastian tayari amekwisha toka nje ya

hospitali.Alipita getini na akasaini kutoka.Nimejulishwa pia kwamba muuguzi ambaye alitakiwa kuwepo katika chumba cha Gosu Gosu amekutwa sasa hivi akiwa amefariki chooni.Sifahamu ni mambo gani yanaendelea hapa hospitali. Vyombo vya dola vitatusaidia katika suala hili lakini ninawahakikishia kwamba Dr Sebastian atapatikana tu.Hawezi kukwepa mkono mrefu wa dola.Ahsanteni sana kwa kutusaidia tumeweza kupata

mwanga wa nini kilitokea na nani amefanya.Tukiliweka pembeni suala hilo kwa muda kuna suala lingine muhimu sana ambalo mnatakiwa mlifahamu” akasema Dr Masawe.

“Kufuatia sumu kali aliyochomwa Gosu Gosu kuna tatizo kubwa limejitokeza.Ini lake linashindwa kufanya kazi hivyo basi anahitaji kupandikizwa ini haraka iwezekanavyo ama sivyo atapoteza maisha”

“Jesus ! akasema Ruby

“Najua nimewastua sana vijana wangu lakini huo ndio ukweli.Ili kuokoa maisha ya mwenzenu lazima kumfanyia upasuaji na kumpandikiza ini.Bila kufanya hivyo tutampoteza” akasema Dr Masawe

“Daktari unadhani Gosu Gosu ana muda gani wa kuweza kuishi kuanzia sasa?Mathew akauliza

“Kwa hali aliyo nayo sasa ninaweza kusema kwamba ana saa arobaini na nane kama

asipopandikizwa ini atakufa” akajibu Dr Masawe.

“Ni muda mfupi sana huo tutapata wapi ini la kumpandikiza? Tunaweza kupata ini hapa hospitali?akauliza Mathew

“Hapa hospitali ni vigumu kwani kuna orodha ndefu ya wagonjwa wanaohitaji kupandikizwa ini lakini idadi ya wanaojitokeza kuchangia ini ni ndogo sana au niseme hakuna kabisa” akasema Dr Masawe.

“Unatushauri nini mzee?Mathew akauliza

“Anatakiwa mmoja wenu ajitolee kumchangia ini mwenzu.Si lazima awe ni ndugu wa damu mtu yeyote ambaye yuko tayari kujitolea ini kwa ajili ya huyu mwenzenu atapimwa na akionekana ini lake linafaa basi kitachukuliwa kipande na kupandikizwa kwa mgonjwa.Ni upasuaji ambao unaweza kuchukua saa tano au zaidi”

“Endapo ini hilo likipatikana upasuaji huo unafanyika hapa hapa hospitali

au nadi nje ya nchi?akauliza Mathew

“Tunapandikiza hapa hapa hospitali” akajibu Dr Masawe

“Vijana kujitolea ini kuokoa maisha si kitu cha hatari kabisa japo wengi wanaogopa.Tunachukua kipande kidogo cha ini safi tunakipandikiza katika ini la mgonjwa.Baada ya miezi mitatu ini litarejea katika hali yake ya kawaida” akasema Dr Masawe.Mathew akawaomba madaktari wale wawape dakika mbili wakajadiliane

“Guys kwanza kabisa tunashukuru kwa Gosu Gosu kuwa hai mpaka sasa.Jaribio la kumuua limeshindwa lakini bado yuko kwenye hatari kama asipopata ini.Sisi ndio ndugu zake hivyo inabidi kufanya kila tuwezalo kuokoa maisha yake.Binafsi ninajitolea kupimwa na kama nikikutwa ninaweza kutoa ini basi nitafanya hivyo kuokoa maisha ya Gosu Gosu”akasema Mathew

“Hapana Mathew.Wewe hupaswi kuwa kitandani.Wewe ni mtu muhimu sana kwa

sasa.Niache mimi nikapimwe na kama ikionekana ninafaa basi nitolewe mimi ini ili wewe na Ruby muendelee na operesheni” akasema Austin

“Nadhani Austin yuko sahihi.Mathew hutakiwi kulala kitandani kwa muda huu.Kumbuka una siku saba tu za kuhakikisha unampata James Kasai “ akasema Ruby

“Sawa Austin.Nalikubali wazo lako.Wakati vipimo vikiendelea mimi na Ruby tutaendelea na operesheni ambayo kwa sasa inazidi

kutanuka kwani tunatakiwa kumpata huyo mtu aliyetaka kumuua Gosu Gosu kwa sumu ambaye nina uhakika mkubwa ametumwa afanye hivyo” akasema Mathew wakarejea ndani ya kile chumba na wakawajulisha madaktari kwamba Austin amejitolea kutoa ini litakalopandikizwa kwa Gosu Gosu.

“Dr Masawe nahitaji kufahamu huyu daktari Sebastian anaishi wapi?akauliza Mathew na kuelekezwa kisha wakaondoka pale hospitali na

kumuacha Austin akijiandaa kwa ajili ya kupimwa.

“Ruby kuna picha inaendelea kujitengeneza kufuatia hiki kilichomtokea Gosu Gosu.Kuna watu wanataka auawe.Naamini kuna kitu anakifahamu ndiyo maana watu hao hawataki apone na wakamtumia huyo Dr Sebastian ili akamchome sindano ya sumu afe.Kifo cha muuguzi mkuu na muuguzi aliyekuwa akimuuguza GosuGosu vinahusiana na hiki kilichomtokea Gosu Gosu.Naamini kabisa kwamba

Dr Sebastian alimtumia muuguzi mkuu kumuondoa muuguzi katika chumba kile cha Gosu Gsou ili aweze kupata nafasi ya kwenda kumchoma sindano ile ya sumu na wauguzi wale wawili wameuawa ili kuharibu uchunguzi" akasema Mathew akiwa katika usukani wakielekea nyumbani kwa Dr Sebastian

"Kwa vyovyote vile lazima mwanamke huyo ambaye anadai ni mchumba wa Gosu Gosu anahusika na hiki kilichomtokea Gosu Gosu na

ndiyo maana ametoweka na hajulikani alipo.Umefanikiwa kupata taarifa za Yule Melanie Davis?akauliza Mathew

“Nimekwisha sahau kama nina kazi kubwa ya kufanya.Nimejielekeza katika suala la Gosu Gosu” akasema Ruby na kuikunjua komputa yake akaanza tena kazi.

“Melanie Davis na Melanie Chuma ! akawaza Mathew

“Hawa ni watu wawili tofauti au ni mtu mmoja? Akajiuliza

“Ngoja tuendelee na uchunguzi tutaupata ukweli” akawaza Mathew akiendelea kukanyaga mafuta

“Mathew unaweza ukasimamisha gari?Kuna kitu nataka uone” akasema Ruby na Mathew akatafuta sehemu nzuri akasimamisha gari .

“Kuna nini Ruby?akauliza Mathew

“Nimepata taarifa za Melanie Davis” akasema Ruby na kumpa Mathew kompyuta ili asome

“It’s her ! akasema Mathew baada ya kuiona picha ya Melanie Davis

“Huyu ndiye Yule mwanamke niliyekuwa ninamzungumzia.Huyu ndiye ambaye nilimshuhudia Dubai akisaini makubaliano ya kupokea fedha kwa niaba ya James Kasai. Hata ukitazama sura yake haina kovu lolote ni kama ile picha niliyoichora” akasema Mathew

“Taarifa inaonyesha anaitwa Melanie Davis.Ni raia wa Ufaransa mwenye asili ya

jamhuri ya kidemokrasia ya Congo”

“Melanie Davis ana asili ya Congo ! Mathew akashangaa na kuendelea kusoma ile taarifa na kuimaliza

“Taarifa inaonyesha Melanie Davis ana utajiri mkubwa aliorithi kutoka kwa wazazi wake waliofariki katika ajali.Anatajwa kuwa miongoni mwa mabilionea wenye umri mdogo lakini haijaonyesha anamiliki miradi au biashara zipi nchini Ufaransa na hata wazazi wake hawajatajwa kwa

majina ili tujue walikuwa wanamiliki miradi ipi.Bado kuna ukakasi kuhusu huyu Melanie Davis”akasema Mathew

“Ninajiuliza kama anatajwa kuwa miongoni mwa mabilionea wakubwa nchini Ufaransa amekuja kutafuta nini Tanzania? Akauliza Ruby

“Yawezekana amewekeza hapa Tanzania na ndiyo maana IS wanapitisha fedha kwake.Ninadhani hata vyombo vya fedha havijaweza kuwa na mashaka naye kwa vile ni mtu mwenye utajiri mkubwa.Ruby

tutaendelea baadae kuwachimba hawa watu wawili Melanie Davis na Melanie Chuma.Kwa sasa tuwahi nyumbani kwa Dr Sebastian” akasema Mathew na kuingia barabarani wakaendelea na safari

“Melanie Davis ambaye ninaamini ndiye aliyesaini makubaliano ya fedha na IS na ndiye tunayeamini ni mchumba wa Gosu Gosu anatokea Ufaransa.Gosu Gosu naye alikwenda Ufaransa na baada ya kurejea ndipo akaanza

kuonekana na huyo mwanamke.Ni vipi mahusiano yao yalianza? Je walikutana Ufaransa? Nini anakifanya huyu mwanamke hapa nchini ? Melanie Chuma amefanana naye kwa kila kitu je wana undugu au imetokea tu wakafanana? Au ni mtu mmoja? Haya yote baadae kwa sasa ngoja tumsake kwanza huyu daktari aliyetaka kumuua Gosu Gosu" akawaza Mathew

Walifika katika nyumba anakoishi Dr Sebastian kwa mujibu wa maelekezo

waliyopewa kule hospitali.Ni nyumba ambayo ilikuwa na uzio wa maua na geti la bati.Mathew na Ruby wakashuka garini na kuliendea geti kwa tahadhari kubwa.Akajaribu kulisukuma geti halikuwa limefungwa wakaingia ndani.Taratibu wakaelekea hadi katika mlango mkubwa wa kuingilia ndani ulikuwa umefungwa.Mathew akazunguka nyuma ya ile nyuma ambako kulikuwa na mlango mwingine akajaribu kuufungua nao ulikuwa

umefungwa.Akatoa vifaa Fulani vidogo na kuvichomeka katika kitasa akaufungua mlango wakaingia ndani wakaanza kukagua vyumbani.Katika chumba kikubwa cha kulala wakakuta vitu vimepanguliwa hovyo..Kabati la nguo lilikuwa tupu

“Tumechelewa.He’s gone.Inaonekana baada ya kufanya kitendo kile alikuja hapa na kuchukua vitu akaondoka haraka.Unaweza ukajua mara ya mwisho alizungumza na nani?akauliza

Mathew wakatoka na kurejea katika gari Ruby akachukua kompyuta yake na kuziingiza namba za Dr Sebastian katika program maalum na baada ya dakika mbili akasema

“Aliwasiliana na mtu anaitwa Salome Mtete” akasema Ruby na kuufungua ujumbe huo

“Unaweza ukafuatilia na kujua mahala alipo?akauliza Mathew na Ruby akafungua program nyingine akamtafuta huyo mtu aliyewasiliana naye

mara ya mwisho akaweza kujua mahala alipo.

“Samawati tower” akasema Mathew kisha akaondoa gari wakaondoka.

MPENZI MSOMAJI MATHEW MULUMBI TAYARI AMEANZA KAZI ILIYOMLETA TANZANIA USIKOSE SEHEMU IJAYO….